ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 27 Septemba, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 126

Kurudishwa kwa Mfumo wa Kujitolea kwa Wafanyakazi Kabla ya Kuajiriwa

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Serikali hutangaza nafasi za kazi na kuajiri hapo kwa hapo wakati hapo zamani serikali ilikuwa ina wafanyakazi wa kujitolea kati ya kipindi cha miezi sita na kumfahamu mfanyakazi yule vizuri.

a) Je, serikali haioni umuhimu wa kurudisha ule mfumo wa zamani wa kujitolea kwanza halafu ndio unaajiriwa.

b) Je, serikali haioni kuwa wafanyakazi hao watasaidia ufanisi zaidi katika maeneo ya kazi ikiwemo hospitali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 126 lenye vifungu (a) na (b), lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, katika miaka iliyopita baadhi ya Taasisi za Utumishi wa Umma zilitumia utaratibu huu wa kujitolea katika Utumishi wa Umma na kuchukua wafanyakazi kwa njia ya kujitolea.

Hata hivyo, kutokana na kuanzishwa kwa zoezi la Mageuzi ya Utumishi wa Umma lililopelekea kuandaliwa na kupitishwa kwa Sera ya Utumishi wa Umma

ya mwaka 2010, Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011, na hatimaye Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, utaratibu wa kujitolea kwenye Mawizara na Taasisi za Umma umepigwa marufuku. Kwa mujibu wa Kanuni ya 134 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi hatoruhusiwa kuweka wafanyakazi wa kujitolea katika taasisi yake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, serikali haioni umuhimu wa kurudisha utaratibu wa zamani wa kujitolea ndani ya taasisi kabla ya kuajiriwa, kwa sababu mfumo huu wa ajira unakiuka Sheria ya Utumishi wa Umma iliyoweka utaratibu maalum wa ajira, unasisitiza kutangazwa nafasi ya ajira katika vyombo vya habari vya umma, ili wananchi wenye sifa wapate fursa ya kuomba, kukusanya maombi, kufanya uteuzi kwa ajili ya usaili na baada ya usaili kuwapata vijana ambao watapatiwa vibali vya ajira. Katika hali hiyo, na kwa misingi ya utawala bora haitakuwa busara na wala haitawezekana kufanya ajira nje ya utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu wa kufanya kazi kwa kujitolea unamnyima mtumishi kupata malipo halali kwa kazi aifanyayo wakati anapojitolea, na kwamba zinapopatikana nafasi za ajira, utaratibu huu hautoi fursa sawa baina ya vijana wanaojitolea na wale wenye sifa nzuri zaidi ambao hawajajitolea, na kwa kuwa utaratibu huu umekatazwa ndani ya Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma, serikali haioni kwamba utaratibu huo utaleta ufanisi zaidi katika maeneo ya kazi.

   Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka niulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Ingawa Mhe. Naibu Waziri, amejibu kwamba kuna kifungu ambacho kimekataza kuhusu kuajiri kwa muda. Lakini kuna baadhi ya wizara ama idara bado inaonesha kwamba kuna watu hawajaajiriwa rasmi na wanafanya hizo shughuli zao katika mikataba midogo.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri, anao uhakika kwamba katika wizara na idara watu wote waliomo katika wizara zile wameajiriwa rasmi.

(b) Kama wafanyakazi hao wapo na wameshatumikia katika kipindi kirefu na serikali yetu ina mipaka ya kuajiri kwenye miaka 25. Watu wale munawasaidia vipi, kwa ajili ya kukidhi haja jinsi walivyojitolea katika taifa lao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika,

(a) Suala la kwamba tuna uhakika ya wale wote ambao wanaofanyakazi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba wameajiriwa, uhakika huo tunao kwa sababu mtu anatakiwa kufanyakazi kwa yule ambaye ameajiriwa.

(b) Kuhusiana na wale watu ambao wanajitolea katika taasisi za serikali ni kwamba, sheria imezungumzia kuwa hairuhusiki kuweka watu hao kwa njia ya kujitolea. Lakini ikumbukwe kwamba, katika hali ya kawaida kwenye jamii zetu tunavyoishi za Kizanzibari, iwapo pale kuna haja ya kutaka mtu kusaidia basi anasaidia.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, naelewa kwamba Mhe. Mwakilishi, amelenga zaidi katika Wizara ya Elimu. Kweli, Wizara ya Elimu kuna vijana wengi ambao wanajitolea, lakini kujitolea kwao kule hakusababishi kwamba serikali iwe imejifunga katika kuwaajiri. Kwa mfano, unapowaweka wale watu na kwamba sheria inawatambua, inamaana kwamba utakapotoa ajira lazima watu wale waweze kuajiriwa.

Lakini kwa kifungu hiki cha sheria ambacho kipo katika Sheria zetu za Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni yale, inamaanisha kwamba hata kama watu watakuwa wanajitolea, lakini haitoibana serikali kwamba lazima watu hawa waajiriwe pale ambapo zitakapotolewa hizo ajiriwa. Isipokuwa watu hawa ambao wanajitolewa hivi sasa, wana haki na fursa sawa na wale ambao hawajajitolea na mara pale ambapo nafasi ajira zinapotokezea hawa wote wanaangaliwa katika jicho moja, yaani wote wanakuwa na fursa sawa za kufanya maombi ya kuomba na baadaye kupatiwa hizo nafasi.

Kwa hivyo, kujitolea kwao huku hakusababishi kwamba zinapotokea hizo ajira lazima wao wawe wanapata hizo nafasi na wengine kuachwa na wote wanakuwa na fursa sawa na wanatakiwa kuomba na hatimaye baada ya uchaguzi wale ambao wataonekana kuwa na sifa za kustahiki kuajiriwa wanaajiriwa. *(Makofi)*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa amesema kwamba katika kifungu cha Sheria ya Utumishi kuna katazo la kuwa na wafanyakazi wa kujitolea na katika taasisi nyingi za serikali wafanyakazi hao wapo. Je, serikali itachukua hatua gani kwa watendaji wa taasisi hizo. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Mjumbe, arejee swali lake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Yussuf Hassan Iddi, rudia swali lako.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba, amesema katika kifungu cha Sheria ya Utumishi kuna katazo la kuwa na wafanyakazi wa kujitolea na katika taasisi nyingi za serikali wafanyakazi hao wapo. Je, serikali itachukua hatua gani kwa watendaji wa taasisi hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, narejea kusema kwamba sheria na kanuni zilizopo zinakataza wafanyakazi wa kujitolea katika taasisi zetu. Lakini naomba ifahamike kwamba katika hali ambayo Wazanzibari tunayo ya uzalendo na wanaona kwa kiasi fulani kukaa hivi hivi elimu yao inaweza ikapotea. Kwa hivyo, si busara kusema kwamba kwa mfano walimu hawa ambao wanaojitolea moja kwa moja tuweze kuwafukuza hapana, kwa sababu wanatusaidia.

Kwa maana hiyo, kwa dhana ile ya uzalendo walimu hawa ambao wanajitolea, basi waachiwe waendelee na uzalendo wao wa kujitolea na pale ambapo fursa zitatokezea za ajira, ni vyema na hawa wakapata ile fursa ya kuomba kama wanavyoomba wenzao, ili waweze kupata ajira.

Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa tu, hivi sasa tunao walimu ambao wanajitolea na katika harakati za kuhakikisha walimu wa sayansi wanaajiriwa hivi sasa, kwa kweli idadi ambayo ipo pale na tayari wameshafanyiwa usaili, idadi

iliyopatikana wamo wale ambao waliojitolea na wasiokua hawakujitolea, lakini wote wameorodheshwa na watapatiwa hizo nafasi hivi karibuni.

Kwa hivyo, ipo haja ya hawa watu ambao wanaojitolea tuthamini jitihada zao za uzalendo wao kujitolea. Mhe. Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na kwa ruhusu yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la wafanyakazi katika sehemu mbali mbali wanaojitolea ni wengi na mara nyingi zinapotokea ajira huwa hawaonekani, pamoja na Mhe. Naibu Waziri, alivyosema kwamba watapewa kipaumbele, lakini mara nyingi hupigwa buti na wakawa hawafikii karibu.

Je, kwa kuwa orodha zimo katika wizara, maidara pamoja na mashirika, hivi Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina mpango gani wa kuwaorodhesha wafanyakazi wote wanaojitolea kuwaweka katika orodha maalum, ili inapotokea haja wasitangaze ajira nyengine isipokuwa wawaajiri wale kwa ajili ya kuondosha usumbufu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, wazo la Mhe. Mwakilishi, tunalichukua na pale ambapo tunaona upo umuhimu wa kufanya hivyo, basi tutalifanyia kazi. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Nam. 78

Kupelekwa Askari wa Vikosi Wilaya ya Micheweni

Mhe. Shamata Shaame Khamis – Aliuliza:-

Naipongeza sana serikali yetu inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kutekeleza ahadi ya kuweka amani na utulivu nchini, pamoja na jitihada za Jeshi la Wananchi na Jeshi la Polisi, lakini pia na jitihada na ukakamavu mkubwa wa Vikosi vya SMZ.

Kwa kuwa Vikosi vya SMZ vimekuwa na Makao Makuu yake kila Wilaya kwa upande wa Pemba, jambo ambalo limesaidia sana kufanikisha pia azma hii ya serikali ya kulinda amani na utulivu.

Je, ni lini serikali itaweka Makao Makuu ya Wilaya ya Vikosi vya SMZ katika Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 78 kama ifuatavyo:-

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi tayari kinamiliki eneo katika Wilaya ya Micheweni, ambalo tayari limeshapimwa na kupatiwa hatimiliki. Kikosi kimeshawalipa fidia wakulima waliokuwa wakilitumia eneo hilo mwaka huu wa fedha 2016/17. Kikosi kinatarajia kulizungushia uzio eneo hilo na kuanza ujenzi wa kituo hicho.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Kikosi cha KMKM kwa Wilaya ya Micheweni hatuna Makao Makuu ya Wilaya, lakini tunacho Kituo kidogo cha KMKM kilichopo Msuka (Wilaya ya Micheweni), ambacho kinatosheleza kufanya kazi zake za ulinzi na usalama baharini vizuri dhidi ya aina yoyote ya magendo kwa wilaya nzima.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Naibu Spika, napenda nimuulize tena Mhe. Waziri, swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa amesema kwamba katika Wilaya ya Micheweni tayari Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeshakuwa na eneo na pia kimeshapata hatimiliki na shughuli wakati wowote inaweza ikaanza kwa hatua za ujenzi. Lakini katika maeneo hayo ya Wilaya ya Micheweni liko jengo ambalo limeanzishwa kipindi kirefu sana na Kikosi cha KVZ. Je, ni lini jengo hilo litakamilika, ili tuone huduma zinaanza kupatikana.

Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa katika eneo la Micheweni tunacho Kituo cha Kambi ya KVZ, yaani Kikosi cha Valantia Zanzibar na ujenzi ulianza tokea mwaka wa bajeti uliopita na hivi sasa ujenzi huo umeshafika hatua ya kuweka *lintel* na kumalizia kazi hiyo. Kwa hivyo, tunatarajia mara tu baada ya kupata fedha kutoa serikalini na fedha zinazotokana na vianzio vyengine vya mapato, basi tutalikamilisha jengo hilo, ili kikosi chetu kiweze kufanya kazi vizuri katika Wilaya hii ya Micheweni.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya serikali, naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Kikosi cha Zimamoto ni kikosi muhimu sana kwa maisha ya binaadamu na Wazanzibari kwa jumla. Lakini kwa vile Kikosi hicho cha Zimamoto makao yake ya Pemba yanaishi katika hali ngumu tena ya kusikitisha. Je, Mhe. Waziri, ana taratibu zipi za kuweza kuwapatia makazi bora wafanyakazi wale wa eneo la Wete, Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wapiganaji wetu wa Kikosi cha Zimamoto wanaishi katika mazingira sio mazuri sana. Hata hivyo, serikali inao mpango mzuri sana wa kuweza kukipatia fedha Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ili waweze kuimarisha majengo yao katika vituo vyote vya Unguja na Pemba.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, swali dogo la nyongeza.Mhe. Waziri amesema kwamba kumeshapimwa kiwanja cha Zimamoto, lakini Wilaya ya Micheweni ni kubwa. Je, kiwanja hicho kiko jimbo gani na ni eneo gani hasa tunataka kujua kama wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu swali mama kwamba kiwanja hicho kipo katika eneo la Micheweni kama alivyouliza Mhe. Shamata Shaame Khamis, muuliza swali. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba nilipojibu swali la msingi na swali la nyongeza wananchi wa Zanzibar wamejua kwamba kiwanja hicho cha Zimamoto kiko katika Jimbo la Micheweni, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba. *(Makofi)*

Nam. 181

Kuhusu Ujenzi wa Jengo la Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Ujenzi wa jengo la Afisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi bado halijaanza tangu kuvunjwa kwa jengo la zamani.

Je, ni sababu zipi zinazopelekea ucheleweshaji wa ujenzi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 181 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakiri kuwa ni kweli ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi haujaanza tangu kuvunjwa kwa jengo la zamani. Aidha, napenda kumjuilisha kuwa taratibu zote za awali zinazohusinana na ujenzi wa jengo hilo zimeshakamilika. Sababu kubwa iliyoifanya ujenzi huo kuchelewa kuanza ni ukosefu wa rasilimali fedha. Hata hivyo, serikali hivi sasa inaendelea kufanya mazungumzo na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*) pamoja na Kampuni ya *AFCON* ya Israel na wenzetu wa Afrika ya Kusini juu ya namna ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mhe. Naibu Spika, mazungumzo hayo pia yameshirikisha Shirika la Nyumba la Zanzibar. Mazungumzo hayo kwa sasa yamefikia katika hatua nzuri na ni matarajio yetu kuwa muda si mrefu tutafanikiwa na hatua za ujenzi zitaanza rasmi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza. Katika jambo ambalo tunaona aibu sisi wengine katika Mkoa wetu ni suala la jengo la Makao Makuu ya Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa kuwa katika eneo hilo ni karibu na uwanja wa Taifa wa Amani ambapo sherehe mbali mbali zinafanywa na tunashuhudia kuwekwa mabati katika eneo lile ni moja ya kuondoa mandhari ya eneo hilo.

Sasa kwa kuwa Mhe. Waziri, amenijibu kuwa rasilimali fedha hazipo, kwa nini wizara ilichukua hatua za haraka kulibomoa jengo lile kabla hawajajiandaa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kuzungushwa mabati ni sehemu moja ya kuanza ujenzi wa jengo ambalo tumelikusudia kulijenga, lakini pili, kwa nini tumeamua kulivunja jengo la zamani. Tuliamua kulivunja jengo la zamani kwa sababu kwanza hilo jengo lilikuwa halitumiki kwa shughuli za wilaya, wala mkoa, lakini pia lilikuwa halina uwezo wa kuweza kuwaweka watumishi na wakaweza kufanya kazi zao pale.

Kwa hivyo, Mheshimiwa, aelewe tu kwamba tulivunja kwa nia ya kutaka kujenga jengo jipya na lengo ni kulijenga ili wafanyakazi wetu waweze kupata mazingira mazuri ya kufanyia kazi, lakini kwa sababu ya rasilimali fedha

ndicho kilichotupelekea mpaka sasa hivi tukawa hatujaweza kulijenga jengo lile.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini na mimi nataka kuuliza kwamba, kwa pale tunapotaka kujenga ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni wazo zuri na mikakati mizuri, lakini pana jengo pale la mtu binafsi ambalo nahisi serikali imelizuwia kujengwa kwa sababu linachungulia *VIP*. Mhe. Waziri, anaonaje wakafanya mazungumzo na yule mwekezaji binafsi lile jengo wakauziwa serikali ikali-*develop* lile jengo, ikai-*modernize* na pale palipozungushwa mabati ikawa *garden* ya ofisi mpya ya Mkuu wa Mkoa. Kwa sababu jengo lile kuweko pale sio vyema kwani linachungulia *VIP* ambako viongozi mbali mbali wa ndani na nje wa kitaifa huwa wanakuja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, wazo lake ni zuri sana na serikali ilishalifanyia kazi hilo wazo ambalo amelitoa leo la kukaa na mmiliki wa jengo na kumshawishi atuuzie. Bado mazungumzo yanaendelea na mmiliki wa jengo ili akubali kutuuzia jengo lile. Jambo linalocheleweshe mpaka sasa hivi bado hatujakubaliana bei ambayo anaitaka mmiliki na bei tunayoihisi sisi kwa mujibu wa thamani ya jengo lilivyo hatujafikia muwafaka bado.

Kwa hiyo, pale tu atakapoamua kutuuzia kwa bei tutakayokubaliana tunaweza tukalifuata tukalitekeleza hilo wazo lake, lakini kwa vile bado hatujafikia muwafaka kwa mmiliki wa jengo basi azma yetu itabakia katika azma yetu ya awali ya kujenga katika kiwanja chetu ambacho kinamilikiwa na serikali.

Nam. 65

Ushirikishwaji wa Wananchi katika Kupanga Maendeleo ya Nchi

Mhe. Simai Mohammed Said (Kny. Mhe. Salma Mussa Bilal) – Aliuliza:-

Serikali imekua ikipanga bajeti kila mwaka kwa ajili ya shughuli mbali mbali za maendeleo ya wananchi.

Je, serikali inawashirikisha vipi wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa maendeleo hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali Nambari 65 la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Bajeti ni zana inayotumiwa na serikali ili kupanga na kugawa rasilimali zake kwa sekta mbali mbali kwa mujibu wa vipaumbele na mahitaji muhimu ya jamii kama yalivyoelekezwa katika mipango yake ya maendeleo. Kuna utaratibu tofauti unaotumiwa na serikali duniani katika kuwashikisha wananchi katika upangaji wa bajeti, ama moja kwa moja au kwa utaratibu wa uwakilishi.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inatumia zaidi utaratibu usio wa moja kwa moja kwa kutumia njia ya uwakilishi na ushirikishwaji katika kupanga mipango ya maendeleo, ambapo bajeti inaweka mgao wa fedha za kuitekeleza. Ushirikishwaji huo huwa wa wananchi katika mipango na bajeti huwepo katika taratibu zifuatazo:

Moja kwa hapa Zanzibar tunatumia utaratibu wa uwakilishi wa wananchi kupitia uandaaji wa mipango ya kitaifa kama (DIRA ya 2020), (MKUZA) na mipango mingine ambapo wananchi wanashirikishwa kutoa maoni yao, lakini vile vile kupitia Ilani ya Vyama vya Siasa. Wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu aghalabu hutenguliwa na kuibua mambo mbali mbali ambayo ama yanawatatiza wananchi au wananchi wangependa yashughulikiwe ili kuwaletea maendeleo yao.

Kwa utaratibu uliopo, serikali iliyopo madarakani hutekeleza Ilani ya Chama kilichoshinda uchaguzi. Utekelezaji wa ilani, kwa hivyo, huingizwa katika Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya wananchi.

Njia nyengine ni Majukwaa pamoja na vikundi kazi. Serikali imekuwa ikiandaa majukwaa mbali mbali kama vile Maabara "*lab*", zinazokaa na kujadili maeneo mbali mbali yanayotakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka zaidi, ama yale maeneo yenye changamoto pamoja na mikakati ya utatuzi wa changamoto hizo.

Vile vile, kuna Majukwaa ya kila Mwaka. Mhe. Naibu Spika, kumekuwepo na utaratibu wa serikali wa kukutana kila mwaka na wadau mbali mbali wanaojihusisha na kazi za uchumi ndani ya Zanzibar, kujadili juu ya masuala mbali mbali ya mageuzi ya mfumo wa kodi ambao ni eneo muhimu katika bajeti. Aidha, kupitia Tume ya Mipango, Masheha wamekuwa wakishirikishwa moja kwa moja katika kupata taarifa na maoni ya wananchi katika shehia zao.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Kamati za Baraza la Wawakilishi, Wajumbe tuna jukumu na wajibu wa kuchukua maoni ya wananchi na kuyawasilisha katika Baraza hili ili serikali ipate kuyafanyia kazi.

Njia nyengine ni njia ya tafiti mbali mbali ambazo hufanywa kuchukua maoni ya wananchi na maoni hayo yanatumika katika kupanga mipango ya serikali na hatimaye bajeti.

Mhe. Naibu Spika, mageuzi ya Tawala za Mikoa yanayoendelea hivi sasa katika kutekeleza Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2014, nayo yana lengo la kurudisha madaraka kwa wananchi na kuongeza ushiriki wa wananchi katika kuanda mipango na bajeti zao, lakini vile vile katika kusimamia utekelezaji wa mipango na bajeti hizi.

Mhe. Naibu Spika, serikali inawashirikisha wananchi katika njia hizo mbali mbali nilizozitaja na kazi ya serikali ni kugharamia na kutekeleza mahitaji kadhaa yaliyoibuliwa na wananchi kwa mujibu wa vipaumbele vilivyoainishwa katika mipango hiyo kwa kadri hali ya mapato inavyoruhusu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa serikali kama alivyozungumza Mhe. Waziri, mambo yote ambayo wanapanga ni kwa ajili ya wananchi na fedha ambazo tunatumia ni za wananchi. Sasa mimi ningependa kuuliza swali lenye kifungu (a) na (b).

(a) Ni utaratibu gani uliotumika katika ushirikishaji wa wananchi katika ununuzi wa Meli ya Mapiduzi II.

(b) Katika mradi mkubwa wa Bwawani ambao tayari umekodishwa kwa Mwekezaji pamoja na serikali ilichokusudia kujenga bandari ya Mpigaduri. Ni utaratibu gani unaotumika katika ushirikishwaji wa wananchi kwa ujumla katika maeneo ambayo na wakaazi wanaokaa katika maeneo husika ili na wao waweze kutoa yale waliyokuwanayo au kwa Kiingereza wanasema, *stake holders' meeting or public enquiry*. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, swali mama lilikuwa ni ushirikishwaji wa wananchi katika kuandaa bajeti na hilo nimelijibu na naamini kabisa Mheshimiwa, atakuwa ameridhika na jibu hilo. Ama kwa nini, kwa utaratibu gani wananchi wameshirikishwa katika ununuzi wa meli. Nataka nimjuilishe Mheshimiwa, ni kwamba yako mambo ambayo wananchi wanashirikishwa moja kwa moja, lakini yako mambo serikali kuu kutokana na

mazingira yaliyopo inabidi lazima ichukue hatua madhubuti ya kuhami hali hiyo. Hili la mfano wa meli, Mhe. Mwakilishi, anafahamu fika matatizo ambayo yametufika katika nchi yetu, ambapo wananchi wengi walipoteza maisha yao kutokana na ajali mbili zilizotokea katika nchi yetu na *concern* ilikuwa kwa wananchi kuwa na meli yao. Lakini hata ndani ya Baraza la Wawakilishi hapa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lililopita walizungumza kwa hisia kubwa na kuiomba serikali kuwa na meli hiyo.

Kwa hivyo, utaratibu umefuatwa kwa sababu Waheshimiwa Wawakilishi, kama nilivyosema wanawakilisha mawazo na maoni ya wananchi wao. Sasa hiyo ni pamoja na hayo mengine yote, lakini moja kwa moja niseme kwa ujumla wake ni kwamba, yako mambo moja kwa moja wananchi wanashirikishwa ambayo yanatoka chini kuja juu, lakini katika serikali zote yako mambo ambayo yanatoka juu na yanakwenda chini. Huo ni utaratibu wa kawaida wa mashirikiano na ushirikishwaji wa wananchi katika kuendesha serikali.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, nami nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Fedha. Kwa kuwa Wizara ya Fedha ndio wizara inayotengeneza bajeti ya matumizi ya kazi za maendeleo na kazi za kawaida. Je, serikali kupitia wizara hii itakubaliana na wazo langu la kwamba kupanga bajeti ambayo itaweza kufanya marekebisho ya wastaafu katika pencheni zao ambazo kwa sasa ni ndogo sana.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba alirudia tena, sikulisikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Rudia Mheshimiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Fedha ndiyo yenye kupanga bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Je, serikali kupitia Wizara ya Fedha itakubaliana nami lengo la kupanga bajeti ambayo itaweza kuwafanyia marekebisho ya pencheni wanazolipwa wastaafu wa zamani ambayo kwa sasa haikidhi haja, yaani ni ndogo sana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, swali la msingi sio hilo, kama unataka kuulizia swali la pencheni nafikiri ufuate *procedures* za maswali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona nami niweze kupata kidogo kwa Mhe. Waziri wa Fedha. Mhe. Naibu Spika,

kwa kuwa kuna malalamiko kama niseme kutofahamiana sana kwa watu au wananchi wetu kwa kuwa Rais wetu wa Zanzibar Dkt Ali Mohd Shein kwa nia njema aliamua kupandisha mishahara asilimia mia moja kwa wafanyakazi wa kima cha chini.

(a) Je, asilimia hii ya kima cha chini itapanda kwa mishahara yote au inapanda kwa kima cha chini.
(b) Ni lini ahadi hii itatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, mmekuwa mkiuliza maswali ambayo hayatokani na swali la msingi. Kama hakuna maswali Waheshimiwa, tuendelee.

Nam. 122

Kutengeneza Vifaa kwa Ajili ya Walemavu

Mhe. Zaina Abdalla Salum – Aliuliza:-
Ugonjwa wa kisukari umekuwa ukiongeza kiwango kikubwa cha idadi ya watu wenye ulemavu Zanzibar. Hivyo, hufanya idadi ya watu wenye ulemavu kuongezeka kwa asilimia kubwa kwa kupoteza viungo mbali mbali na wanapohitaji visaidizi kama vile miguu, mikono na masikio hupata usumbufu na kugharamika kutumia fedha nyingi.

Je, wizara ina mpango gani katika kutafuta wataalamu wa kuweza kutengeneza vifaa hivyo hapa Zanzibar ili kuingizia pato maalum serikalini na kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Kwanza naomba kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wenye afya njema na wazima katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 122 kama hivi ifuatavyo: -

Mhe.Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba, kuengezeka kwa ugonjwa wa kisukari unachangia kuengezeka kwa idadi ya watu wenye ulemavu. Hii ni kutokana na kupoteza viungo mbali mbali kama vile vidole, miguu, mikono na viungo vyengine. Kufuatia hali hii, Wizara ya

Afya kupitia Hospitali ya Mnazi Mmoja imeanzisha utaratibu wa kutengeneza viungo bandia ambavyo huwasaidia wale wote wenye mahitaji maalum ya kuweka viungo hivyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa wataalamu wa kutengeneza viungo bandia, Hospitali yetu inao wataalamu ambao wanasaidia kwa asilimia kubwa kutengeneza viungo hivi. Changamoto kuu inayoikabili kitengo cha kutengeneza viungo bandia ni ukosefu wa baadhi ya vitendea kazi na kemikali za kuchanganyia za kutengenezea viungo bandia hivyo. Kwa sasa mgonjwa anaehitaji kutengenezewa kiungo bandia analazimika kuchangia katika gharama za manunuzi ya baadhi ya vifaa hivyo na kemikali za kuchangia ili aweze kutengenezewa kiungo hicho bandia.

Hii ni kutokana na kuwa mahitaji ni makubwa zaidi kuliko bajeti ambayo tunaweza kuipangia kitengo hichi. Lengo la serikali sio kuingiza pato katika eneo hili bali ni kutoa huduma kwa wananchi wetu wote, mazungumzo yanaendelea hivi sasa na wataalamu na vifaa vya ziada vya kutengenezea viungo bandia kwa wenzetu mbali mbali nchini na nje ya nchi ili kuweza kupata misaada zaidi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Naibu Spika, napenda kukuuliza kwamba, ni lini hasa Wizara yako ya Afya itaboresha huduma zake ili iweze kutoa huduma bora kwa jamii.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali kadri tunavyopata fedha na kadri serikali inavyoweza kuingiza fedha ndipo huduma za afya zitaweza kuwa bora zaidi. Mwenyezi Mungu akitujaalia tukeshapitisha mswada huu wa Mafuta na Gesi na Mwenyezi Mungu akitujaalia Mafuta na Gesi yakitoka, katika michango mingi sana ya Waheshimiwa Wawakilishi wamekuwa wakizungumza kwamba kipato kitakachopatikana kitasaidia elimu na afya ambazo ni huduma kuu za jamii. Kwa hiyo, kila tutakapopata fedha na sisi tutaendelea kufanya huduma zetu ziwe bora zaidi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis:

(a) Mhe. Naibu Spika, ni sababu gani za msingi zinazopelekea kitengo hicho kukosa kuingiziwa fedha za kuendelea na shughuli zake za kila siku.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kitengo hichi kinapatiwa fedha ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi wake.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, sikusema kwamba kitengo hichi kinakosa kutilia fedha. Nimesema kwamba katika mpangilio mzima wa Wizara ya Afya, sisi tunapata bajeti bilioni kama hamsini na tisa, katika mpangilio mzima wa ugavi wa zile fedha katika kila kitengo kitengo hichi huwa kinapata kasma yake ambayo inapangiwa kutokana na bajeti na fedha mbayo ipo na tunaipata.

Sasa fedha zile hazitoshi kutengenezea viungo vyote vya wale wanaohitaji kwa sababu hizi ni huduma kama za ziada, kwanza suala la madawa, matibabu muhimu na kadhalika. Sasa kitengo hichi kinapangiwa fedha ambazo hazitoshelezi. Kwa hivyo, tutakapopata fedha zaidi na sisi tutaweza kupangilia zaidi hichi kitengo kiweze kupata fedha hizo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Waziri, amekiri kwamba hichi kitengo kipo na kimeanza kufanya kazi. Sasa mimi nilikuwa nataka nijue je, ni watu wangapi ambao wameshafaidika na mpango huu toka kuanzishwa kwa kitengo hichi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa hivi katika daftari la wale waliofaidika ni takribani wananchi mia nne thakanini ambbao waliofaidika katika kipindi hichi cha miaka mitano ya ripoti na kitengo hichi hadi sasa hivi kina wataalamu wawili, lakini pia kina wasaidizi wao watatu. Kwa hiyo, watu watani jumla yao ambao wanafanyakazi katika kitengo hichi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 138

Matibabu ya Saratani hapa Zanzibar

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Aliuliza:-

Katika Mkutano wa Tano wa Kikao cha Kwanza cha Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika tarehe 8/11/2011 Dodoma. Mhe. Naibu Waziri wa Afya wa Tanzania wakati wa kipindi cha maswali na majibu alisema kwamba alifanya mazungumzo na aliyekuwa Waziri wa Afya wakati huo wa SMZ Mhe. Juma Duni Haji na alimueleza kwamba SMZ ina mpango wa kuanzisha huduma za kutoa matibabu ya Saratani hapa Zanzibar badala ya Wagonjwa wa Saratani Zanzibar kufuata huduma hiyo Tanzania Bara.

a) Je, Mhe. Waziri, unakubaliana na maelezo hayo yaliyotolewa Bungeni.

b) Mpango huo wa kutoa huduma ya matibabu ya Saratani hapa Zanzibar unategemewa kuanza lini.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 138 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba, Wizara ina mpango wa kuanzisha huduma za matibabu ya saratani moja kwa moja hapa Zanzibar ili kuweza kuwapunguzia wagonjwa wetu mzigo wa kufuata matibabu hayo Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, kwa hatua za awali, wizara imeanza kutekeleza mpango huo kwa kuanzisha kliniki maalum mnamo mwezi wa Januari mara tu pale aliporudi mtaalamu wetu wa kwanza kabisa aliesomea na kubobea katika "*Oncology*" Dkt Salama Uledi Mwita ambaye ndiye mtaalamu wetu wa mwanzo aliyerudi na *clinic* imeanzishwa moja kwa moja mnamo mwezi wa Januari mwaka 2016.

Aidha, upanuzi wa huduma hizo unaendelea na unahitaji nyezo mbali mbali zikiwemo majengo maalum ya '*Oncology'*, vifaa vya kisasa vya uchunguzi na tiba ya saratani. Bado tunaendelea kutumia huduma za wenzetu Tanzania Bara Ocean Road, Muhimbili na kwengineko. Ingawa sasa hivi *clinic* ya awali huwa inatolewa hapa Zanzibar.

Kwa upande wao kule tunatumia pia tiba ya mionzi na tiba nyenginezo kwa vifaa ambavyo sisi hatuna. Wizara hivi sasa imeelekeza mpango huo kuingizwa moja kwa moja hospitali inayotarajiwa kujengwa Binguni, ambapo katika ramani na michoro yake kuna eneo maalum ambalo limetengwa kwa ajili ya *speciality* hii ya *Oncology*, yaani maradhi haya ya kensa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ugonjwa huu wa saratani za shingo ya kizazi umekuwa mwingi sana kwa kina mama. Je, serikali ina mpango gani wa kushajihisha kina mama vijijini ili waje wapime na kuonekana mapema tatizo lile ili serikali isipate hasara kubwa ya kuwapeleka Ocean Road na kwengineko.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa kwa kuniuliza swali hili. Ni kweli kabisa idadi ya wagonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi

inazidi kuwa kubwa sana. Katika *clinic* ya kina mama wanaohudhuria pale Mnazi mmoja tu kila akina mama 100 wanaofanyiwa basi 18 kati yao huonekana na viashiria vya awali vya saratani ya shingo ya kizazi.

Tiba kubwa kabisa ya saratani ya shingo ya kizazi ni kuigundua mapema ndipo yanapoweza kutibiwa, yakichelewa inakuwa umechelewa sana na tiba yake inakuwa ngumu sana na inaweza ikasababisha pia kupoteza maisha. Hilo linakwenda pia kwa tenzi dume kwa wanaume, tiba yake kubwa ni kugundulika mapema. Nchi za wenzetu zilizoendelea wakina mama wao wanakwenda kufanyiwa uchunguzi ya saratani hii ya matiti pamoja na shingo ya kizazi anapotimia mwanamke umri wa miaka 30.

Kwa hiyo, kama kuna mwanamke ambaye hajenga kuanzia umri wa miaka 30 mpaka sasa hivi pengine miaka 40, basi huyo ameshachelewa kwa miaka 10 anatakiwa ashajihike haraka sana aende kwaajili ya kufanyiwa *test* hiyo. *Test* hiyo inafanyiwa pale pale Mnazi Mmoja shingo ya kizazi pamoja na saratani nyenginezo na baada ya hapo unapewa ushauri nini kinachotakiwa kifate.

Kwa hiyo, mimi namshukuru sana Mhe. Mohammed Said, kwa kuleta swali hili, ni kweli bado tunatakiwa tuongeze vifaa zaidi na hivi sasa tuna wataalamu wetu wawili wako pale Ocean Road ambao wanasomea masuala haya. Watakaporudi wao tunatarajia kitengo hichi kitakuwa kikubwa na Mwenyezi Mungu akitujaalia madhali Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imetamka suala la Binguni, kwa hiyo, hospitali hiyo ikishaanza mara moja miongoni mwa kitengo cha mwazo kabisa kitakuwa ni "*Oncology*".

Hapo hapo naomba kuongezea pia katika upande wa Wizara ya Afya, wagonjwa wengi tunaowasafirisha kwenda nje ya nchi basi ni wa maradhi haya ya saratani hivi sasa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Afya, amekiri kwamba kwa mdomo wake kwamba ndio kwanza wana mtalamu mmoja aliesomea masuala haya ya saratani na vifaa hakuna.

(a) Je, ana mpango gani na mkakati gani katika kutafuta na kuleta wataalamu wengine wa saratani kwa sababu maradhi haya ni maradhi sugu na yanawasumbua kina mama wengi na vifaa lini vitakuja.

(b) Jana Mhe. Waziri, alikiri kwamba kunako taasisi yake anayoiongoza ni wazembe. Sasa je, atatuhakikishia vipi kunako masuala haya ya saratani mtaalamu keshakuja na vifaa hakuna, uzembe huu atatuhakikishia vipi

hautorejea tena katika Hospitali ya Mnazi Mmoja hasa katika maradhi haya sugu ya kina mama ya saratani, kwa sababu ukifanya uzembe, yaani usipogundua mwanzo kama mama huyu ana viashiria vya saratani mama yule umemua. Sasa na hospitali yake jana kakiri kama wao ni wazembe atatuhakikishia vipi.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nadhani tungekwenda kwenye *Hansard* hili neno 'wazembe' au 'uzembe' lingepata tafsri nzuri zaidi.

Uzembe unaweza kutokea sehemu yoyote hata kama barabarani unatokea uzembe na ajali ikatokezea na hiyo ajali inaweza kuwa imesababishwa na uzembe au binaadamu. Ajali kama hizi huwa zinatokea sehemu nyingi, lakini kwenda kwenye swali moja kwa moja. Hichi kitengo ambacho kinafanyakazi pale nimesema hapo awali kwamba sasa hivi kuna daktari mmoja Dkt Salama Uledi Mwita na wawili wengine wanasomeshwa.

Hiyo Ocean Road yenyewe ambayo wameanzisha miaka mingi iliyopita wanawataalamu bingwa 9 pale, wote wako 9, mimi nimefanya ziara nimekwenda kutembelea, nimefanya mazungumzo nao, pale kuna wataalamu bingwa 9. Kwa hiyo, ukichukulia kwa miaka hiyo ambayo wameanzisha wao na sisi hapa tulipo na wawili wako masomoni ambao wanamaliza hivi karibuni, kwa kweli kwa upande wa wafanyakazi au mabingwa wa maradhi haya tunakwenda vizuri.

Changamoto zilizokuwepo bado ni fedha, pale tutakapopata fedha, pale tutakapopata fedha hizi *clinics* tutaziimarisha zaidi. Kwa sababu hivi sasa *clinic* hiyo inakwenda kama siku mbili au tatu kwa wiki hatujaweza bado kufanya wiki nzima kwa sababu changamoto hizo hizo za kifedha. Lakini pale fedha tutakapopata zaidi basi nayo *clinic* hii itaweza nayo kutoa huduma zaidi. Nia sio kuwasulubu wafanyakazi wetu ama kusema wazembe, wale wafanyakazi wanajitolea na wafanyakazi kwa moyo wao wote katika kuwatumikia wananchi. Hata tuwalipe nini hakitotesheleza kwa kazi ambayo wanafanya.

Kwa hiyo, mimi naendelea kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara ya Afya, ajali kutokea kazini ni jambo la kawaida, makosa kutokea mote hata humu ndani tunafanya makosa mbali mbali, ni jambo la kawaida.Wafanyakazi wa Wizara ya Afya hususan wale wanaotoa matibabu wanaendelea kufanya kazi vizuri sana, naomba tushirikiane na sisi kuwapongeza ili waweze kuwa na moyo wa kuendelea kutoa ili bora zaidi kwa wananchi wetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, kuhusu kanuni ya 37(1), naomba kusoma:

"Waziri au Mjumbe yeyote ataeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Mhe. Waziri mmoja anaweza kujibu Mhe. Waziri mwengine".

Mhe. Naibu Spika, narudia kwamba jana wakati ilipokuja hoja ya maharibiko ya yule mtoto katika hospitali ile mpaka kumepelekea kutoa harufu, Mhe. Waziri, alikiri kwamba kumefanyika uzembe kwenye Baraza hili. Lakini leo katika swali ambalo alilouliza Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri, kaikana. Sasa sijui tukamate ipi. Katika *Hansard* jana Mhe. Waziri, alisema ni kweli ulifanyika uzembe, lakini leo kauliza Mheshimiwa, Mhe. Waziri, ameikana, sasa tukamate wapi Mhe. Naibu Spika, naomba muongozo wako.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Abballa Maulid Diwani, mimi nafikiri nimemfahamu Mhe. Waziri wa Afya, alivyosema na nafikiri wengi wamemfahamu uzembe unaweza ukatokea pahala popote na yeye hakukataa kwamba hakusema uzembe. Alichosema kwamba, uzembe pahala popote unaweza ukatokea hata barabarani.

Kwa hiyo, alikiri katika hilo suala la hiyo kesi ambayo unaizungumza kweli palitokea uzembe *on that issue*, sijui umenifahamu vizuri. Ndicho ambacho amekizungumzia Mhe. Waziri. Sasa sijui ulikuwa unataka akiri kwamba, kweli nilisema watu wa Wizara ya Afya wazembe au vipi, sifahamu, unataka kumueweka katika sehemu hiyo. Lakini kwa nilivyofahamu mimi, yeye ameelezea wapi uzembe unaweza ukatokea. Kama umetaka muongozo wangu na busara zangu mimi nafikiria sana kwamba Mhe. Waziri, amelijibu vizuri sana swali lako.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, basi alikuwa akiri kwamba huo uzembe uliotokea atatafuta njia gani kuweza kujua kwamba uzembe hautotokea tena. Ndiyo swali nililouliza.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya, nikupe nafasi na wewe ujibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani labda nitoe ufafanuzi ambayo nilioelezea jana.

Jana nilieleza mambo matatu ambayo ni matukio yaliyotokea baada ya kuchunguzwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Jambo la kwanza, baba wa mzazi aliyemleta yule mama alikuwa hakuacha namba. Jambo la pili, kuna buku pale aliambiwa ajaze namba, hakujaza namba yake, ninafikiri kwa sababu labda alikuwa hana simu au kuna tatizo jengine.

Jambo la tatu, aliondoka moja kwa moja baada ya kumuacha yule mama mzazi, yeye aliyeondoka moja kwa moja bila ya kubaki pale au kuulizia kinachofuata. Yule mama akapelekwa kwenye *operation theatre*, baada ya kutoka hapo akapelekwa *ICU* moja kwa moja na akachukua muda kupata fahamu. Waliporudi wafanyakazi wetu wakawa wanamtafuta baba mtu, hata chakula hakuletewa yule mama kwa muda wa siku tatu, hakuletewa chakula pale. Chakula kapatiwa na hospitali kwa muda wa siku tatu.

Sasa wafanyakazi hao huwezi kuwalaumu. Tatizo lililotokezea ilikuwa ile maiti waitoe pale kuipeleka *mortuary*. Kila *shift* walijua kwamba yule baba atakuja katika *shift* ijayo. Ndiyo tatizo lililokuwepo pale. Ile maiti ilitakiwa ipelekwe *mortuary* moja kwa moja. Ndiyo maana kwa kitendo hicho tumetoa dokezo na tumewachukulia hatua wafanyakazi 28 wa Hospitali ya Mnazi Mmoja *shift* tatu, pamoja na *supervisor* wao. Tisa mara tatu ni ishirini saba pamoja na *superviser* wao. Tumechukua hatua za kuwapa onyo kali la kimaandishi na majina yapo na hapa nilipo ninayo. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Naibu Spika, haya ni mambo ambayo yanatokea kila pahala. Uzembe unatokea kila pahala na hatua lazima zichukuliwe panapotokezea uzembe na sisi tumefanya wajibu wetu wa kuchukua hatua. Na kila litakapotokea jambo tutaendelea kuchukua hatua.(*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, tuna Mswada tunataka kuupitisha. Hapa hatushindani, hatujaja kushindana. Mhe. Hassan, nakuomba ukae, taratibu tutafanya baadae. Sasa hivi tunakwenda kwenye maswali, tukimaliza maswali, tunakwenda kwenye hoja. Hakuna haja. Umejibiwa suala lako vizuri sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Katika nilivyojibiwa ndiyo maana ninaomba muongozo tafadhali kwa heshima na taadhima.

Mhe. Naibu Spika: Muongozo nimesema siutaki. (*Makofi*)

Mhe. Amina, swali la pili la nyongeza.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba maradhi haya ya saratani yanaongezeka siku hadi siku. Na kwa kuwa Wizara yake inafahamu kwamba akinamama tunaathirika sana na ugonjwa huu. Je, Mhe. Waziri, umejiandaa vipi kuwaelimisha wananchi kupima afya zao ili kama mtu akigundulika na viashiria ili aweze haraka iwezekanavyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Ninamshukuru sana Mhe. Amina Iddi Mabrouk, kwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo ambalo naomba nilijibu.

Ni kweli maradhi haya ya saratani, hasa ya shingo ya kizazi *Cervical Cancer* yamekuwa yanaendelea kukua kwa kasi sana. Hili ninalolifanya hapa na ndiyo maana nikarudia lile jibu wakati ule ni miongoni mwa kuendelea kutoa elimu. Na leo ninaamini Wawakilishi wote wa wananchi wamepata elimu hiyo ya kwamba mwanamke anapotimia umri wa miaka 30 anatakiwa kila mwaka aende kufanyiwa *Cervical Test Nia*, *test* hii ya saratani ya shingo ya kizazi.

Tiba kubwa ni kugundulika mapema. Kwa hivyo, sisi kwa upande wetu kuna vile vipeperushi ambavyo tunavyotoa, kunakuwa na zile kliniki za kwenda vijijini kupitia vituo vyetu vya afya. Vituo vyetu vya afya vyote ni mia moja na arobaini na mbili. Na huwa kuna zile *outreach programmes*, kila baada ya muda huwa zile kliniki zinatembea kwa Unguja na Pemba kwenda kutoa hizo huduma.

Lakini kwa kuwa bado wafanyakazi ni wachache ndiyo maana unakuta hakuna kliniki hizo kwa kila mwezi au kila mara. Kliniki kubwa inayotolewa ni Hospitali ya Mnazi Mmoja na Rahaleo mpaka hivi sasa. Hizo ndizo kliniki kubwa. Kwa hivyo, sisi kadri ya uwezo utakavyopatikana tutaendelea kushajihishana na Mwenyezi Mungu akitujaalia hapa pia tutaleta hivyo vipeperushi ambavyo vinaelezea ili kila Mwakilishi apatiwe nakala kwa ajili ya kuwapelekea wananchi wake kwa ajili ya kusambaza elimu hiyo.

Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Nam. 38

Vijana Wanaojitolea *ZBC*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza :-

Kwa kuwa katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) kuna vijana kwa muda mrefu sana wanajitolea tena usiku na mchana, bila ya kupatiwa ajira za kudumu.

(a) Je, ni vijana wangapi wanaojitolea *ZBC – TV* na *ZBC – RADIO*

(b) Je, lini vijana hao Serikali itawaajiri.

(c) Je, kama Serikali haiwezi kuwaajiri vijana hao, haioni haja ya kuwaongezea posho angalau 150,000/= kwa mwezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 38 lenye kipengele (a), (b) na (c), naomba kutoa Maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, kwenye sekta ya Habari inakuwa na wafanyakazi wa aina mbili zifuatazo:-

i. Kuna kuwa na wafanyakazi wa kudumu ambao wanalipwa mishahara yao kila mwisho wa mwezi.
ii. Pia, kunakuwa na wafanyakazi wanaojitegemea ambapo awafanyakazi hawa wanalipwa kutokana na kazi zao kwa mujibu wa "*story*" zinazorushwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 38 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Wafanyakazi ambao wanajitegemea jumla 70 kwa mchanganyiko wa *TV* na Redio.

b) Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) huwapa nafasi za kuwaajiri wafanyakazi wa kujitolea kwa nafasi za wataalamu pale ambapo hutokea nafasi tupu za ajira kwa mfano mwaka 2015 tumeajiri wafanyakazi 12 na mwaka huu

2016 kuna nafasi tupu tatu (3) ambazo zinasubiri majibu kutoka Afisi ya Rais, Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ituingizie Mishahara yao, hata hivyo, tuna nafasi tupu tisa (9) ambazo tunazitegemea kuwaajiri kwa upande wa Pemba ambao wanasubiri kufanyiwa Usaili.

c) Kwa vile vyombo vingi vya habari mara nyingi hutegemea wafanyakazi wa kujitegemea kwa kuwa wafanyakazi hawa pia wana uwezo wa kufanya vizuri. Hivyo, Shirika hutegemea kuwalipa kiwango cha mshahara kutokana na uwezo wake wa kujiendesha.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa *Spice Fm Radio* ya *ZBC* haina wafanyakazi wa kujitegemea kama alivyosema, kuna wafanyakazi wa kujitolea na wa muda mrefu na mpaka sasa hawajaajiriwa. Je, ni lini Serikali itafanya hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda nimjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi, nakiri kwamba hicho kituo kuwa hakina hao wafanyakazi wa kujitolea. Lakini niseme kwamba Serikali kwa kuwa hawa vijana wa kujitolea tunao katika sehemu yetu ya *ZBC* na *TV* na pale kwa kuwa wameshaiva, pale nafasi zitakapotoka za ajira basi tutawaajiri wale vijana wetu, tutachukua vijana wale na kuwapeleka katika kituo kile waweze kufanya kazi.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa masuala ya ajira ni changamoto kwa nchi nyingi zetu za Afrika pamoja na sisi Tanzania pamoja na Zanzibar, tumekuwa tunahangaika miaka nenda mbele ili kuhakikisha kwamba ajira zinaongezeka ndani ya Serikali lakini pia na kwenye sekta binafsi.

Labda mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali dogo tu la nyongeza. Ni kitu gani au ni kikwazo gani ambacho kinachofanya *ZBC* hadi leo kutounganishwa ndani ya *DSTV*.
Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Simai Mohamed Said, kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, sababu ambazo zinafanya *ZBC* kutojiunga na kituo kile cha habari. Mhe. Naibu Spika, arudie swali lake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, naona munapiga makofi mengi sijui kwa nini. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu swali la nyongeza la Mhe. Simai Mohamed Said, baada ya majibu mazuri sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari.

Mhe. Naibu Spika, kujiunga *DSTV* ni uamuzi wa kituo husika na hatulazimiki kama Serikali kujiunga na *DSTV*. Kwa hivyo, pale *ZBC* ama Shirika la Utangazani na Televisheni litakapoona kuna umuhimu kujiunga na *DSTV* itafanya hivyo. Kwa sasa haioni sababu ya ulazima kwa nini wajiunge na *DSTV*. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba, leo hii Waziri wa Kazi aliniambia kwamba Serikali imepiga marufuku kuajiri watu hawa ambao siyo rasmi. Wakati huo huo Naibu Waziri, hapa kathibitisha kwamba wanafanya kazi hao na bado anaendelea kuajiri.Anafuata sheria kutoka wapi isipokuwa sheria na Katiba ya nchi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mhe. Suleiman Sarahan Said, baada ya majibu mazuri ya msingi ambayo Mhe. Naibu Waziri, alieleza.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa ajira utaendelea kufuata sheria na utaratibu uliowekwa na kamwe Serikali haitokiuka misingi ya ajira. Lakini kama Serikali tunaona umuhimu wa kusababisha kupata ajira kwa vijana wetu. Kwa sababu lipo wimbi kubwa la vijana ambao hawana ajira. Kwa hivyo, Serikali itachukua kila aina ya hatua kuwawezesha wananchi ili waweze kujiajiri na pale Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuajiri, basi taratibu na sheria zitafuatwa ili wananchi waajiriwe Serikalini kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Nam. 92

Kuimarishwa Kwa Kilimo Cha Matunda Nchini

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:-

Wananchi wa Zanzibar wameonekana kujiimarisha sana katika kilimo, hasa katika kilimo cha matunda kama vile matikiti, mapapai, machungwa, maparachichi, tungule na kadhalika. Hata hivyo, kuna aina fulani ya matunda kama vile maembe na minazi inaendelea kupotea.

(a) Je,Wizara haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa wakuotesha miti ya kupandisha (*budding, grafting, air layering*, n.k*)* ili kuweza kutunza aina nyengine za miti yetu isiendelee kupotea.

(b) Je, Wizara haioni kuwa ipo haja ya kuotesha miche yetu ya asili ya minazi ili kuwa minazi mingi Zanzibar ikizingatiwa kuwa miche ile inadumu kwa muda mrefu zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 92 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara inakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, wakulima wetu hivi sasa wamejikita zaidi katika kilimo cha matunda ili kuongeza kipato na upatikanaji wa chakula nchini. Mwamko huu wa kilimo cha matunda na mboga umetokana na elimu inayotolewa na wataalamu wa Wizara pamoja na taasisi za Serikali vile vile na taasisi binafsi.

Mhe. Naibu Spika, uzalishaji wa miche ya kupandishia una gharama kubwa na pia unahitaji utaalamu maalumu, Wizara imekuwa ikiotesha miche hii katika vitalu vyake viliopo Unguja na Pemba ambapo kila mwaka huotesha wastani wa asilimia 15 ya miche ya kupandishiwa ambayo inauzwa kwa wakulima.

Mhe. Naibu Spika, Wizara inakubali kwamba ipo haja ya kuotesha miche yetu ya asili ya minazi ili kuwa na minazi mingi Zanzibar ikizingatiwa kuwa miche ile inadumu kwa muda mrefu. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeanza kuandaa programu maalum ya kuendeleza zao la nazi. Utekelezaji wa programu hiyo utawezesha kutoa taaluma kwa wakulima pamoja na kuzalisha

miche mingi ya minazi ya asili hapa Zanzibar. Aidha, kwa hivi sasa Wizara inalenga kuotesha miche 1000 ya minazi kila mwaka.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Sheha Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize swali langu la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri, naomba nikuulize kwa kuwa wimbi la ukataji na utumiaji wa mbao za minazi umeongezeka mkubwa sana. Je, Wizara yako inalitambua hili na kama inalitambua, ni hatua gani ambazo Wizara ambazo inapanga kuchukua kwa kuzuia ukataji huu wa minazi asili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumjibu swali lake Mhe. Mattar, kama ifuatavyo.

a) Wizara inalitambua hili kwamba minazi inakatwa ovyo.

b) Hawa wanaokata minazi, tuna doria tunaifanya tunapowakamata tunawatoza faini na yale magogo au kama wametumia misumeno basi pia tunaikamata.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, kama ulivyotwambia kwamba miche ya *design* hii ya kupandishia (*budding*), ni miche ambayo inahitaji gharama katika kuotesha kwake. Lakini pia ukizingatia miche hii hii ni miche ambayo haina ukuaji mpaka wa kudumu kama miche mengine hii ya kawaida ambayo tunaotesha. Je, Wizara yako ikishirikiana na Serikali inalionaje suala la kuotesha miche ile ile ambayo tumeiozea, yaani ya zamani ile ambayo iliyokuwa inatumika kwa muda mrefu na inadumu na matunda yake yanakuwa yana uimara zaidi kuliko hii ya *budding*.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Hidaya, swali lake kama ifuatavyo.

Hilo suala Wizara imeliona na ndiyo imeamua hivi sasa kupanda miche yetu ya asili na lengo letu la Wizara kupanda miche hiyo laki tano kwa mwaka. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Mhe. Naibu Waziri, ametuambia kila mwaka tunapanda minazi laki moja. Sasa ningependa kumuuliza Unguja na Pemba minazi hii imepandwa shamba ipi ama vijiji vipi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana. Mhe. Naibu Spika, katika jibu langu mama sikusema tuna panda, nilisema inalenga kuotesha miche laki moja. Kwa hivyo, hili ni lengo, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 112

Ujenzi wa Barabara ya Msuka – Konde

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata ruhusa ya kuuliza swali. Mhe. Naibu Spika, swali langu namba 112, kabla ya kujibiwa naomba nilifanyie marekebisho, limekuja kidogo na makosa ya hesabu. Wameandika shilingi milioni 3,000,000/-. Sio shilingi milioni 3,000,000/- ni shilingi milioni 300,000,000/-, na kipindi kile wametaja kipindi kifupi, mimi nilisema sio kipindi kifupi. Kwa hivyo, naomba lisomeke hivyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya marekebisho hayo naomba swali langu nambari 112 lijibiwe. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mwaka 2012 Shirika la Tanzania/Japan *Food Aid Counter Part Fund* kupitia Jumuiya ya Maendeleo ya Jimbo la Konde (*KCDO*) lilitoa msaada wa jumla ya shilingi milioni tatu (3,000,000/-) kwa lengo la ujenzi wa barabara ya kiwango cha kifusi yenye urefu wa kilomita 4.3 ya Msuka - Konde ambayo ilikamilika mwaka 2013. Hata hivyo, katika kipindi kifupi cha matumizi ya barabara hiyo hivi sasa kumekua na tatizo la kuchimbuka sana kwa barabara hiyo na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wa maeneo hayo na wanaotumia njia hiyo.

Na kwakuwa Mhe. Rais, alitoa ahadi ya kuitengeneza barabara hiyo alipokuwa katika mkutano wa kampeni katika viwanja vya Polisi Konde kwa mwaka 2015 kwa kiwango cha lami.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia barabara hiyo isiendelee kuharibika ikiwa ni pamoja na kuziba mashimo makubwa ambayo yamekuwa ni kero kubwa kwa wananchi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga barabara hiyo ikiwa ni pamoja na kutimiza ahadi za Mhe. Rais, alizozitoa katika mikutano huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake namba 112 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja, pamoja na marekebisho aliyoyafanya kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yetu itahakikisha kwamba barabara zote zilizojengwa katika hatua hiyo zinafanyiwa ukarabati ili ziweze kupitika, na mipango ya kuziwekea lami barabara hizo utafanyika pale wizara itakapopata fedha za kufanya hivyo.

Aidha, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba zile ahadi zote ambazo Mhe. Rais wetu kipenzi, Dk. Ali Mohammed Shein, alizitoa wakati wa kampeni, basi sisi ni agizo kwetu, na tutazifanyia kazi kwa kadri hali ya uwezo utakavyoturuhusu.

Vile vile, napenda kumpongeza sana Mhe. Omar Seif, kwa jitihada alizochukua mpaka akampata huyo mfadhili. Mimi mwenyewe nilikiri nilipotembelea barabara hii hivi majuzi, kusema kweli tunazipongeza jitihada hizo, na tuko tayari kushirikiana nao tena hawa wafadhili katika kuhakikisha kwamba barabara hiyo ahadi ya Mhe. Rais, tunaitekeleza. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kilio hiki cha barabara hii ni cha muda mrefu, ambapo kama ikiachiwa kutokuifanyia matengenezo ya dharura basi itarudia katika hali yake ya asili kama mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kujua ni lini huu utaratibu wa kuanza angalau kuziba mashimo makubwa yaliyoanza kujitokeza utaanza ili kuidhibiti isije ikabomoka na wakati wa ujenzi ikatuongezea gharama kubwa serikali. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, sisi tuna utaratibu katika Idara yetu ya *UUB* kwamba, zile sehemu zote korofi tunazifanyia matengenezo ya haraka. Kuna barabara yake hiyo anayosema, kuna barabara ya Finya ambazo yeye mwenyewe anazijua.

Mhe. Hamad Mattar, zile barabara kama anavyosema, hali ya kifedha kama itaturuhusu tutazifanyia ukarabati zile sehemu korofi. Lakini napenda kumuarifu Mhe. Omar Seif, kwamba sisi lengo letu ni kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika wakati wowote, ili kuhakikisha kwamba tunarahisisha usafiri kwa wananchi wetu na kuwaondoshea kero za usafiri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika,

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba nitowe taarifa kwa Waheshimiwa Wajumbe, wanapouliza swali la nyongeza, basi waelewe kwamba wanamuuliza ni waziri husika na Mhe. Naibu Waziri, yuko hapa kwa niaba ya Mhe. Waziri. Kwa hivyo, nilikuwa napendelea sana waseme kwamba, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kitu kadha kadha, sio waseme Mhe. Naibu Waziri na waziri yupo hapa hapa, Mhe. Naibu Waziri, anajibu kwa niaba yake.

Mhe. Naibu Spika, ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuuliza swali langu moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali ina malengo mazuri ya kuwaondolea kero wananchi wakiwemo wa Jimbo la Chukwani, kilio kikubwa katika Jimbo la Chukwani ni ubovu wa barabara na katika majibu yake alisema kuwa wanachukua sana ahadi za Rais kuwa ni agizo la kiserikali. Tokea Awamu ya Sita, ahadi ile ya Serikali ya Awamu ya Sita katika barabara ya Chukwani mpaka leo haijafanyiwa kazi. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, anijibu swali hilo.

(a) Je ni lini atalifanyia kazi suala hilo.

(b) Katika kuwaletea maendeleo wananchi mbali mbali kwenye maeneo yao, kuna utaratibu ambao Mhe. Waziri, tulifuatilia na tukafanya kwa pamoja, na kuna wadau tofauti katika Jimbo langu la Chukwani wamejitolea katika

kutengeneza au kushirikiana na wizara yake katika kutengeneza zile njia ambazo zinatakiwa kwa kiwango cha fusi.

Je, ni sababu gani zilizokwamisha wakati taratibu zile zote tumeshazifuatilia na tumeshazifanya. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu katika kipindi kilichopita katika Baraza lako hili tukufu la Wawakilishi kwamba, ile ahadi ya Mhe. Rais wa Awamu ya Sita Dk. Aman Abeid Karume ya kuimaliza kwa lami ile barabara mpaka Buyu pwani, sisi kidogo tulisita kwa sababu lile eneo pia linapita uwanja wetu wa ndege katika hiyo *phase* ya mwisho ambayo tunataka kuijenga.

Mhe. Mwenyekiti, yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe, anajua na tulikuwa pamoja na sheha wake, na tukaoneshwa mpaka zile sehemu. Lakini licha ya hivyo, namuarifu kwamba sisi tutakaa tena na wataalamu wetu na yeye pamoja na wajumbe wake wa kamati yake ya maendeleo ya Jimbo la Chukwani, ili kuangalia namna gani ya kuhakikisha kwamba kwa kiasi fulani tunaitekeleza ile ahadi.

Swali lake la pili, mimi nampongeza sana kwa sababu tulikuwa pamoja na wale watu wa Chuo cha *Science Marine*, na wakaahidi kwamba wao wako tayari kutoa fedha ili kuhakikisha kwamba ile barabara ambayo inapita katika Chuo chao Kikuu ambacho kitafunguliwa mwezi wa Oktoba, tuwasaidie katika kuiweka kwenye hali nzuri. Ile ahadi tumeichukua. Lakini kama nilivyosema mwanzo, tatizo tuna vifaa vichache na ni chakavu na hivi sasa tuna ahadi ya kuimalizia barabara ya Jendele mpaka Unguja Ukuu Kaebona. Pale ambapo tutakuwa tayari tuna vifaa vya kutosha, basi tutakwenda kuiangalia tena barabara yake, tuifanyie ukarabati ili wanafunzi wakienda kusoma pale Chuo Kikuu cha *Science Marine* wasipate tabu.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, siku ambayo alikuja akafungua soko la samaki na mboga mboga pale kwenye Jimbo langu la Tumbe, moja ya ahadi aliyoiweka ni barabara kutoka pale KOJIFA barabara kubwa ya kuendea Konde hadi Bandarini, alisema kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, swali lako lazima lielekee kwenye swali la msingi.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ndio naendelea Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Hilo silo. Hilo unalolizungumza silo kabisa, unazungumzia barabara nyengine kabisa sio ambayo imeulizwa humu kwenye swali la msingi. *(Makofi)*

Tunaendelea na swali jengine Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Nam. 27

Kuharibika kwa Barabara za Pemba

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:-

Kwanza naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein, kwa kujenga barabara zenye urefu wa 127.7 *k.m* kwa Unguja na 203.4 *k.m* kwa Pemba kwa viwango mbali mbali ikiwemo kiwango cha lami na fusi. Kwa upande wa Pemba miongoni mwa barabara hizo ni:

- Mzambarauni Takao - Finya
- Mzambarauni Kariim - mapofu Kiwango cha lami
- Wete - Konde
- Pandani - Pembeni - Kiwango cha fusi

Kwa kuwa barabara hizi nilizozitaja hapo juu zimeonekana kuanza kupasuka na kuwekwa viraka hata kabla kukabidhiwa kwa serikali, na baada ya kukabidhiwa kutoka kwa Kampuni za *H-Young* na *Mecco* jambo ambalo ni kuitia hasara kubwa sana Serikali na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara hizo.

(a) Je, serikali inafahamu suala hili la kuharibika kwa barabara hizi na kama inafahamu Je, wakati kazi inaendelea hapakuwa na wakandarasi wazalendo waliosimamia ujenzi huo kwa ajili ya kuishauri wizara.

(b) Je, serikali imechukuwa hatua gani kwa kampuni zilizohusika baada ya kubaini upasukaji huo wa barabara au iliridhika na kazi iliyofanywa baada ya kukabidhiwa.

(c) Ni hatua gani zilizochukuliwa na serikali kwa kampuni hizi baada ya kuitia hasara kubwa sana serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake namba 27 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu swali lake Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe.Naibu Spika, barabara ya Mzambarau Takao-Pandani-Finya, pamoja na ile barabara ya Mzambarau Karibu-Mapofu, ni barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami kwa msaada wa watu wa Marekani. Barabara hizi zimetekelezwa kulingana na masharti ya *MCC,* ambayo yameanishwa katika mkataba wake na serikali, na kwamba msaada huu masharti yake ilikuwa lazima serikali iunde kitengo maalum kinachojitegemea kusimamia mradi huo, kwenye Sekta ya Umeme, maji, barabara na Viwanja vya Ndege.

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Wete-Konde, ni miongoni mwa barabara zilizojengwa kutokana na mkopo wa ushirikiano wa fedha, kutoka Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu, yaani *BADEA* na *Saud Fund* na Serikali ya Zanzibar. Ujenzi ulianza mwaka 2009 na kukamilika mwaka 2015, baada ya changamoto nyingi zilizojitokeza wakati wa ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Pandani–Pembeni, imejengwa kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) chini ya Mradi wa *MIVAF*, ambao ulikuwa chini ya Wizara ya Kilimo na Uvuni kwa wakati huo, ambapo Kampuni ya *H-YOUNG* kutoka Kenya, ndiyo ilishinda na kupewa kazi ya ujenzi wa barabara zenye zaidi ya kimomita 80 kule Pemba na hapa Unguja zaidi ya kilomita 70.

Baada ya maelezo mafupi, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inajuwa kama kuna changamoto zilizojitokeza katika barabara alizozitaja. Aidha, mikataba ya kazi hii hairuhusu mkandarasi awe au

asiwe mzalendo, katika kumsimamia mkandarasi mwenzake, badala yake hutafutwa msimamizi ambaye huiwakilisha wizara au serikali, kusimamia kazi zote za mradi wa ujenzi kwa mujibu wa mkataba. Hivyo, hakuna mashaka juu utaratibu wa usimamizi wa mradi huo.

(b) Serikali ilichukuwa hatua za kuwaandikia maagizo ya kurekebisha dosari zote, ambazo zilijitokeza ndani ya muda wa uangalizi wa barabara hizo, na kampuni ya *H-YOUNG* na *MECCO*, zilifanya marekebisho kwenye maeneo ambayo yalionekana yanahitilafu.

(c) Baada ya mkandarasi kukamilisha mradi pamoja na marekebisho aliyotakiwa kuyarekebisha, kulijitokeza dosari kubwa za kiufundi hasa kwenye baadhi ya maeneo ya mjazo mkubwa wa udongo, barabara ya Mtambwe-Bahanasa, wakati tayari mkandarasi alishakabidhi barabara hizo serikalini.

Kwa kuwa mradi huo ulikuwa chini ya *MCA-T*, kulifanyika uchunguzi na kubainika kuwa kosa halikuwa la mkandarasi. Hivyo, *MCA-T* iliamua sehemu zilizoharibika zifanyiwe matengenezo kwa kutumia fedha za *SMT*, kwa vile akaunti ya *MCC* kwa wakati ule ilikuwa tayari imefungwa. Kazi ya matengenezo hayo ilipewa Kampuni ya *MECCO* baada ya kushinda zabuni, mkandarasi tayari ameshakamilisha kazi ya matengenezo hayo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Je, ni sababu zili zilizopelekea kuikubali barabara mpya ambayo imejaa viraka, badala ya kumuambia zile sehemu ambazo zimeathirika kujenga vipande vile. Leo ukiangalia barabara ina michirizi ya viraka.

Kwa nini nguo mpya iwe na viraka, na barabara mpya tunaikubali serikali na tunaipokea ikiwa katika hali ya vipande vipande vya viraka. Ukienda sasa hivi utaviona, ni kwa nini na ni sababu zipi zilizopelekea kuikubali barabara kama hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, sisi barabara baada ya mkandarasi kuzijenga huwa tunapewa miezi sita baadae ndio anatukabidhi rasami. Lakini kama nilivyosema barabara hizi za *MCC*, zilikuwa katika mkataba maalum na SMT. Lakini baada ya kuonekana kweli zile barabara zina matatizo, ndio wakakubali kutoa dola milioni 1,680, 000 kwa ajili ya kufanyia marekebisho na hivi sasa zile barabara baada ya

mkandarasi kuzifanyia marekebisho, tumepewa tena miezi sita ili kuhakikisha kwamba zile kasoro hazipo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimezitembelea barabara hizi zote, kusema kweli kuna barabara hiyo aliyosema, kuna barabara ya Kojani, Dikoni, Kangagani barabara hizo sasa hivi zimetengenezwa tena katika ukarabati wa hali ya juu sana, na tunampongeza sana mkandarasi *MECCO*, kwa kufanyakazi kwa ufanisi.

Mhe.Naibu Spika, mimi namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba, sisi tutaendelea barabara kabla ya kukabidhiwa kama kutakuwa na matatizo mengine, basi hatutosita kumtaka mkandarasi huyu wa pili *MECCO* aliyepewa, aturejeshee tena katika kufanya ukarabati. Namuomba Mhe. Mwakilishi, atuamini na sisi serikali tutachukua hatua yoyote ambayo tutahakikisha kwamba ile barabara itakuwa katika viwango, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Said Omar Said: Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa barabara hizo zimeshafikia kupasuka, na mpaka leo kuna baadhi ya wananchi wa Melisita hawajalipwa fidia zao kwa ajili ya kuondolewa nyumba zao kwa ajili ya barabara ile.

Je, Mhe. Naibu Waziri, ni lini utakwenda kuonana na uongozi wa Shehia ya Mgogoni ili kupata hali halisi ya suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, niko tayari kukutana naye na kwenda kuangalia hiyo hali halisi ya hao wananchi ambao wana kero zao, ili tuangalie ni kero zipi, kwa sababu sasa hivi barabara nyingi hasa hizi za *MCC* tayari tumeshalipa fidia kwa wahusika. Ahsante sana, tunalipokea ombi lako na tutalifanyia kazi.

Nam. 98

Kuhamishwa Watu Wanaokaa Maeneo Hatarishi

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: (Kny: Mhe. Mihayo Juma N'hunga) - Aliuliza:-

Serikali imekuwa ikishuhudia madhara tofauti kutokana na mvua kwa kuathiri makazi ya wananchi.

Je, ni lini serikali itatoa uamuzi wa kuwahamisha watu waliomo katika maeneo hatarishi, kwa kuwatafutia viwanja ambavyo vitakuwa vimepangwa hasa kwa utaratibu wa Mipango Miji.

UTARATIBU

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Naomba tutazame kanuni muongozo wa kifungu cha 39, kuhusu muda wa maswali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nimeona lakini kuna dakika 15 za ziada na hizo ndio ambazo tunazitumia, nafikiri hili swali letu litakuwa ni la mwisho kabisa. Kwa hivyo, tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 98 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kila mwaka wakati wa msimu wa mvua kumekuwa na maafa ambayo yanaathiri baadhi ya wananchi, serikali tayari imeshalifanyia kazi na inaendelea kulifanyia kazi suala hili kwa kupitia taasisi zake tofauti.

Kuna wananchi wengi wamo katika maeneo hatarishi walishapewa viwanja na matokeo yake wengi wameviuza na wengine hawajakuwa tayari kuviendeleza. Viwanja hivyo havijajengwa kwa muda mrefu sasa, lakini hata hivyo serikali inaangalia maeneo mbadala, na pale yatakapopatikana utaratibu utaandaliwa katika kuhakikisha inaendelea kujali maslahi ya wananchi wake.

Kwa mfano, Jimbo la Amani bonde la Sebleni walipewa viwanja mwaka 1992, eneo la Magogoni, Mwanakwerekwe na Mpendae wameuza na wamerudi katika makazi yao ya kawaida. Kumbukumbu zetu zinaonesha walipewa mpaka baadhi ya vifaa vya ujenzi kama vile mabati.

Pia, kuna watu walihamishwa na kupewa nyumba za Michenzani badala yake wameziuza kwa watu wenye uwezo na wao kurudi kwenye maeneo hatarishi. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Pamoja na malalamiko ya muda mrefu ya maeneo ambayo viwanja vimetolewa kwa watu hawa waathirika hawajaviendeleza na viwanja vyenginevyo. Je, ni

lini Serikali itavifuta viwanja vile na kuwapatia watu waliokuwa tayari kuviendeleza katika suala la ujenzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nisharti na Mazingira: Ni hapo baada ya utaratibu kukamilika, ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi, 2016

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, Majadiliano yanaendelea ninao wachangiaji 10 na kama utaratibu wetu unavyotwambia kwamba tutakuwa tuna dakika 15 kila mmoja, ningewaomba sana Waheshimiwa, wachunge wakati hasa katika michango yao ili tuweze kwa hawa wote ambao wameomba kuchangia waweze kuchangia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa imani yako na kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo leo, kwanza tuseme tu Serikali imetuletea mswada wa mafuta na gesi asilia ni mswada muhimu sana kwetu na kwa kizazi chetu, niseme naunga mkono kwa asilimia zote mia ilimradi tu kwa manufaa ya wnanchi wa Mpendae tuone mafuta haya yamechimbwa kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni mwema sana kwa maendeleo mengi ya taifa leo lakini hususan kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Afya, basi tutapata dawa na mambo mengine kiurahisi zaidi, tunaitakia mema sana Serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda kwenye vifungu kidogo sana kwa sababu vifungu vingi tayari vimeelezewa lakini na mimi nitaelezea si zaidi ya vifungu 6 ambavyo nitajaribu kwenda kidogo baada ya kidogo ili niweze kuchunga muda wako.

Nianze kwanye kifungu 21, ukurasa wa 78 wa mswada huu wenye *marginal note*; Kinga zaidi ya Wajumbe wa bodi na maafisa wa mamlaka, Mhe. Naibu Spika, kuwaekea kinga Wajumbe wa bodi hapa naona sio sahihi, kwa sababu rasilimali tunazowapa ni kubwa mno tukianza kuwawekea kinga imeandikwa

hapa; "Watafanya kazi kwa nia njema kabisa". Sasa atakapokuja Mhe. Waziri, nataka anitafsirie hii nia njema ni ipi, kwa sababu wengine wanasema nia njema hata ya kuelekea *Jahanam*, ni nia njema tu, mtu anaweza kutuibia ni nia njema tu. Lakini tunawapa rasilimali kubwa, hatuwezi kuwa tunawawekea kinga, mimi hili Mhe. Naibu Spika, naomba tuweke marekebisho hapa na nahisi nitaleta *Amendment* kuona jinsi gani tunaweza tukafanikisha suala hili, lakini kuwawekea kinga hili halikubaliki.

Mhe. Naibu Spika, tunaendelea kwenye ukurasa wa 80, kwenye kifungu cha 31, kuhusu Ripoti za mwaka, kifungu 31(3) Mhe. Naibu Spika, Naomba hapa ninukuu:

Kifungu kinasema:

"Waziri ndani ya miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya mwaka atawasilisha taarifa hiyo katika Baraza la Wawakilishi na taarifa nyengine ambazo ataona zinafaa".

Mhe. Spika, nije kwenye *reference* wakati tulipokuwa tunazungumza suala la bajeti ya Wizara ya Fedha kuona jinsi gani taarifa hizi haziletwi, sasa naomba ninukuu *Hansard* ambayo Mhe. Waziri wa Ardh,i Maji, Nishati na Mazingira, alipokuwa akisema:

"Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimjibu Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kuhusu hoja yake ya ripoti, jamani lazima tuelewe kwamba kila kitu kina utaratibu wake sheria haiendi, sheria ipo lakini na sheria pia inaongozwa na kanuni, utaratibu wa miongozo mbali mbali ndani ya Baraza hili kuna taratibu zake, utaratibu wa Baraza katika kuwasilisha ripoti ni utekelezaji wa maamuzi ambayo sisi kama Mawaziri wao sio mie, tunatoa kabla ya bajeti ndio maana tunatoa nini kutekeleza".

Mhe. Naibu Spika, napata ukakasi sana kuwa kama sheria hizi ambazo tunazitunga hapa zitaletwa ndani ya Baraza la Wawakilishi, hii inaeleza wazi kabisa tunatunga sheria kuleta *annual report* katika Baraza la Wawakilishi, lakini taasisi na mashirika ya umma ambayo tunatunga sheria hii hapa hailetwi Barazani, huu ni uvunjifu wa sheria, Serikali inavunja sheria na ndio maana kwa mujibu wa hoja yangu binafsi ambayo nataraji sana kuiwasilisha Ijumaa itakuwa namna hiyo.

Sasa hizi ni kitu chengine na uwasilishaji ni kitu chengine kwamba Mawaziri wamekuwa hawawasilishi, tunaomba sana kama itakuwa hawataki kuwasilisha

tuanze kuiondoa kabla hatujatunga sheria hii ili tuweke sawa na mipaka yetu tuone tumefikia wapi.

Mhe. Naibu Spika, niende tena kwenye ukurasa wa 49, kuhusu Utaratibu wa zabuni, utaratibu wa zabuni sote tunauelewa, taratibu za zabuni hizi hazifuati sheria ya nchi hii na ndio maana uzoefu unaonesha sana kuwa taasisi zetu nyingi hazitoi zabuni kama inavyofuatwa na sheria yenyewe tunakwenda ovyo ovyo. Sasa tunakwenda kule kwenye kupambana na makampuni makubwa na yenye pesa nyingi, ni hatari kwa wananchi wetu, anaweza akanunuliwa mtu mzima mzima hapa, akatolewa ndani akawekwa nje. Sasa tunataka kusema tu hata suala hili la Sheria na Manunuzi limeanza kupitwa na wakati sana na litatu-*cost* sana.

Mimi ningeomba Serikali ilete *amendment* kubadilisha suala hili, kwa sababu suala hili ni muhimu sana ukizingatia utangazaji wa zabuni hizi ni mkubwa na wachimbaji hawa wa makampuni ya gesi asilia ni makampuni makubwa sana, niombe sasa hivi Serikali ifuate taratibu hizi za zabuni lakini vile vile ikizingatia na kufuta au kuleta *amendment* ya Sheria ya manunuzi, ambayo tunaihisi imeanza kupitwa na wakati mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende tena kwenye kifungu cha 62. Mhe. Naibu Spika, Tasmini na uchunguzi wa maeneo. Mamlaka inaweza kuagiza kwa *notice* ya maandishi kwa kampuni yenye leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kufanya tafiti ndani ya kipindi kisichozidi miaka miwili, na kwa utafiti wa mafuta ni miaka mitatu, watafidi wa gesi asilia ufanywe kwa miaka miwili, huo upembuzi yakinifu utakaofanywa. Sasa nimejaribu kuangalia wenzetu Tanzania Bara uzoefu unasema nimeangalia Sheria ya Tanzania Bara, lakini vile vile nimeangalia Sheria ya Botswana, wao wanasema hazikuwekwa. Hazikuwekwa kwenye muda maalum na sheria hizi mbadala na mamlaka hii amepewa Mhe. Waziri, kuona kwa sababu inategemea, aidha ndani ya bahari au nchi kavu, wenyewe wanasema wataalam *offshore or onshore*, ndio utatekeleza na unategemea jinsi gani wa kuweza kuweka muda maalumu. Mimi nafikiri tumpe madaraka Mhe. Waziri, hapa ili aone jinsi gani yeye anaweza kutoa na sehemu husika ikiwa *offshore* au *onshore.*

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee tena kwenye kifungu namba 72, ukurasa wa 96, kuhusu Uzalishaji wa pamoja. Kifungu kinasema;

"Waziri anaweza kutekeleza kwamba, iwapo mkusanyiko wa mafuta na gesi asilia, utapatikana katika eneo moja au zaidi la nje au la mkataba huu,

ni uzalishaji wa namna nzuri utakaohakikisha ufanisi mzuri wa shughuli za mafuta na gesi".

Mhe. Naibu Spika, kama hatutokuwa makini kwenye kifungu hichi tunaweza tukasababisha mizozo mbali mbali na migogoro mbali mbali inawea kutokea hapa, ni lazima kabla hatujaanza kutoa leseni ya mafuta na vitalu, tuweze kuona mipaka imeendaje.

Namsisitiza sana Mhe. Waziri, atakapokuja hili aweze kunijibu vizuri sana tumegawaje mipaka hii, kwa sababu inaweza tukasababisha adha kubwa sana kwa wananchi, na mipaka hii ndani ya vitalu hivyo ili ionekane kwa pamoja kwa sababu Makampuni haya tukishakuwapa leseni tunaweza kusababisha migogoro mikubwa sana ambayo inaweza kutokea.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimalizie kwa kifungu 99 na naomba nikinukuu:

"Endapo kati shughuli za ufuatiliaji na uchimbaji wa mafuta na gesi kwenye fidia hizi asilia, kampuni na mkandarasi ataingilia haki za mkaazi halali wa ardhi yoyote kulingana na shughuli zinazofanyika kampuni na mkandarasi, watamlipa mkaazi halali fidia inayofaa kwa mjibu wa Sheria ya usimamizi wa ardhi".

Mhe. Naibu Spika, naanza kupata ukakasi mkubwa sana, kifungu hichi naona kinaweza kuelekeza kitu kimoja, kinaweza kisitende haki kwa muathirika ambaye huyu mkaazi atakayekutikana katika eneo lake, kinaweza kisitende haki kabisa kabisa. Nafikiri kuna haja ya kuanza kuzipitia sheria zetu kwanza, tuweze kuzipitia sheria zetu za usimamizi wa ardhi, bado Sheria za usimamizi wa ardhi zinalega lega mno na hazifuatwi. Zanzibar tumekuwa matajiri wakubwa sana wa kuunda sheria lakini hatuzifuati, hata Serikali yenyewe inaanza kuzipinda pinda, sasa ningeomba tu tuanze kutilia mkazo kwenye Sheria hizi za usimamizi wa ardhi ili kuepusha migogoro ambayo inawaza ikatokea baina ya wananchi na wawekezaji, lakini vile vile wakati wa kulipa fidia hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Mwanasheria Mkuu, arudi katika Sheria nam. 7 ya mwaka 2010 ya Sheria ya uvuvi, wasi wasi wangu ninaoupata hapa kuwa hata sheria hii itakuwa inaingiliana wavuvi wenzangu kule watakuwa wanapata kadhia kama ile ya mwanzo tuliyowapa wawekezaji wa mahoteli, wawekezaji wa mahoteli tuliwapa fukwe tukaona adha kubwa inasababishwa na wawekezaji wale kuambiwa hapa msiweke makaazi, hapa hapana diko, hapa msipite, hapa msivue, sasa wasi wasi ninaoupata huu ndio maana nikaelekeza

Sheria nam. 7 ya mwaka 2010. Mwanasheria Mkuu aitizame kwa uangalifu ili aweze kuona wavuvi wenzangu wasije wakapata tabu, wasije wakaambiwa huku msivue, hapa hapawi hivi, tuweze kutoa elimu na mapema mno na tuone basi jinsi gani tunaweza kuwafaidisha wavuvi wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa leo niseme hilo tu na niseme naunga mkono, lakini nipatiwe majibu wa hizi sheria ambazo nimezizungumza kwa Mwanasheria Mkuu, lakini na hii *Annual report* na nikaomba nioneshe *hansard* ambayo Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, kwa maneno yake mwenyewe, leo namwambia *hansard* zinakaa ili aweze kuona jinsi gani ripoti hizi zinaletwa Barazani. Pengine alikuwa hajui kwa njia moja au nyengine, lakini nadhani kuanzia leo ameijua kwamba ripoti hizi na Mungu bariki yeye ndiye anayetunga sheria hii, na sheria hii inazungumzia hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Sheha Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi angalau kuchangia mawili matatu katika Mswada huu ulio mbele yetu. Kwanza sina budi niipongeze Serikali kupitia vyombo vyake vyote ambavyo kuwa vimeandaa Mswada huu, hadi leo mbele yetu ikawa ndio tunaanza kuujadili na hatimae kuufanyia kazi.

Lakini mimi katika mchango wangu katika Mswada huu ni sehemu ndogo sana kwa sababu nyingi zimeshazungumzwa na kwa kuokoa muda naomba nikumbushie vitu viwili tu nilivyoviona mimi, ambavyo kuwa sijavisikia katika Mswada huu. Suala zima la masharti kama ilivyozungumzwa katika kifungu 15 cha Mswada huu kuhusu Masharti ya Wajumbe wa Bodi pamoja na kifungu namba 17, kuhusu Masharti ya Uteuzi wa Mkurugenzi Muendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, masharti hapa yamesema kwamba;

> "Mkurugenzi Muendeshaji awe na uzoefu usiopungua miaka 10 ya fani".

Kwenye kifungu namba 15 kinasema;

> "Mwenyekiti wa Wajumbe wa bodi asipungue uzoefu wa miaka 10 ya fani".

Sasa wasi wasi wangu mimi kwamba kama tunataka Mzanzibari ambaye kuwa ashiriki katika shughuli hizi, awe na uchungu na kuwa muaminifu wa nchi

yake, sijui hizi sifa kama tutaweza kuzipata. Sababu zangu na hofu yangu ni kwamba leo jambo hili tunalianza uzoefu wa fani hii ataupata wapi kama tunataka Mzanzibari.

Ndio pale tulipokuwa tunazungumza masuala ya ajira kwamba kuleta masharti ya mfanyakazi nafasi inayoombwa kwamba awe na masharti ya miaka mitano, kwa kweli wengi tutawaacha pembeni na hatimae nafasi hizi zitachukuliwa na wageni ambao kuwa sisi lengo letu tunataka mradi huu ukamatwe na Wazanzibari wenyewe, sasa wasi wasi wangu mimi naomba Waziri atakapokuja anindolee ili haya masharti pengine atayafafanua vizuri zaidi masharti haya miaka kumi, au miaka saba yametajwa katika Mswada huu kwamba ndio iwe miongoni mwa sifa, bado mimi nina wasi wasi wangu kwamba tutaweza kumpata mtu wa aina hiyo. Hivyo, itabidi tuchukue kwa wenzetu ambao kuwa tayari wameshalianza jambo hili.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, pia katika Mswada huu sikuliona suala la usalama sehemu ambazo kuwa tutaekeza hasa tukizingatia mradi huu pengine utaanza bahari kuu, hali yetu tunaiona ya ulinzi wetu, kwanza nashukuru si mdogo lakini kuna haja uongezwe nguvu zaidi, bahati kuu ni maeneo makubwa sana kutokana na visiwa, je, tumejipanga vipi watu hawa wakiwepo kazini hawatoweza kudhurika kwanza kuweka mali zao zile ambazo watawekeza pale, usalama wa mali zao wale wawekezaji, lakini pia usalama wa roho zao, tukizingatia kwamba nchi yetu sasa hivi inanyemelewa na watu ambao hawaitendei mema nchi hii kwa kila pemba na tunaona dalili ambazokuwa tayari zimejitokeza.

Je, Serikali itaweza kupanga vipi katika kusimamia usalama wa wawekezaji hawa pamoja na mali zao, hili ni jambo ambalo naona nilikumbushie kabla hatujalianza kama Waziri alisahau au atakapokuja atanieleza tumejipanga vipi kwa suala la ulinzi na usalama.

Kwa sababu ukizingatia vyombo vyetu ambavyo tumekuwa navyo havifiki hata baadhi ya wavuvi wanakuja kutuibia samaki wetu hapa kupitia bahari kuu hiyo. Leo watu wanakwenda kukaa kwa muda usiopungua miaka 5, 10 wapo kule, maharamia wanapita kwa baharini huko, je, watu hawa watakuwa na usalama gani? Huu ndio mchango wangu ni mfupi lakini nimeona niutoe niweze kupata maelezo na mimi roho yangu ikae vizuri kuona kwamba watu hawa hapa tunapoekeza panakuwa salama.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki nichukuwe muda mwingi, naunga mkono mswada huu mia juu ya mia.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie machache ambayo yamo katika sheria hii. Kwanza niipongeze Serikali kwa ujumla wake kwa kuleta mswada huu, lakini pia niipongeze Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kazi kubwa walioifanya wakishirikiana na Wizara ya Ardhi na Nishati, kuhakikisha mswada huu unaandikia lakini pia kuhakikisha kwamba mswada unakuja katika Baraza.

Mhe. Naibu Spika, sisi wanasiasa tunasema sitaki kupiga siasa sana kwa sababu najua wajumbe waliotangulia wameshasema, naomba niende moja kwa moja kwenye mswada wenyewe. Kwa kuanzia naomba nianze na hotuba ya Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana kwa kazi kubwa aliyoifanya, nilikuwa nasoma hotuba yake kwa ujumla nimeona wamefanya kazi katika kamati kwa muda siku nane. Kwa hivyo, tuwapongeze kwa kazi kubwa walioifanya kwa niaba yetu na tunaamini kwamba Serikali itasikiliza yale ambayo Kamati imependekeza, pia itasikiliza yale ambayo wajumbe wamependekeza kama watakavyoona inafaa kwa sababu *at the end of it* mswada hauendi kutufaa sisi wamoja wamoja isipokuwa ni kwa manufaa ya Wazanzibari wote kama wajumbe wengine walivyotangulia kusema.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kuanzia naomba nianze na kifungu cha 6(2), ambacho kinampa *power* waziri kinazungumzia *duties* na *responsibilities of the ministers*. Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hiki kifungu cha 6(2)(d), kinasema kwamba;

"*Minister … ensure full accountability, transparency and efficiency in developing a system of revenues management and tax collection and their planned expenditures".*

Nilikuwa ninajiuliza *minister* wa nishati atafanya haya yote kwa *power* gani, kwa sababu inaonekana kwamba hizi *responsibilities* ambazo amepewa *minister* wa nishati ni *responsibilities* za *Minister* wa *Finance*. Kwa hivyo, nilikuwa naomba na taasisi zipo ambazo zinafanya hizi kazi, kwa hivyo, nilikuwa naomba Serikali *power* ndio apewe *minister* kwa sababu yeye ndio *responsible* kwa mswada huu wote, lakini sio vibaya mswada ukatambua pia akishirikiana na *Minister of Finance*, kwa sababu tunajua *Minister of Finance*, yeye ndio yuko *responsible* kwa hizi *duties* ambazo wamepewa *minister* anayehusika na mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nikiingia katika kifungu cha 8, kinazungumzia *Functions and Responsibilities of the authority*, na kifungu cha 8(2)(e) kinazungumzia kwamba; *the authority* itamu-*advise the minister in the*

granting and revocation of licenses. Pendekezo langu kwamba hiki kifungu cha 8(2) kinaonesha *functions* za mamlaka katika kumu-*advise* waziri. Lakini ukiangalia kifungu cha 19(2), kumetajwa na mambo mengine ambayo waziri atakua anatakiwa kufanya, lakini *authority* imepewa mamlaka ya ku-*grant* and ku- *revocate the license*. Lakini ukiangalia huku kuna mambo mengine ambayo pia *minister* anatakisa kufanya, lakini *authority* haijapewa mamlaka yaku-*advise* kwenye yale mambo.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba kifungu hiki pia kiipe *power authority* kama ilivyopewa katika kifungu cha 19(2). Mhe. Naibu Spika, wakati tukipitisha tukikaa kama kamati nadhani tutaelewana vizuri na Serikali.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 9, kinasema kwamba;

"*The minister shall give directives in writing to the authority with respect to the Zanzibar Oil and Gas Policy, for public interest".*

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba kifungu kinasomeka kwamba; "*The minister may...",* Neno '*may'* linaonesha kuwa anaweza akafanya au anaweza asifanye. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kifungu hiki cha 9, kisomeke '*shall'* na marekebisho ya Serikali yatavyokuja tutazidi kuelewana zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, katika kifungu cha 11(1), kinaonesha *consequences* ambazo Kampuni na Mkandarasi zitapata watakaposhindwa ku-*comply* au wataposhindwa kufuata yale maelekezo ya *minister*. Lakini hakuna sehemu ambayo inaonesha kwamba, mamlaka itakaposhindwa kufata *directives* za waziri kutakuwa na *consequences* gani, wakati tunajua kwamba mamlaka ambayo itakayoundwa itakuwa chini ya waziri na waziri anatakiwa kutoa *directives* kwa hii mamlaka. Kwa hivyo, mamlaka itakaposhindwa kufata *directives* za waziri hakuna *consequences* ambazo zimeoneshwa.

Mhe. Naibu Spika, pia, kifungu cha 14, kinaonesha mamlaka ya *Board of Directors* ambayo inatakiwa ku-*recommend* hatua za kinidhamu kwa *Managing Director*. Mhe. Naibu Spika, *concern* yangu hapa ni kwamba *Managing Director* ni *presidential appointee*. Hapa Mamlaka ya Bodi kama Bodi zetu tunavyozijua zinakuwa mara nyingi watu wa nje wanachaguliwa kuja katika hizi bodi.

Sasa *concern* yangu ni kwamba Bodi ita-*recommend* vipi hatua za kinidhamu za kuchukuliwa kwa yule *Managing Director* wakati Bodi haijapewa *power* ya *inquire,* yaani ya kumchunguza yule *Managing Director*, kwa sababu kutoa

recommendation juu ya mtu ni lazima umchunguze halafu utoe mapendekezo ya kinidhamu ambayo yanatakiwa kuchukuliwa. Lakini Bodi haijapewa *power* ya kumchunguza lakini inapewa *power* ya kuandika mapendekezo kwa Mhe. Rais, kwamba huyu hafai, wataandikaje mapendekezo kwamba huyu hafai wakati hawajapewa *power* ya kumchunguza yule ambaye wanatakiwa wamuandikie mapendekezo.

Jambo jengine ni kwamba pia katika kifungu hiki hiki bodi imepewa *power* ya kuchukua hatua za kinidhamu juu ya *staff authority* na tunajua kwamba watumishi wa Serikali wote wanawajibika chini ya Tume ya Utumishi wa Serikali. Sasa kwa nini Bodi inapewa *power* ya ku-*deals* na *staffs* ambao wao hawana *power* ya kuajiri na badala yake *staffs* hawa wanaajiriwa na ile Tume ya Utumishi, lakini Bodi inapewa *power* ya kuadhibu au ya kuchukua hatua za kinidhamu juu ya hawa *staffs* ambao watakuwa chini ya mamlaka. Kwa hivyo, nilikuwa naona hii sio sahihi, nadhani utaratibu ule ule utumike kwamba watumishi wa umma wawe chini ya Utumishi wa Umma na kila kitu kinachohusiana na wao kichukuliwe hatua chini ya Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Serikali ikija ije na maelezo sahihi juu ya hii.

Kifungu chengine cha 19, kinaelezea kwamba *heads of unit* wa *authority* watateuliwa na Bodi. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba hizi Bodi zetu mara nyingi inakuwa wazee wetu washastaafu huko, hawana la kufanya hatimae wanaletwa kwenye Bodi wajishikize shikize mpaka muda wao utakapoisha. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najiuliza hawa Wajumbe wa Bodi watawajuaje hawa *heads of unit* au *heads of unit* wa *department* ambazo zitaundwa, nadhani utaratibu ule ule utumike kwamba *heads of unit* aachiwe *MD* mwenyewe ateue na Bodi i-*approve* tu kwa wale ambao wameteuliwa. *Otherwise*, Mhe. Naibu Spika, itakuwa tunatengeneza malalamiko ya hapa na pale ambayo yatakuwa hayana tija.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho mengine ambayo niliyokuwa nayo ni madogo madogo ambayo yatahusiana kwenye *section* ya 43, *section* 47 na *section* 53 ambayo yanataka maelezo kidogo tu kuweka sawa ili tupitishe mswada wetu.

Mhe. Naibu Spika, sitaki kuchukua muda mkubwa baada ya kwisha kusema hayo, naomba niunge mkono mswada huu kwa asilimia 50 na asilimia 50 nitaunga mkono wakati Serikali ikinipa maelezo ambayo yataniingia, yatanifikisha na nikubaliane nao.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Ahsante.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Gesi Asilia hapa Zanzibar. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* kuniwezesha leo hii kuwepo tena katika kikao hiki cha Baraza lako tukufu. Lakini pia nikushukuru na wewe kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu. Kwa kuwa tumeshauchangia sana mswada huu sitokuwa na mchango mkubwa lakini naona ni vyema na mimi nitoe yangu kidogo kuhusiana na mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, tunaelekea katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi hapa Zanzibar, sasa nataka tuelewe kwamba huu ni kama mche ulioletwa hapa katika shamba lenye mbolea tukatakiwa wafanyakazi wa shamba hili kuutilia maji na kuupalilia mpaka kufikia kutoa matunda. Sasa kufikia hatua hiyo, inahitaji uvumilivu wa hali ya juu, mche mpaka kufikia matunda lazima tuwe wavumilivu, kwamba unapokuwa na uvumilivu unakuwa unajengeka imani, kwa hivyo, kwanza tuwe na uvumilivu wa hili kwa Wazanzibari wote ili tujengeke imani ya kuwepo mafuta katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Tutumie nafasi hii ya uvumilivu kama walilvyoitumia wazazi wetu waliopita waliotupandia mikarafuu ambayo leo tunaihitaji, tunaitumia na tunaishi kwa kutegemea hiyo mikarafuu.Wazee wetu walianza kufanya utafiti mwanzo wapi inaota mikarafuu, kila jambo linakwenda hatua kwa hatua. Baada ya kupata wataalam wakagundua Pemba ni ardhi nzuri ya kupanda mikarafuu ikapandwa, ikaletwa mbegu wazee wakaanza kuifanyia kazi. Wazee hao nadhani kama wapo ni wachache sana waliofanya kazi hiyo, lakini kwanza walipanda baadae wakaipalilia na kuishughulikia wengine hawapo tena, lakini wengine sasa tunatumia na wengine wanaokuja pia watatumia.

Lakini walianza na uvumilivu na uaminifu ili kuamini kweli baada ya wataalam washagundua hapa inakuwa na wao wakafanya kazi na baadae leo tunapata tija Zanzibar nzima. Kwa hivyo, suala hili lazima tujenge imani kwamba mafuta tunayo na kwa nini tusiwe nayo mafuta Zanzibar, kwa sababu viashiria vyote vya kupatikana mafuta tunavyo hapa Zanzibar. Kila kitu kina asili yake, kwa hivyo, ule uasili wa hayo mafuta yapo.

Mhe. Naibu Spika, tuwaenzi sana wataalam wetu waliopo nchini, wataalam hawa ndio watakaotuletea maendeleo ya nchi yetu kupitia katika suala hili la mafuta na gesi. Lazima tuwaamini kwanza na kuamini bila vitendo, imani bila kitendo haifanyi kazi. Baada ya kuamini tuwaenzi, tuwathamini katika kila nyanja za kielimu na za kimaslahi ili tuwajenge wafanyakazi kizalendo. Bila kuwajenga hawawezi wakafanya kazi kizalendo kama tunavyokusudia

wafanye. Jambo hili linahitaji utaalamu, uaminifu na uadilifu mkubwa sana na hayo tutayapata kama tutawaenzi wataalam wetu.

Mhe. Naibu Spika, suala dogo tu la kutafuta maji, maji yapo kila pahala hapa lakini utapompeleka mtaalamu wa kukuchimbia yale maji, anaweza yeye akatumia utaalamu wake, maji yapo lakini kwa kutumia utaalamu wake ambao wewe huuelewi akakwambia aah, maji hayapatikani.

Siku moja nilikuwa nazungumza na mtaalamu mmoja wa uchimbaji wa kisima, akaniambia kwamba sisi tunaweza tukamtia hasara yule tunayemchimbia kisima, kwa sababu gani, Naweza nikachimba kisima nikaona maji tayari haya basi nikaweka jiwe kwa sababu kule anakochimba yuko peke yake. Lakini nimeshayaelewa hapa ndio penye jicho la maji basi naweka jiwe halafu mimi natoka, nikitoka namwambia mzee pana kazi kubwa hapa, kwa hivyo, itabidi kutokana na mapatano yetu itabidi uniongezee kitu au mimi uniruhusu niende nikafanye kazi zangu kama hizi sehemu nyengine.

Basi anamkwapua tena pale kidogo ndio anaingia kule hafanyi kazi yoyote, kwa sababu kazi ameshaimaliza. Kazi yake ni moja tu kwenda kuondoa lile jiwe pale lakini ameshalipwa mara mbili. Sasa hayo ni maji, je, mafuta, hapa inahitaji wataalamu wetu tuanze vizuri ili wawe waadilifu na wawe bega kwa bega pamoja na wataalamu watakaokuja kushirikiana nao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tumeshapewa taarifa kamili kamba mafuta yapo, maana yake, toka zamani mbona hatujapewa hii kuijadili, lakini ni kwamba yapo na wanakuja watu kwa kuwa yapo na wataendelea kuja kwa kuwa yapo mafuta. Kwa kuwa mafuta yapo na kwa kuwa tumeshapewa hii sheria, basi tunaifanyia kazi, sasa tuwaache wataalamu waendelee na shughuli tuliowapa hali ya kuwaamini kabisa, tuwaache wananchi waendelee na kazi zao za kawaida…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Said Oma Said: Nashukuru sana Mheshimiwa, zitanitosha hizo.

Kwa hiyo, tuwaache watu waendelee na shughuli zao za kawaida kwamba wasione hili ni jambo la papo kwa papo, hili ni jambo lenye uvumilivu kama nilivyosema. Hatua nyingi sana zitachukuliwa mpaka kufikia kuyapata mafuta haya.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa tunajua kwamba, Zanzibar ni visiwa vidogo vyenye wakaazi wengi na wengi wao ni wanyonge, na wanyonge hao hao wanatumia ardhi hiyo hiyo ndogo kwa ajili ya maisha yao. Kwa kuwa sisi ni wengi kulingana na ardhi tuliyonayo kila mmoja anaishi kwa kutegemea kijisehemu kidogo tu cha ardhi ambacho alirithi tokea huko kwa mababu zao. Lakini sehemu hiyo hiyo ndogo ndio anayoitegemea kwa maisha yake ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, ninalotaka kusema ni kwamba, lazima hapa pawekwe utaratibu maalum kuhusu hawa watakaohamishwa katika maeneo yale kwa ajili hii ili na wao waishi vizuri kwa kutegemea ardhi yao hiyo hiyo. Kama tulivyopendekeza nasisitiza tena kwamba hapa kwa yule atakayehusika na kuondoshwa katika sehemu ile, hapa fidia yake isiangaliwe Sheria ya ardhi ila patungwe utaratibu ambao utampa yeye maisha endelevu. Lakini kama utamuhamisha mtu pale anapotegemea ukampa milioni tatu, milioni tatu mara ngapi zinazotoka huko nyuma mpaka leo kwa pale pale. Hivyo, tunasisitiza sana kuundwe utaratibu mzuri kwa watu hao.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niwaombe tu wenzangu tuupitishe mswada huu kwa salama na amani, mswada huu hauna mashaka yoyote, umerekebishwa kila kipengele, hauna wasi wasi wowote, kamati imekaa muda wa siku nane ili kuujadili huu na umeona hauna mashaka yoyote kwa Wazanzibari. Tusije tukageuka mtu na bosi wake, anamwambia bosi wake kwamba kutokana na hali ya nyumba ilivyo umasikini tulionao…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Wingwi, tunakubali mswada huu na tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Said Soud Said (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza nataka nichukue nafasi ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama ni msimamizi mkuu wa serikali. Vile vile, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais kwa uteuzi wake wa wataalamu ambao kwa safari nyingi ambazo wamekwenda katika nchi yetu na nje ya nchi yetu kutafiti namna gani ya uchimbaji wa mafuta, hasara zake, faida yake na yale ambayo yanajitokeza, wameweza kufanya kazi nzuri na kwa maana hiyo napongeza jitihada yao ambayo wameifanya.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nataka niseme ndani ya nchi yoyote ile duniani kunakuwa na wanasiasa, kuna wabeba mikoba ya wanasiasa, kuna wakereketwa, kuna wafurukutwa na kuna watu wasiojielewa wanafanya nini ndani ya harakati zao.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba unaweza kuwa Mwakilishi lakini si mwanasiasa, na kwa maana hiyo unatakiwa uheshimu taratibu ambazo zimechukuliwa na viongozi wako wa juu wa siasa wanaongoza nchi kwa madhumuni na faida ya nchi na hatimae uweze kuchangia lile ambalo liko mbele ya meza yako. Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwaambia baadhi ya Wawakilishi kwamba mipaka ya bahari inafatiliwa na serikali, mipaka ya *block* inafatiliwa na serikali na serikali inajitambua nini inataka kufanya. Na vile vile ni wakati muafaka wa kuelewa kwamba sasa hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendeshwa na Rais mzalendo, Rais anayependa watu, Rais anayefikiria watu na Rais anayejitambua.

Mhe. Naibu Spika, ushahidi tunauona hivi sasa kwa watu wote wenye umri wa miaka 70 wanalipwa pesa shilingi 20,000/= jambo ambalo hakuna mjukuu wa aina yeyote anayeweza kumpelekea babu yake shilingi 20,000/=, lakini Dkt. Ali Mohammed Shein anazitoa 20,000/= kwa kila mtu bila ya kujali rangi, kabila, wala dini yake.

Huu ni utaratibu ambao umepangwa na serikali yake na kwa maana hiyo uzalendo huu ndio uliomfikishia kuangalia kwamba sasa umefika wakati muafaka wa kuchimba petroli katika visiwa vya Unguja na Pemba. Nampongeza sana, sana pamoja na msaidizi wake Mhe. Makamu wa Pili, na pia nawapongeza mawaziri walioridhia mpango huo. Sasa ni wakati wetu muafaka wawakilishi wote kama watu ambao tumetumwa na wananchi kukubaliana na hoja hii na kuweza kukubali kwamba nchi yetu sasa ipige hatua ya kuchimba mafuta ili kuondoa yale madhila ambayo kwa miaka mingi yametukabili na siku zote tulikuwa tunaambiwa mafuta yapo, yapo, yapo lakini hayachimbwi.

Lakini kwa bahati nzuri wawakilishi waliomo ndani ya Baraza hili ndio kwa mara yao ya kwanza wanaanzisha historia ya kupitisha mswada huu utakaoipeleka Zanzibar kwenye maendeleo, utakayoiondoa Zanzibar katika nchi ya omba omba, itakayoifanya Zanzibar kupiga hatua kwa makundi na hata mtu mmoja mmoja kuweza kufanikiwa na maisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa hakika neema inapotokea mara nyingi yanatokea mambo mbali mbali. Katika mwaka 1945 Kisiwani Pemba zilizaliwa karafuu

nyingi sana, hatima yake karafuu hizo zilipanda bei kwa siku moja, lakini jeuri ya wakulima walifikia hatua ya pesa kuzisokota na wakavutia sigara.

Mhe. Naibu Spika, katika hali kama hiyo ilitokea mwaka 1949 katika Kijiji cha Mchanga Mdogo zikazaliwa chooko nyingi sana, baada ya kuwa chooko ile kutumika kwa ajili ya kula, matokeo yake ilipondwa na hatimae ikajengewa msikiti huo unaotambulika, unaitwa Msikiti Chooko. Kwa vile matokeo yatakayotokea ndani ya uchimbaji wa mafuta, mimi naamini ni neema, na ni neema kubwa ambayo itawafikisha watu kuondoa zile idhilali ambazo zimewakumba na kuondoa zile shida ambazo zinawakwaza kila siku na kufikisha hatua ya watu kujikwamua na hata kusogeza misingi ya Dini ya Kiislamu katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyotambua kitabu chetu kinasema kila mwanamme anatakia aoe wake wanne, tukichimba mafuta hawa wote wataoa wake wanne wanne hawa. Napenda ieleweke kwamba tukichimba mafuta naamini kabisa kwamba Wazanzibari wataoa wake wanne wanne. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu ni neema ambayo inakuja kwa pamoja, kwa makundi na hata mtu mmoja mmoja. (*Makofi*)

Sioni sababu leo ya kwamba tayari tumeshafika hatua hii ambayo wenzetu wamewania miaka mingi iliyopita kutaka kuchimba mafuta lakini ilishindikana kwa migogoro mbali mbali, na mizozo mbali halafu baadae leo tumefika pahala Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na serikali yake wamekubali hoja hii ianzishwe ili watu waondokane na hii hoja, lakini watu wakawa wanabeba maneno ya kwenye vijiwe, wanabeba maneno ya kwenye mizizi ya miembe, wanabeba maneno ya watu wasioitakia mema nchi hii halafu wanayatumbukiza humu. Tunawaambia serikali hii iko makini na hoja ya mafuta itashughulikiwa ipasavyo ili watu waweze kufika pale wanapotaka Zanzibar waliyoikusudia.

Mhe. Naibu Spika, katika hali kama hiyo tunaweza tukafika pahala Wazanzibari tukawa watu ambao kwa makusudi ni vyema tukatambuana, kwa sababu nchi yetu baada ya hoja hii kuanzishwa naamini kwamba wataingia wenzetu wengi sana kutoka nchi mbali mbali kwa ajili ya kuja kutafuta ajira na kwa maana hiyo ajira zitakuwa wazi, kwa sababu wengi wetu hatuna utaalamu na mimi ninavyoielewa mafuta na gesi mpaka bati inatolewa katika uchimbaji wa mafuta. Zile tope tope basi zinatengenezwa mpaka bati.

Sasa kimsingi kama tutakuwa na uwezo wa kuweza kupata *petrol, diesel, oil* na *oil* ziko kwa daraja, girisi, lami, bati, mafuta mazuri, mafuta ya kuendeshea ndege, halafu leo anatokea mtu anakwambia aah, maana yake hii haiwezekani,

inawezekana, wakati umefika Wazanzibari kusema inawezekana. Inawezekana kwa sababu gani Mhe. Naibu Spika? Kwa sababu hakuna serikali yoyote duniani iliyokuwa inataka wananchi wake wapate dhiki, sasa sisi kama serikali tumekubali kuunga mkono jitihada hizi na kuona kwamba serikali inaweza ikaondoa shida za wananchi ambazo kwa muda mrefu zimewapelekea ni vikwazo vya maisha na maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba kila mkulima wa nchi hii atakuwa tayari kusimamia mikarafuu yake, minazi yake, migomba yake na vilimo vyote tunaamini hivyo. Na kila mfanyakazi atakuwa tayari kufanya kazi kwa mujibu wa ufanisi na hatutafanya kazi tena kwa mazoea, tutafanya kwa ufanisi zaidi na ninaamini kwamba litakapotokea tatizo lolote lile ambalo litakuwa linakwaza sekta moja katika sekta hizo za maendeleo, serikali iko makini kuweza kulitatua suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaambia wawakilishi wote wa Zanzibar kwamba tupitishe hoja hii mia kwa mia ili tuweze kufika pahala nchi yetu kuinasua. Unapokuwa mwakilishi halafu ukajenga hoja ya kwamba labda serikali yako bado tu itakuwa ina vikwazo vya kuweza kutoka pale ilipo, lazima ukubali wewe mwenyewe binafsi ni serikali. Wewe mwakilishi mwenyewe ni serikali, sasa mawaziri umewapa nafasi ya kusimamia wizara ama umewapa nafasi ya kusimamia shughuli nyengine za maendeleo, basi wewe kazi yako ni kuwasukuma mawaziri ili waweze kufanya kazi inayotakiwa na wananchi.

Lakini usiwe wewe mwakilishi kikwazo cha maendeleo katika nchi hii, hao wananchi wako huko wamekuchagua wakiwa na hali ngumu, wanataka wewe uwasaidie na hapa ndio pahala pakuwasaidia, hapa sio pahala pakuanzisha wewe mgogoro na wananchi wako ukasema kwamba mimi labda maana yake nina wasi wasi, labda mimi hili jambo halitakuwa, labda maana itakuwa hivi, labda gani, yaani hiyo labda unayoitafuta wewe ni labda gani unapiga ramli? Usipige ramli Katiba na miongozo ipo wazi inakuelekeza kuwa wewe ni mtu ambaye unatakiwa kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilete maendeleo.

Leo ikiwa wewe bado unapiga ramli maana yake haitakuwa, labda itakuwa hivi, mnakuwa na waganga wa kienyeji humu, tafuteni basi pahala tuwafuate sisi, maana tuna shida mbali mbali mje mtusaidie. Lakini kama mmekuja kwa hoja ya serikali na Katiba, basi serikali iko makini kwa hoja hii na tuna Rais makini, tuna msaidizi wa Rais Mhe. Makamu wa Pili makini, tuna uwezo wa kuweza kusema hili tunalitaka, hili hatulitaki.

Mhe. Naibu Spika, nawaambia kwamba kule kwenye Baraza la Mapinduzi hayo mambo yaliyozungumzwa jana hapa, yuko Mheshimiwa mmoja hapa alizungumzia sana mambo ya mipaka, mambo ya ma-*blocks*, mambo sijui ya nini. Namwambia hivi na nawaambia na nyinyi wengine kwamba serikali yenu inalishughulikia hilo suala, ma-*blocks* yanaangaliwa, mipaka ya bahari inaangaliwa, yaani kila kitu kinaangaliwa, sio kama tunakwenda mule sisi kula korosho tu, hatwendi kula korosho, sisi tunakwenda mule kujadili maendeleo na mafanikio ya Wazanzibari. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwaambia mutoe shaka, muondoe wasiwasi serikali yenu iko makini katika hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Said Soud Said, umesema kwamba mafuta yakichimbwa akinababa wataongeza wake wanne. Mheshimiwa, kwa hilo nafikiri wanawake wengi hutowapata kupitisha mswada huu. Tunaendelea. (*Kicheko/Makofi)*

Mhe.Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukue nafasi hii kwa heshima kabisa ya kusema kwamba, nilidhani sitapata nafasi kwa muda uliobakia, kwa hiyo, mengine nilikuwa nimeandika kupeleka kwa maandishi. Lakini kwa haya niliyonayo mara nyingi unaposema mwisho inakuwa mambo mengi wenzako wameshayazungumza, lakini hata hapo sikosi neno.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wizara yangu kama alivyosema Mheshimiwa aliyekaa sasa hivi anazungumzia kabla hatujapata mafuta anaanza kututishia sisi wanawake kwamba wataowa sana na watakuwa na wengi. Mimi nasema kama Waziri wa Wanawake na Watoto aendelee kusema lakini tutajipanga vizuri, wahakikishe watakapoowa wanawake wanne tutakuwa na taratibu za kuhakikisha kwamba wote wanapata haki sawa pasipo kupungua, wanapokuhitaji wanakupata na asiwe na sababu ya kusema naumwa, aa, awe mzima saa zote. (*Makofi/Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika, akinunua zawadi zifanane, lakini pia atakapokuwa anaongeza watoto ahakikishe kwamba Bima ya afya ya mtoto inakatwa siku ile ile anayozaliwa, ile siku na saa atakapoanza kukorofishana na mama kwa sababu amepata mambo mazuri kwa mke mdogo au mkubwa, huyu mtoto tayari ameshapata kinga ya kutosha ambayo haitabughudhiwa kwenye masomo wala kwenye afya yake.

Mhe. Naibu Spika, hayo ni nyongeza ya mazungumzo ambayo wanapopanga mambo mazuri yanayohusu wanaume wajue kwamba na wanawake pia hatujalala.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kutoa pongezi kubwa sana kwa Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuweza kutoa nafasi hii ambayo bahati nzuri ikamuangukia mwanamke katika kipindi muwafaka ambacho tunajua kabisa mambo mengi yatakuwa ni mazuri, hasa kwa kuamini michango ya wanawake kwamba tunakuwa waaminifu sana tunapopewa nafasi kama hizi. Naamini kabisa kazi iliyoletwa na ndio maana mambo haya yanakwenda kwa *speed* nzuri na akinababa waendelee kutu-*support* kwa sababu wanajua kwamba chochote wanachofanya bila mama mambo hayendi.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kusema tu, bahati nzuri masuala haya ya uchimbaji wa mafuta kwetu Zanzibar yanakuja wakati tuna elimu kubwa sana kuweza kujifunza kwa wenzetu ambao mengi yaliwapata matatizo kwa sababu hawakuwa na muono mahali gani waweze kujifunza kwanza, lakini bahati nzuri ni kwamba Zanzibar tumeona mataifa mengine wamechimba mafuta, matatizo waliyokuwanayo sisi tutayazingatia.

Mfano mdogo tu ni kwamba, Nigeria walichimba mafuta na bado mafuta yanaendelea kuwepo, lakini kwa kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo hayakusimamiwa vizuri yamekuwa na wimbi kubwa sana la kuwafanya wanawake wengi kukosa ajira zilizokuwa na staha na badala yake wanakuwa ni watu wa kungoja, watu wafanye kazi halafu wao wafanye kazi ndogo ndogo zisizokuwa na msingi. Aidha, ikapelekea hata wananchi kuanza kuungua kwa moto, ajali za moto pale walipoona kwamba manufaa ya mafuta hayaendi kwao wakawa wanapasua *pipes* halafu wanachota kwa kutojua kabisa kwamba akichota moto ukiripuka utawaumiza, wengi waliteketea na wamekufa.

Mhe. Naibu Spika, pia, litakapoingia suala la mafuta tuna tumaini kabisa kwamba ajira zitaongezeka, ajira za serikali, ajira za binafsi, ajira zenye staha na ajira ambazo zitatusaidia kuhakikisha kwamba watoto wetu watakuwa na matumaini ya kuwa na ajira ambazo zitakuwa nzuri. Lakini hapo hapo nasema kabisa kwamba tunaamini kabisa kutokana na hali nzuri ya kwamba tumejifunza, waziri wetu anapata nafasi ya kwenda, watendaji wanapata nafasi ya kwenda kujifunza kwa wenzetu, ni pamoja na kuhakikisha kwamba mikataba inayofungwa na ambayo serikali naamini imezingatia, wakati watakapokwenda kuchimba katika maeneo, basi maeneo yale yawe na mikataba endelevu itakayoweza kuwasaidia wananchi, isije ikasababisha kama sasa hivi jinsi ambavyo wawekezaji katika mahoteli ya watalii waliahidi

mambo mengi sana kwa wananchi waliokuweko katika sehemu zao. Waliwaahidi kwamba wataweka barabara, skuli, hospitali, wengine wamejitahidi lakini bado wengine wanatusumbua. Kwa sababu mpaka sasa hivi kuna maeneo ambayo ahadi nyingi walizozitoa hawajaweza kuzitekeleza.

Mheshimiwa, nataka niseme tu, Wizara ya Ustawi na Ushirikishwaji ni wizara ambayo iko karibu sana na masuala yatakayokuweko ya uchimbaji wa mafuta. Kwa sababu unapozungumzia masuala ya ustawi wa jamii unazungumzia masuala ya ustawi yote na inamgusa kila mtu. Kwa hiyo, suala zima la ushirikishwaji wa watu watakaokwenda kufanyakazi sehemu hizo ni pamoja na kuwa na *cross-cutting* kwa sababu katika kila wizara itakuwa na mambo yatayowahusu kwenye masuala ya mafuta. Jambo hili naamini kwamba limezingatiwa na tumeliona kwamba linazingatiwa kutokana na hali halisi.

Mhe. Naibu Spika, utunzaji wa mazingira wakati wa maandalizi, naamini wizara imejipanga vizuri, kwamba baadae wakishachimba yale mafuta yatakayobakia mambo labda ya uharibifu wa mazingira yatachukuliwa hatua.

Pia, napenda nitoe pongezi kwa viongozi wetu wakuu Mhe Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, kusimama kidete kuhakikisha kwamba suala hili linafika mahala ambapo litaanza kufanyiwa kazi. Watu wanaingia kuja kuangalia, tunaona mashirika mengi na sasa hivi tumekuwa na *market* kubwa sana, ukisema tu tunatoka Zanzibar wanakuuliza ni kule mnakotaka kuchimba mafuta? Kumbe ukitaka kuchimba mafuta unakuwa mtu wa maana sana kama vile ambavyo tunajiona sisi waume zetu wanasema kwamba watakuwa wa maana, kumbe hata huko nje tunaonekana tutakuwa ni wa maana sana.

Vile vile, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kuunga mkono moja kwa moja baada ya juhudi za viongozi waliopita akiweko pamoja na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na viongozi wengine waliopita ambao waliona kuwa kuna ndoto hii angalau sasa hivi tutakuwa na matumaini ya kuona tunapata mafuta Zanzibar.

Kwa kuwa tutakuwa na kipato kikubwa basi yale masuala ambayo mmekuwa mkiuliza sana kwenye wizara yetu ya kusema kwamba kukiwa kuna mambo ya ujasiriamali mengi, masoko yatapatikana wapi, hayapatikani. Sasa hivi tunaona kabisa masoko mengi yatapatikana ya mahitaji mbali mbali na tutakuwa na njia bora ya kuweza kutumia vitu vyetu vya asili.

Sasa hivi kuna sabuni za kila namna zinazopatikana, niweze kuwaambia tu kwamba ndugu zangu masoko ya sabuni sasa hivi yanakwenda mpaka Marekani. Kuna ndugu zetu wanaokuja kuuliza sabuni huku na wanataka kufungua maduka ya Kizanzibari katika maeneo mbali mbali. Uingereza wanakuja kuuliza sabuni za liwa, sabuni za mkarafuu, sabuni za mchaichai, sabuni za Mkaratusi. Kwa hivyo, utaona kwamba ni maendeleo makubwa, watu wakipata pesa hao wajasiriamali hawatakosa mahali pa kupeleka bidhaa zao.

Pia, ningependa kusema tu kwamba suala hili la mafuta mara nyingi katika dunia linaonekana linakuwa na mambo mengi, usalama wa ndani na nje kwa ajili ya nchi yetu nao unaendelea kuimarishwa kuhakikisha kwamba, watu watakaokuja kwa ajili ya masuala ya mafuta wawe ni wale watu watakaoweza kuacha nchi yetu katika amani na usalama. Lakini pia kuna masuala ya ukuzaji wa vijana wetu watakapokuwa wanakuwa katika mazingira ya ukuaji wa mafuta katika machimbo ya mafuta ili kuhakikisha kwamba wanalindwa ipasavyo, wasiweze kurubuniwa kuona wanaweza kufanya *short cut* ya kuona kwamba mafuta yamefika basi wasiweze kusoma na kuona kuwa maisha yao yamekuwa bora.

Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba mkiunga mkono na tuunge mkono sote kwa pamoja ili tuweze kuona hizi baraka na neema zilizokusudiwa ambazo zimekuwa na msuguwano wa muda mrefu. Sasa hivi imefika nafasi ya kufuata njia ya kuona kwamba tunaweza kufikia mahala tuweze kuendelea na hatua zetu. Napenda kutoa shukurani na pia nipende kusema kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Baada ya kusema hayo, naomba nishukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Juma Ali Khatib (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, ahsante na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu na naomba sote tumshukuru kwa kujaalia katika historia ya nchi yetu tunaiandika tukiwa humu ndani kwamba ndio andiko la Mwenyezi Mungu, kwa sababu Mabaraza ya Wawakilishi yamepita mengi lakini kwa bahati mbaya hawakubahatika kwamba wao ndio watunge sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, pia, namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia vyema harakati za serikali na mipango yote na kuifanya nchi yetu sasa itoke hapa ilipo iende mbele. Hii ni kutokana na kwamba watu hawa wawili na sisi mawaziri tuna mashirikiano mazuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuwashukuru kwanza wataalamu wetu wa wizara hii, hawa wataalamu kwa kweli wametengeneza sera nzuri na sheria iliyopo ni nzuri lazima tuwashukuru na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Wawakilishi wenzangu wametoa hoja nyingi, nzuri, naziheshimu hoja zao, lakini sasa hivi tunatizama kwamba kuna mafuta yako mbele yetu. Sisi wawakilishi nataka kutoa rai kwamba, katika majimbo yetu tuwahamasishe wale wananchi wetu itakapokuja miundombinu, rasilimali basi tuzitunze zile rasilimali kwa sababu hu ni uchumi wetu. Uchumi huu utatunyanyua kutoka hapa tulipo tuweze kwenda sasa tuwe katika zile nchi zinazosonga mbele.

Lakini tukifurahia tu kwamba tuna rasilimali, tuna mafuta, lakini bado kama wawakilishi tuna jukumu la kuwahamasisha watu wetu katika majimbo tulinde miundombinu, tulinde rasilimali, tuwape mashirikiano wenye makampuni makubwa yatakayokuja kwa sababu ukiacha tu wale watakaokuja kuchimba mafuta Mhe. Naibu Spika, kuna makampuni mengi na wawekezaji wengi watakuja Zanzibar kuja kuwekeza.

Kwa hivyo, sasa ni wakati muwafaka vijana wetu wasome wapate elimu kwenye fani hii, wasome wapate elimu na kwenye fani nyengine. Kama unavyokumbuka Mhe. Naibu Spika, serikali hapa Zanzibar zimepita za awamu nyingi sana, lakini tunamkumbuka Rais wa Awamu ya Kwanza Mhe. Hayati Abeid Amani Karume, yeye alifanya mambo mengi mazuri, lakini kuna yale mazuri ya haraka haraka tunayaona, kwa mfano eka tatu tatu, elimu bure, majengo ya Michenzani na kadhalika.

Awamu hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kweli kafanya mambo mengi mazuri, tunakumbuka mambo ya pencheni ya wazee, amani na utulivu, maendeleo, lakini hili la mafuta ni jambo kubwa sana, lazima tumpongeze Rais wetu. Kwa sababu jambo hili lilifika mpaka kwenye Bunge Maalum la Katiba (Katiba Pendekezwa) na kwa bahati nzuri Katiba Pendekezwa imeridhia kwamba mafuta yasiwe ya Muungano; Zanzibar tuwe na mafuta yetu na Bara wawe na yao.

Kwa hivyo, nataka kuwaambia wale wawakilishi ambao kwa bahati mbaya labda hawajaisoma ile Katiba Pendekezwa, hili jambo limo ndani ya Katiba Pendekezwa. Sasa tujiandae tu Katiba Pendekezwa ikija tuipitishe kwa sababu kuna mambo mengi mazuri ya Zanzibar na kama hawajapata nafasi nawasihi na nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuisome ile katiba.

Halafu jengine mimi ninalotaka kusema ni kwamba, sasa hivi tunafurahia lakini lazima tujipange vizuri na tutoe ushirikiano wa kutosha, tunatoka mbali na

tunapotaka kwenda ni mbali. Mafuta kama alivyosema mwenzangu msemaji aliyepita Mhe. Said Soud Said, ni kwamba kuna rasilimali nyingi sana lakini hii ni neema tusije tukaifanya lana, tusije tukatumbukiza siasa kwenye mafuta, mafuta ni uchumi na uchumi ndio ngao yetu, uchumi ndio uti wetu wa mgongo. Wazanzibari tokea baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 tulikuwa tunasimama kwa zao la karafuu kwamba ndio uti wetu wa mgongo, lakini Mwenyezi Mungu mkubwa amejaalia kwamba tuna rasilimali ya gesi na mafuta. Nataka niwaambie wale waliokuwa wana wasiwasi mafuta yapo kutokana na vyanzo vya habari na vyanzo vya uchunguzi, si kitu kwamba labda kinabahatishwa isipokuwa ni kujua tu yako wapi na wapi. Lakini Wawakilishi wenzangu tusitie shaka haya mambo yapo, jambo ninalotaka kuwasihi tushirikiane tupitishe sheria hii ili lengo la serikali liweze kufikia.

Siku zote Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya Wazanzibari na wananchi. Kama wasemaji waliopita walivyosema ni kweli tukichimba mafuta huduma za afya zitakaa sawa, elimu itakaa sawa, barabara itakaa sawa, hata mishahara ya wafanyakazi itakaa sawa, ile pencheni ya wazee itaongezeka. Haya ndio malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, sasa hivi mimi nawasihi na nawaomba kwa heshima kubwa Waheshimiwa Wawakilishi, kwa kauli moja basi tuipitishe sheria hii ili iweze kuleta malengo yetu. Tulikuwa tukisikia tu hapo mwanzo kwamba mafuta na gesi tunayo, lakini tukumbuke Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere zamani alikuwa anasema kwamba, Tanzania kuna madini, halafu baadae akasema uchumi tunao tunaukalia, lakini muda ulipofika basi tumeona wenzetu wanachimba kule almasi, dhahabu, *Tanzanite*, *Sapphire* na kadhalika.

Sasa na sisi hebu tutoke hapa tulipo tusiweke ugumu, tusifanye misuguano misuguano, hili jambo ni letu, hii ni neema halafu sio neema tu ni jambo la historia, ni jambo la kujivunia, ni fahari yetu hii sisi Wazanzibari, tushirikiane sote kwa pamoja kwa furaha kabisa. Naamini tukipitisha sheria hii Mhe. Rais, naye ataisaini itakuwa sheria, kisha kazi ianze.

Mhe. Naibu Spika, wataalamu wetu wamefanya kazi hii kwa muda mrefu, wametembea nchi nyingi, wamejifunza mambo mengi na mimi nataka niwaambie hawa wataalamu mimi nimewasoma mmoja baada ya mmoja ni wazalendo, wanafanya hii kazi kwa uzalendo mkubwa kabisa, si watu wenye kujali maslahi. Kwa hivyo, na sisi tukikaa sasa Washwahili wanasema 'kwanza ujisifu mwenyewe, yaani ukisifu chako', kama sisi hatukuwasifu hawa na kuwapa moyo, lazima tuwape moyo, nguvu na ujasiri ili uzalendo wao

uendelee, sisi wengine tumo humu ni wanasiasa, wasomi na wataalamu mbali mbali, lakini sasa wao taaluma yao ni hii.

Kwa hiyo, changamoto zipo lakini tusiziogope kwa sababu ukitaka kulima hujui lile shamba kama utalima utapata eka ngapi za yale mazao utakuwa na makisio tu, hata ukitaka kujenga. Lakini sisi tukianza kuchimba mafuta, changamoto zitakazojitokeza kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa pamoja sote tutapambana nazo na kila kitu kitakaa sawa, hakuna jambo ambalo litatushinda.

Mhe. Naibu Spika, kuna wenzangu wengine walilalamika kuhusu mambo ya jiografia. Nchi yetu jiografia inajulikana, visiwa vyetu vinajulikana Unguja na Pemba, mipaka inajulikana na ramani zipo. Kwa hivyo, hili jambo lisitutie hofu wala lisituvunje moyo na Muungano wetu sisi hatuwezi kuja kuuvunja kwa sababu eti tunagombania *block* moja ya mafuta. Muungano wetu una viongozi wenye akili, wenye busara, watakaa pamoja wahusika kama kuna *block* kidogo imeingia Pemba, imetoka Tanga, hili jambo lisitutie wasiwasi, jambo hili wataalamu wapo makini, ramani zipo na kila kitu kipo na tusichukue yale maneno ya vichochoroni au ya pembeni. Serikali siku zote inakuwa na mipango madhubuti na mipango sahihi kuhakikisha kwamba wananchi hawapati tabu, ndio kazi ya serikali na ndio kazi ya Rais.

Kwa hiyo, nimefurahi tumezungumza mengi mazuri na tumeonesha zile hisia zetu kwa uchungu kwamba, tunahisi kuwa *block* hili liko huku lakini tunahisi tunaambiwa sio letu. Mimi nasema tusiwe na hofu, hii serikali hailali tena usiku na mchana watu wanafanya kazi, ni kukaa kama wawakilishi.

Kwanza mujitambue nyinyi ndio serikali yenyewe, usije hapa mtu ukaona unataka kumkomoa Waziri fulani, wewe ndio serikali na uko hapa kwa sababu unatunga Sheria za serikali hii. Kwa hivyo, ni vizuri kwanza sisi tukajitambua, sisi tumekuja humu, sisi ni nani na humu ndani tunafanya nini?

Sitaki kumlaumu mtu lakini kama binaadamu kila mtu ana mapungufu, mimi niko hapa na ninayo mapungufu yangu sio kwamba ninafanya kila kitu kizuri. Lakini sisi kwa pamoja tukisaidiana tukikumbisha wajibu wetu lengo letu la serikali litafikiwa Mhe. Naibu Spika.

Tusiona kwamba labda waziri fulani hichi kitu kaleta, mimi nataka nimkomoe, mimi nataka nimsuguwe, tuwe wazalendo tuonesha uchungu wa nchi yetu, kama kuna kitu kimekosekena na kina mapungufu, wewe kama Mwakilishi usingoje ukaja hapa kwenye Baraza la Wawakilishi unakwenda kwa waziri

husika, unakwenda kwa Katibu Mkuu husika, unakwenda kumwambia moja, mbili, tatu, anakusikiliza. Kwa sababu hii ni serikali yetu sote, tunataka kwamba tushikane mikono na tusibaguane kusema kwamba Mpinzani ni Mpinzani tu, si maneno mzuri. (*Makofi*)

Yako maneno Mhe. Naibu Spika, yanasemwa kwamba 'Mpinzani ni Mpinzani tu', yanatuuma, inawezekana sisi tunaumwa na nchi zaidi kuliko wewe unaejiona kwamba labda uko huko. Ifikie wakati tuaminiane kama sisi serikali imetutambia Mhe. Rais, ametutambua, tumekula kiapo tumekamata *Quran* tukufu, sisi haturudi nyuma, ni kweli ukitafunwa na nyoka unatakiwa uwe makini, lakini sisi sio wale. Ifike wakati sote kwa pamoja tuna safiana nia kutaka kuongoza nchi yetu iende itoke hapa tulipo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, kwa pamoja tushirikiane tupitishe sheria hii, tupitishe mswada huu ili nchi yetu iweze kufikia yale malengo iliyokusudia. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi niungane na wenzangu waliokwisha kutangulia katika kuiunga mkono hoja na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo katika Baraza letu tukufu na kutujaalia na kutuwezesha kufanya shughuli zetu kama ambayo tumezipanga kuzifanya. Mwenyezi Mungu atuwezeshe azidi kutupa kheria na baraka katika nchi yetu.

Aidha, niwashukuru sana viongozi wetu wakuu hususan Mhe. Rais wetu Mhe. Dkt Ali Mohd Shein, kwa kazi kubwa na jitihada kubwa aliyoifanya katika kuhakikisha kwamba sheria hii inafikia ukingoni na kuja hapa Barazani.

Lakini vile vile naomba nimpongeze sana Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano Dkt Jakaya Mrisho Kikwete kwa mashirikiano makubwa na Rais wetu ili kuhakikisha tunapa shughuli hii. Lakini pongezi maalum ziende kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Magufuli kwa baraka zake na msimamo wake wa kutaka Zanzibar iweze kuchimba Mafuta na Gesi kwa sheria yake. Tunamshukuru sana na tunamuunga mkono kwa msimamo huo.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, jambo hili lina historia kubwa katika nchi yetu, limeanza kwa muda mrefu tokea mwishoni mwa miaka ya 50 Zanzibar ilianza jitihada za kutafuta mafuta, wakati huo kampuni ya *BP Shell (British Petroleum)* ilianza hatua za awali katika kutafuta mafuta, na wakati huo kilichogundulikana ni kwamba mafuta yapo lakini hayatoshelezi kibiashara na ikaja hoja kwamba inategemea baada ya miaka 50 mbele ndio kuna tamaa kubwa ya kwamba mafuta kwa Zanzibar yangeweza kuwepo ya kutosha yanayoweza kujiendesha kibiashara.

Kwa hiyo, tokea enzi ya Ukoloni baada ya Mapinduzi tumekuwa katika jitihada hizi na tumepita katika hatua mbali mbali mpaka leo tumefikia tunaelekea sasa kuweza kuchimba mafuta na gesi na inafikia katika hatima nzuri hatima ambayo Wazanzibari sote tulipenda kwamba rasilimali hii iweze kufanywa na Wazanzibari wenyewe na tuweze kupata matapo yanayotokana na rasilimali hii na hilo *Alhamdulillah* tumshukuru Mwenyezi Mungu sasa linaelekea vizuri.

Kwa hiyo, leo ni siku ya historia kubwa sana kwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuwa tayari kutaka kupitisha jambo kubwa lenye historia refu, lakini ni jambo ambalo linaloweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na maendeleo katika nchi yetu.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, ni vizuri Wajumbe wako hawa wakawekwa katika kumbukumbu maalum kwa kipindi hichi kikubwa cha kimaendeleo katika nchi yetu. Nimeisikiliza kwa makini sana michango ya Wajumbe wetu ambayo yote ina muelekeo wa kujenga na kuimarisha sheria hii. Takribani wote ambao wametoa michango yao wameonesha wazi namna ya imani ya sheria hii na wanavyotaka sheria hii ifanye kazi na ifanye kazi katika mazingira mazuri zaidi. Maelezo yao yanaendana kabisa na nia na dhamira ya serikali katika sheria hii na ndio maana sheria hii ni moja katika sheria iliyochukuwa muda mrefu sana katika kutayaishwa kwake mpaka kufikia hapa leo katika Baraza lako tukufu.

Serikali kupitia watendaji wake mbali mbali katika ngazi tafauti imechukuwa jitihada kubwa sana kutaka kujifunza kwa hali ya juu ili kuona tuna sheria inayosheheni uwezo mkubwa wa kutuelekeza tuweze kupata rasilimali yetu hii tuipate kwa salama na iwe na tija kwa nchi yetu. Kwa hivyo, kazi hiyo imefanyika sana wataalamu wetu na watendaji wamekwenda nchi mbali mbali kujifunza tumechukuwa mifano ya nchi mbali mbali na mara nyingi jambo hili limezungumzwa katika serikali na kila pale ambapo imeonekana bado pana kasoro serikali ilikuwa inairudisha kwa watendaji ili walifanyie kazi vizuri.

Naamini kazi ya biaadamu kwa njia moja ama nyengine haikosi kasoro, lakini kwa kiwango kikubwa sana sheria hii inakidhi haja ya mahitaji ya leo na mahitaji ya miaka mingi ijayo. Kwa hiyo, ushauri mwingi ambao Wajumbe wameutoa naamini kabisa Waziri muhisika ameusikia na yale mambo ya msingi yanayohitaji kufanyiwa marekebisho nahakika waziri atayaeleza, lakini kwa kiasi kikubwa sheria hii imekidhi haja na yale mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe, mmekuwa mkieleza hapa tayari sheria hii imeweka utaratibu mzuri wa kuyatafakari na kukidhi matakwa yenu.

Moja katika eneo ambalo limezungumzwa sana ni suala la kuimarisha mapato yetu, suala la kuimairisha uchumi wetu na kwamba rasilimali hii iwe rasilimali ya taifa ili itufae sote. Hilo hasa mlilolizungumza ndio ilikuwa lengo kuu la sheria hii. Kwa hiyo, sheria hii imewekwa kujali maslahi ya taifa na si kujali tu kwa vizazi vya leo lakini na kwa vizazi vijavyo. Maana kuna mfuko maalum wa mafuta utaanzishwa ndani ya sheria hii kwa msingi wa kwamba kile knachopatikana kwenye mafuta hakitotumika kwa wakati wa leo peke yake bali kitaweka kitumike leo kitufae sisi tuliopo kiwafae vizazi vyetu vinavyokuja na kwa miaka mingi mbele ijayo.

Kwa hiyo, sheria hii imejikita katika maelezo mengi ambayo mmeyalenga kwa maslahi ya nchi yetu. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa yale yote ambayo mliokuwa mna wasi wasi nayo katika eneo hili muondoe wasi wasi kwa sababu sheria yenyewe imejieleza vizuri katika eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, Suala la kimazingira. Sheria hii imeliona limeitafakari, imeweka misingi mizuri ya kuhifadhi mazingira yetu katika eneo hili la mafuta. Ni kweli nchi nyingi duniani zimeathirika ambazo zinachimba mafuta kwenye suala la mazingira, na sie kwa njia moja au nyengine athari zitajitokeza, lakini kutokana na sheria yenyewe kwa kiasi kikubwa tutaweza kupunguza au kuondosha athari zenyewe za kimazingira. Tumefanya tafiti mbali mbali kuona namna gani tunaweza kupunguza athari hiyo. Naamini sana katika eneo hilo tutaweza kufanya vizuri kutokana na muelekezo wa sheria yenyewe.

Lakini vile vile tumezungumzia sana suala la amani ya nchi na rasilimali hii. Ni kweli zipo nchi zimeathirika kwa kuwa na rasilimali hii. Mfano ni Sudani ya Kusini licha ya kuwa na rasilimali kubwa ya mafutaM lakini ina matatizo mengi ya ugomvi wa ndani na vita vya wenyewe kwa wenyewe vikichangiwa zaidi na rasilimali hii. Lakini bahati nzuri kwa upande wetu wa Zanzibar kutokana na umakini wake ilichukuwa kila hatua kuhakikisha jambo hili kwetu tuepukane nalo. Naamini kabisa muelekeo huu wa sheria yetu na utaratibu wake utatuepusha sana na mazonge hayo.

Kwetu tujitahidi kuiunga mkono sheria hii ili utusaidieM maana kila ambalo limezungumzwa na Wajumbe hapa kwa kiasi kikubwa kama mtaipitia hii sheria mtaona lina majibu yake. Kwenye masuala ya ajira, sheria hii imetoa mwanga mzuri kwa ajira kwa wananchi wetu na serikali yetu imechukuwa hatua kubwa kuanza kuwasomesha vijana katika eneo hili na wakati huo huo kuwahamasisha Wazanzibari wengine wenye uwezo kuwasaidia watoto wao ili wasomee maeneo haya kwa msingi ya kuweza kuhimili vyema rasilimali hii pale tutakapoanza na huu ni mwanzo tu wa kupitisha sheria, baada ya hapo kuna kazi kubwa yenye ushindani mkubwa yenye ushindani mkubwa ya kupata makampuni makubwa yenye uwezo mkubwa katika eneo hili katika kuyachimba mafuta yenyewe.

Kwa hivyo, kwa moyo huu ambao Wajumbe wameuonesha na taaluma ambayo wananchi wetu wameipata kutoka kwenu tutapa mashirikiano makubwa kwa wananchi wote ili tutakapoanza kazi ya kutafuta mafuta yale makampuni yakatakayokuja hapa yatapata matayarisho mazuri tutashirikiana nayo ili tuweze kuyachimba kwa utaratibu ulio bora zaidi rasilimali hii itunifaishe sote.

Naamini sana kwamba kwa jitihada zilizofanywa na hatua zilizofikia tutaweza kuvuka kila mtihani unaohusiana na jambo hili na bado nafasi ipo pale tutakapoanza zoezi zima, tukakumbana na vikwazo mbali mbali basi nafasi ipo ya kurudia na kufanya marekebisho yatakayoonekana yanafaa.

Kwa hivyo, yale mawazo ambayo Wajumbe wametoa yako sasa yatakuwa ni wakati muafaka, yako ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Naamini mawazo yote ni ya msingi na yote yatatiliwa maanani.

Lilizungumzwa jambo linalohusu sekta yetu ya utalii, ni kweli sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa ni sekta muhimu sana kwa Zanzibar. Nataka niwatoe ghofu Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wa Zanzibar kwamba, bado tutaendelea na sekta yetu ya utalii na kama kadri tutakapopata uwezo wa rasilimali hii ya mafuta ambayo mapato yake ni makubwa tutazidi kujenga nguvu ya sekta ya utalii. Na wapo wenzetu tuliojifunza kwao kwa mfano Dubai, Abudhabi na kwengine tumeona wanachimba mafuta shughuli za mafuta zinaendelea na wakati huo huo shughuli za utalii zinakuwa kwa haraka sana.

Kwa hiyo, napenda kabisa tuelewe tusiwe na wasi wasi wa aina yoyote katika kuhakikisha kwamba sekta yetu ya utalii itaendelezwa na sekta yetu ya mafuta tuiendeleze kwa msingi wa kuleta tija. Imejitokeza jambo hapa kuhusu suala la Vitalu, sheria iko wazi kabisa imeeleza vizuri kwamba kutakuwa na nafasi ya

kikanuni ya kugawa Vitalu upya. Kwa msingi huo tunapoipitisha sheria hii yale yote ambayo umeona mapungufu ndio yatakuja yarekebishwe na sheiria.

Mhe. Naibu Spika, Suala la ushindani ulio sawa ndani ya sheria hii pia limezungumza vizuri. Mimi naamini kabisa kabisa sheria hii imekidhi haja, imekidhi malengo, imetizama maslahi ya Wanzibari na yote yale Waheshimiwa mliyoyasema ndani ya sheria hii yamo. Kwa hivyo, niwaombe wenzangu sote kwa pamoja tuinge mkono sheria hii ili itufae sisi na vizazi vinavyokuja.

Baada ya maelezo haya Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono sheria hii na nawaomba wenzangu wote wajitokeze kuunga mkono. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Lakini pili niwapongeze sana viongozi wetu wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulipatia ufumbuzi suala la Mafuta na Gesi asilia.

Suala hili Mhe. Naibu Spika, ni suala ambalo lilikuwa lipo na la muda mrefu sana na tulikuwa tunaliona ni changamoto kubwa, nalikumbuka lilijadiliwa sana katika vikao vya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini kwa hekima za viongozi wetu suala hili sasa limepata ufumbuzi na tuko katika hatua nzuri sana na muhimu ya kutayarisha sheria kwa upande wa Zanzibar inayohusu masuala ya Mafuta na Gesi asilia.

Nichukuwe nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuwasikisha mswada huu. Lakini vile vile nichukuwe nafasi hii kuwashukuru kamati iliyoandaa Mswada wa Sheria hii. Mhe. Naibu Spika, kamati ile ni kamati ya wazalendo wafanyakazi wetu wa ndani ambao kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana ya kuandaa mswada wa sheria hii. Kazi waliyoifanya ni kubwa walifanya *references* mbali mbali na wamekuja na kitu ambacho kwa kweli sote tunahisi kabisa kwamba kimekidhi haja na matakwa ya nchi yetu katika suala hili. (*Makofi*)

Lakini pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe, waliochangia kabla yangu kwa michango yao mizuri ambayo imejikita zaidi katika kujenga na kuimairisha zaidi mswada wa sheria hii na ni imani yangu kwamba sote kabisa kwa umoja wetu tutaipitisha sheria hii ili suala la mafuta na gesi liwe na sheria yake kwa hapa nchini petu na tuanze kazi nyengine zitakazoruhusu utoaji wa

leseni na kazi nyengine za utafutaji na huko mbele tena uchimbaji na shughuli nyengine zote zilizoelezwa katika ile *upstream*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nizungumze katika maeneo mawili ambayo katika mjadala wa jana niliyasikia yakizungumzwa na baadhi ya Wajumbe. Eneo la kwanza ambalo nilitaka nilichangie Mhe. Naibu Spika, ni hili suala la mapato yanayotokana na mafuta na gesi asilia. Nieleze kwamba Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(Petroleum Act)* ya mwaka 2015, Kifungu cha 4 (1) hadi (3), kimelitoa sasa suala zima la mafuta kutoka iliyokuwa suala la Muungano na kulifanya kwamba mamlaka yake yasimamiwe na Zanzibar yenyewe.

Lakini vile vile katika kutoa fursa hiyo ukiangalia pia Sheria ya Mapato ya Mafuta na Gesi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kifungu cha 2(2), nacho kimeeleza wazi kwamba suala la mapato yanayotokana na mafuta kwa upande wa Zanzibar yatasimamiwa na Baraza la Mapinduzi kwa upande wa Zanzibar. Kwa hivyo, Zanzibar litashughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na yale maeneo na yanahusu upatikanaji wa mapato kwa Jamhuri ya Muungano yataendelea kusimamiwa na Sheria iliyotungwa na wenzetu ambayo ni Sheria ya Mapato ya Mafuta na Gesi ya 2015.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu wakati hivi sasa tupo katika hatua muhimu sana ya kupitisha sheria hii, Serikali tayari imeanza mazingatio ya kuandaa sheria yake itakayohusu mapato kwa upande wa Zanzibar, ambayo mapato yatakayotokana na mafuta na gesi asilia. Suala hilo lipo kwenye maandalizi na katika sheria hiyo ambayo ninaamini haitochukua muda, itaelezea kwa kina hali nzima ya usimamizi wa mapato yanayotokana na mafuta na gesi asilia kwa upande wa Zanzibar.

Lakini vile vile yataweka kwa uwazi kabisa, yaani yatabainisha kwa uwazi kabisa vyanzo vya mapato vitakavyotokana na mafuta na gesi asilia kwa upande wetu, ikiwemo masuala ya *dividend* ambayo yalizungumzwa hapa, masuala ya faida kwa maana ya faida *profit share* ambayo yatatokana na mafuta hayo, kodi mbali mbali zitakazotokana na mafuta, masuala ya mapato yatakayotokana na leseni zitakazotolewa kwa upande wetu.

Vile vile, kutakuwa na mfuko maalum ambao utawekwa fedha hizi. Hilo ni suala ambalo tutalizingatia wakati wa matayarisho ya sheria hii. Lakini kubwa ambalo itabidi lazima tuliweke utaratibu ni jinsi gani fedha zitakazotokana na vyanzo vya mafuta na gesi asilia zitakavyoweza kudhibitiwa, ili visije vikaleta athari kwenye uchumi wa nchi yetu. Kila uchumi una uwezo wake wa *up solve*.

Tuna *capacity* ya ku-*up solve* fedha. Kwa hivyo, hiyo *fund* itakayowekwa itaandaa utaratibu huo mzuri ambapo kuhakikisha kwamba fedha hizi zitakuwa na manufaa kwa wananchi kizazi hichi cha leo na kizazi kitakachofuata.

Lakini kuna suala zima Mhe. Naibu Spika, kwenye suala zima la mapato juu ya uwezo wetu, kwa maana ya *capacity* ya wataalamu wetu katika kuainisha na kubaisha vyanzo vya mapato hayo. Lakini vile vile *capacity* itabidi tuijenge na tunaendelea kuijenga kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais kwamba, suala hili sasa hivi Serikali imeshaanza kusomesha vijana wetu katika maeneo haya. Hivyo, ni suala ambalo litaendelea kupewa kipaumbele kuona kwamba taaluma inajengwa, siyo tu katika masuala ya uchimbaji na utafutaji wa mafuta, lakini vile vile katika kuibua vyanzo vya mapato, lakini na katika usimamizi wa suala zima la mapato yanayotokana na mafuta na gesi asilia.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ningeomba Waheshimiwa Wajumbe, wasiwe na wasi wasi kwa sababu taratibu zipo zinaandaliwa na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakuja na sheria hiyo inayohusiana na mapato yanayotokana na mafuta na gesi asilia.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili nililotaka kulizungumza kwa kifupi kabisa ni suala la mipaka ambalo jana pia lilizungumzwa. Kwa hili Mhe. Naibu Spika, ninataka niseme tu kwamba sheria zetu zote hizi tunazozitunga, iwe ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii ambayo tunaitunga kwa upande wa Zanzibar, msingi wake mkuu ni ule mkataba wa Kimataifa wa Sheria za Bahari *(United Nations Convention on the Law of the Sea).* Ndiyo pale ambapo tunapata uhalali hasa katika lile eneo la kina refu (*EZY*). Na mkataba huu ulipitishwa mwaka 1982, lakini Tanzania iliridhia mkataba huu mwaka 1989 kwa kupitisha Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone.*

Sheria hii iliporidhiwa Tanzania na kwa sababu *United Nations Convention on the Law of the Sea* imetoa mamlaka hasa katika eneo la bahari kuu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana ya *Sovereign State*. Ndiyo eneo hili limetolewa na ndani tukaridhia kwa sheria hii ambayo sasa tunapata uhalali kutokana na mipango yetu ya ndani ya kuwa na sheria mbili zinazotawala masuala ya mafuta na gesi asilia; Moja kwa upande wa Jamhuri na nyengine kwa upande wa Zanzibar.

Sasa kumsingi Mhe. Naibu Spika, *Convention* imeweka utaratibu mzima wa mipaka, imeelezwa wazi jinsi ya vigezo vinavyofuatwa katika kuweka mipaka. Katika hili sasa tunahesabu tuna mipaka ya ndani ambayo itabidi ni sisi

wenyewe ndani kuielewa na mipaka hiyo lazima itatokana na Katiba zetu. Ukiangalia Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 1 inaelezea wazi wazi na naomba ni-*quote* kwenye eneo hilo, kwamba:-

Ibara ya 1; "Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa Vidogo vinavyozunguka na bahari na eneo la bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar".

Kwa hivyo, kimsingi mipaka ipo, inajulikana, lakini vile vile utaratibu wa kuweka mipaka baina ya Tanzania kwa maana ya *Sovereign State* yenye kumiliki eneo la *EZY* na zile nchi jirani. Mfano Msumbiji, Kenya, Seychelles utaratibu huo upo. Tunapozungumzia kwamba *two hundred nautical for miles*, kama *two hundred nautical for miles* zile zita-*overlap* na *two hundred nautical for miles* za nchi nyengine, utaratibu umewekwa wazi wa *Equidistance line* baina ya mipaka ya nchi mbili hizi. Sasa hilo naomba lisiwe kizuwizi, tusikwame kwa sababu ya suala la mipaka kupitisha sheria hii. Ni suala ambalo lipo na ile mipaka inayohusu nchi jirani utatuzi wake utatuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Lakini kwa mipaka yetu ya ndani utaratibu upo na ninashukuru sana Afisi za Wanasheria Wakuu, kwa maana ya Wanasheria Wakuu wenyewe kwa upande wa Zanzibar lakini vile vile kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameshalifanyia kazi suala hili kwa muda mrefu sana na wameshafikia maafikiano kwenye suala la mipaka na ninadhani kama wanaendelea, wanaendelea katika suala la kumalizia tu, lakini utaratibu upo na wao pia walilifanya hili kwa kuzingatia Katiba zetu ambapo Kifungu cha Katiba ya Zanzibar nimekisema, lakini vile vile wanaangalia mikataba ya Kimataifa ikiwemo *UNCLOS* ambayo imeweka utaratibu madhubuti kabisa wa jinsi ya kuweka mipaka ile.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa *spirit* ile ile ambayo imeoneshwa na michango ya Wajumbe mbali mbali hapa basi tumsaidie Mhe. Waziri, kwa kupitisha sheria hii, lakini kwa kupitisha sheria hii tutakuwa tumejisaidia sisi wenyewe lakini vile vile tumesaidia vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Naibu Spika, na kwa hilo sina wasi wasi muda utakapowadia basi kwa umoja wetu tutalipitisha hili na tujenge historia mpya katika yetu ya kwamba Baraza hili, ndilo Baraza ambalo limetunga sheria ya mwanzo kabisa Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri, kwa asilimia mia.Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa muda wetu tulionao tumebakiwa na nusu saa na kwa kuwa bado tuna wachangiaji wawili ambaye atakuwa ni Mwanasheria Mkuu pamoja na Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Kwa sababu jioni tunataka tuje tumalizane na Mswada huu na Waziri atamalizia kujibu hoja katika kipindi cha jioni.

Hivyo basi ningemuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, atengue kifungu cha Kanuni ili tupate kuongeza muda kidogo kwa kumaliza na Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli zilizo mbele yetu bado zinamuhitaji Mhe.Mwanasheria Mkuu na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, waweze michango yao na kwa kuwa muda uliobaki ni mdogo kwa kutoa nafasi kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Hivyo, niliombe Baraza lako Tukufu liweke Kanuni ya Muda Kando ili tuwe na nafasi ya kusikiliza michango ya Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, ili baadae jioni Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, apate nafasi ya kufanya majumuisho.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya kuweka Kanuni kando ili Baraza lako liendelee baada ya muda uliopangwa.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Nikushukuru sana Mhe. Waziri. Sasa niwaulize Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

Sasa nimkaribishe Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kunipa fursa angalau kusema machache kwenye hoja hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ambayo ni hoja muhimu na ambayo tulikuwa tukiisubiri muda mrefu.

Kama ambavyo wengi Mhe. Naibu Spika, wamezungumza suala hili lilikuwa limezungumzwa muda mrefu na lilikuwa ni mtaji wa watu wengi na kila mtu alikuwa analizungumza kwa namna ambavyo anaona yeye inafaa. Kuna wengine Mhe. Naibu Spika, walilizungumzia jambo hili kwa kutaka umaarufu tu, walikuwa wanasikia kama kuna suala la gesi na mafuta. Kwa hivyo na wao wakawa wanalizungumzia siyo kwa kulijua lakini kwa kutaka umaarufu kama na wao wawe miongoni mwa watu ambao walikuwa wanalizungumzia jambo hili. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna wengine wamelizungumzia jambo hili kisiasa ili kwenye mikutano na viriri vya kisiasa inoge, basi ilikuwa lazima wazungumzie suala la gesi na mafuta. Bila ya kuzungumzia suala hilo basi mkutano ule unakuwa haunogi, unakuwa hujazungumzia jambo. Lakini wengine Mhe. Naibu Spika, walitaka kulizungumzia jambo hili kugombanisha ndugu waliokuwepo wa muda mrefu wagombane kwa sababu ya jambo hili tu. Lakini kama haitoshi wengine wakasema ndugu ukiwagombanisha watapatana tu, hawa tuwatenganishe ndiyo ilivyokuwa likizungumzwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wote hao walikuwa wakizungumza nje ya maeneo ambayo hawakuwa na mamlaka nayo. Lakini mwenye dhamira ya kweli ya kulimaliza jambo hili tumemjua ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana kwenye mwezi wa Julai mimi nilikuwa Uholanzi na Katibu Kiongozi alinipigia simu kunipa maagizo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuniambia kwamba wao Marais; yaani yeye na Rais Mstaafu, Rais Jakaya Mrisho Kikwete wameamua kuliondoa mikononi mwetu, maana ilikuwa tunalichelewesha. Kila siku hatwishi visingizio. Wakaamua kuliondoa mikononi mwetu na kuliamua wao na agizo lililotoka ni kila mtu amuagize Mwanasheria wake Mkuu alimalize suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, na mimi jawabu la haraka haraka kwa sababu nilikuwa nje ya nchi nikasema nimepokea wazo ni zuri, nitawasiliana na Mhe. George Mcheche Masaju nitakaporudi. Jawabu la *Chief Secretary* akasema Mhe. Rais anasema hili halitaki usubiri urudi, hili linataka huko huko uliko uanze kulishughulikia. Sasa hii inaonesha jinsi gani Mhe. Rais alilidhamiria jambo hili kumaliza na siyo tu kumaliza yeye, lakini alisema ulete mapendekezo yako na tuyajadili kwenye vikao vya Baraza la Mapinduzi. Sasa waliokuwepo wakongwe watathibitisha hayo kama ni kweli suala hili lilijadiliwa ndani ya vikao vya Baraza la Mapinduzi na viliitwa vikao vya dharura. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe, halikuwa jambo rahisi. Hata sisi tulikuwa wabishi kwenye baadhi ya maeneo. Hatukukubali tu kuambiwa fanyeni hili na mulitekeleze kama lilivyo. Lakini baadae Mhe. Naibu Spika, tukaja kukubaliana kama ili jambo hili lifanyike, basi kuna mambo ambayo sisi kama Zanzibar tunahitaji kupewa *assurance* na wenzetu kama haya watayasimamia. Sasa kwa wale ambao wamepata fursa ya kusoma ile Sheria ya Gesi na Mafuta ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka jana, maeneo matatu ambayo yametambuliwa ndani ya sheria ile.

Moja ni eneo la kila upande kushughulikia masuala ya mafuta na gesi. Tanzania Bara itashughulikia upande wake lakini Zanzibar pia imepewa fursa kupitia sheria ile kusimamia pia maeneo yake. Na sheria imesema siyo tu kusimamia maeneo hayo lakini hata mapato yanayotokana na mafuta na gesi asilia basi yatasimamiwa na sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Hiyo ni kuhakikisha jinsi gani kwa kadri ya wetu tumejitahidi kuhakikisha kama mambo haya yanafanyika kwa utaratibu mzuri. Wenzetu wakakubaliana na sisi, kama kuna maeneo ya Tanzania Bara, kuna maeneo ya Tanzania Zanzibar, lakini kuna maeneo ambayo tutashirikiana. Huwezi ukafanya biashara hii usishirikiane na mwenzio, lazima mutashirikiana tu Mhe. Naibu Spika.

Sasa kwenye maeneo ambayo tutashirikiana nayo pia yametajwa. Lakini pia ukisoma sheria hiyo Mhe. Naibu Spika, imeeleza pia mapato ambayo yatatokana kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wao wenzetu waliwahi na tayari wameshatengeneza sheria. Kama yale mapato yote ambayo yatatokana na mafuta na gesi asilia wameshauwekea utaratibu wao wa kisheria. Lakini sisi tumesema tulete hii kwanza. Lakini na sheria hiyo pia ifuatie baada ya sheria hii ili sasa tuweke utaratibu mzuri wa kudhibiti mapato yanayotokana na mafuta na gesi asilia.

Kwa hivyo, utaratibu wa kisheria Mhe. Naibu Spika, tofauti na watu wachache ambao wanataka kupotosha na kusema kwamba hakuna utaratibu wa kisheria, mimi ninadhani tusiwasikilize. Hakuna Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotungwa na kutoa mamlaka ya Kimuungano kwa pande zote mbili kama hii. Mara zote tumekuwa tukilalamika humu, zinatungwa sheria lakini huoni *component* ya Zanzibar ndani ya sheria ile. Lakini leo imetungwa sheria ambayo imefungua kwa uwazi kabisa mamlaka ya sehemu zote mbili za Jamhuri. Ati tunakaa humu ndani tuna-*question*, tunaulizana kwamba je, hilo jambo ni la kihalali. Haiwezekani Mhe. Naibu Spika, tufike pahala tuanze

kuulizana mambo ambayo tayari tumeshapewa majibu yake. Siku zote tunalalamika humu, kwamba sheria zinatungwa haimtaji waziri, haimtaji sijui nani, haisemi kitu kwenye Zanzibar. Leo imetungwa sheria ambayo kimewekwa kila kitu kwa uwazi, lakini bado kuna baadhi yetu wanajenga hofu na dhana kwamba sheria hii bado haitusaidii.

Sasa tuwasaidie Mhe. Naibu Spika, kwa kuipitisha sheria hii kwa asilimia mia moja. Tena hii naomba nimuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, itakapopitishwa sheria hii naomba ukamshauri Mhe. Rais, hii atakapoitia saini asiitie kama anavyozitia zile sheria nyengine. Lazima awaalike baadhi ya wajumbe humu ndani kwenda kushuhudia sheria hii inavyotiwa saini, kwa sababu tulikuwa tunaisubiri kwa muda mrefu na ndivyo ambavyo alivyofanya pia Rais mstaafu Mhe. Kikwete, kwamba aliionesha dunia kwamba sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ime-*mature*, kwamba inaweza kushughulikia mambo haya bila ya watu kugombana, na kila upande kutoa fursa kuweza kusimamia eneo lake.*(Makofi)*

Kwa hivyo, suala hili Mhe. Makamu wa Pili nikuombe sana utakapomuona Mhe. Rais, atakapokuwa tayari kuitia saini hii, basi Wajumbe wa Baraza lake la Mapinduzi wawepo, wajumbe wa kamati wawepo na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili pia wahudhurie, ili sasa *media* yetu ione kama sasa Zanzibar iko tayari kuingia katika biashara hii ya mafuta na gesi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kusubiri, dunia haitusubiri. Ukisema ukae ikusubiri wewe Zanzibar hujawa tayari, dunia inakimbia. Leo wenzetu wa Mozambique tayari wameshaanza kupiga hatua katika kuchimba mafuta, wenzetu wa Comoro wameshapiga hatua katika kuchimba mafuta. Sasa sisi tukae tusubiri tuseme hapana, acha hao waendelee sisi tusubiri hatujawa tayari, dunia haitusubiri na hakuna mwekezaji atakayeacha yake aje akusubiri wewe, kwani anataka kitu gani, si atakipata huko Uganda kama wewe unasubiri. Sasa huu ndio huo ufunguo wa sisi kuwaalika sasa waje, kuwaambia kwamba na sisi tuko tayari kushirikiana na wenzetu katika kuchimba na kutafuta mafuta.

Kwa hivyo, tusiwe na hofu kabisa, sheria hii kwa kiasi kikubwa na kwa kadiri ambavyo tumeweza, maana tumejaribu na kupitia sheria za nchi mbali mbali. Kuna maeneo ya vifungu Mhe. Naibu Spika, ni *standard*, tutakaposoma sheria za mafuta zote utazikuta hazibadiliki *local content*, jinsi ya kufanya mfuko wa maendeleo ya mafuta, kuwa na kampuni. Hivi ni vifungu ambavyo ni *standard* kwenye sheria zote za mafuta na utazikuta tu, kinachofanyika ni kuweka ukarabati wa kila nchi kwa namna ambavyo inaona inafaa.

Mhe. Naibu Spika, kuna nchi wameweka kampuni, na kampuni yenyewe ni ya serikali, lakini serikali inamiliki asilimia 51. Kuna nchi kama sisi tumesema tuanze na kampuni yetu iwe inamiliki asilimia 100, lakini baadae kwa sababu na hii ni biashara tutakapopata uwezo, basi inawezekana na sisi tukataka kufungua kama ambavyo wenzetu walivyofungua. Lakini angalizo liwe kwamba kwa namna yoyote ile tutakavyofanya lazima tuihakikishie kwamba kampuni ya serikali ndio inakuwa na *majority shareholder*, huwezi ukawa wewe ndio mwenye mafuta, lakini ukatoa *shares* zako zote ikawa wewe ndio *minority shareholder*. Lazima tuhakikishe kama sisi ndio tuna *majority shareholder*.

Mhe. Naibu Spika, sasa niwatoe hofu Waheshimiwa Wajumbe, na wala hatuna haja ya kutunishiana misuli wakati tunapitisha vifungu, baina ya sisi huku mbele na waheshimiwa rafiki zangu wa nyuma.

Nimeona zimeshaanza kutembea *schedule of amendment* kila mtu ana yake, inaonekana wamejifunza vizuri, hawataki kuwa *surprised,* kila mtu anakuja na yake. Lakini tunapokubaliana, basi tukubaliane kwamba jambo hili ni letu sote, hakuna haja ya kuvutana kwenye jambo ambalo lina maslahi na sisi sote, ufafanuzi utakapotolewa utolewe kwenye maeneo ambayo tutakubaliana na tukubaliane, lakini kwenye maeneo ambayo hatutokubaliana iwe ni hivyo, lakini isiwe kama kila upande unataka kung'ang'ania na kuona kwamba hapana hii ni ya kwangu. Hii sheria ni ya kwetu sote, na sisi tutakaoipitisha hapa ndio tutakaokuwa tunaingia kwenye historia, kwamba Baraza la Wawakilishi kwenye kikao hiki kimepitisha sheria hii ya gesi na mafuta kwa upande wa Zanzibar.

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, kama suala hili tutakapolipitisha basi tulipitishe kwa dhana hiyo.

Nimshukuru Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira inaonekana kilainishi alichokitumia ni cha hali ya juu, maana kuanzia Mwenyekiti wa Kamati mpaka wajumbe wengine wote wamelainika, wote kimya. Sasa kuna mawaziri wawili nao wana hoja zao hapa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, sasa uwape dawa hiyo ili waitumie na wao Waheshimiwa Wajumbe waweze kutulia wakati wa kupitisha vifungu, wapunguze joto, joto lipungue kidogo na tupitishe tukiwa tuna furaha.

Sasa baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, labda nisaidie kwenye maeneo machache ambayo yalizungumzwa na Kamati.

Moja ambalo lilizungumzwa na kamati ni kwenye kifungu cha 6(1) na 6(2)(d), kama kamati iliona kama imeeleza waziri, lakini haijulikani waziri gani ambaye atashirikiana na waziri husika wa ardhi. Sasa mimi nakubaliana na ushauri ambao nitamshauri Mhe. Waziri, ni vyema isomeke waziri kwa kushauriana na waziri mwenye dhamana ya fedha, halafu hicho kifungu kiendelee.

Lakini kwenye kifungu cha 1 Mhe. Shamsi alitoa hoja pia na kusema kwamba ukikisoma kile kifungu utaona kimeanza kutoa, waziri atashauriana na mamlaka lakini hakiendelei vile vilivyo. Sasa ushauri wangu ni vyema kifungu hicho cha 6(1) kisomeke, waziri baada ya kushauriana na mamlaka, atatekeleza kazi na wajibu ufuatao na kile cha (a), tufute yale maneno baada ya kushauriana na mamlaka, ili sasa ianze kutiririka vizuri.

Jengine ambalo kubwa waheshimiwa na hata na wewe Mhe. Naibu Spika, ulilizungumzia ni kifungu cha 12(3) ambacho kinazungumzia uteuzi wa wajumbe, lakini kikaacha kuzungumzia jinsia.

Ushauri wangu ni vyema kifungu hicho sasa kisomeke kifungu cha 12(3), wajumbe waliotajwa katika aya ya (c),(d),(e),(f) na (g) watateuliwa na waziri kwa kushauriana na waziri husika, na uteuzi huo kwa kadiri itakavyowezekana utazingatia jinsia. Kwa hivyo, itatoa fursa sasa kwa mawaziri hao watakapokaa kufanya uteuzi, lakini wakahakikisha kwamba wanazingatia jinsi katika kufanya uteuzi wao, kuliko hivi kilivyo ambavyo ni kweli mawazo yaliyotoka kwenye kamati kilikuwa hakitoi fursa hiyo. Sasa ushauri ni huo na tunakwenda vizuri. Tutakapopita kwenye vifungu kwa vifungu leo mtelezo tu hakuna mabuti. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Naibu Spika, lililozungumzwa ambalo na kamati imetoa ushauri ni hili suala sasa la kutia haya masharti ya kampuni yetu kwenye Katiba.

Mimi nadhani hapa tumekwenda mbali kidogo, ni jambo jema, lakini sidhani kwenye *stage* hii, hii ni biashara ni lazima tutambue. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba hii ni biashara na biashara huifungi kwenye katiba, biashara unaiachia ifanye biashara. Sasa kampuni hii itasajiliwa kwa mujibu wa sheria za makampuni. Sasa kuna utaratibu mzima ambao umewekwa ndani ya sheria ile, lazima iwe na *memorandum* na *article* yake ya *association*, lazima itaje idadi ya wakurugenzi ambao itakuwa nao, lazima itaje idadi ya *shares* ambazo itakuwa nazo.

Sasa mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kwenye suala hili tusifike huko mbali na kuanza kutoa uamuzi sasa wa kusema kwamba tutie masuala ya mafuta ya kampuni yetu kwenye katiba, nadhani tutakuwa tumekwenda mbali kidogo.

Mhe. Naibu Spika, mengine ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe, ni suala hili la kujua mipaka yetu.

Nadhani na Mhe. Waziri wa Fedha alilizungumza vizuri. Lakini pia na suala hili la Latham ambalo lilikuwa likizungumzwa muda mrefu, imekuwa kila kikao tukikutana hapa linazungumzwa. Kuna wengine hapa lazima wataje Fungu Mbaraka ndio itaonekana wamechangia mada, kwenye bajeti itazungumzwa, kwenye maswali itatajwa. Leo sijasikia, lakini muda wote linazungumzwa jambo hili.

Sasa Latham Mhe. Naibu Spika, limeanza kuzungumzwa muda mrefu sana, limeanza kuzungumzwa tokea miaka 1880. Kwa nini kisiwa hiki kikapewa jina la Latham. Kisiwa hiki kwanza kilipewa jina la Latham kwa sababu kuna meli ya Kiingereza ilikwenda kufunga gati pale mwaka 1758, ndio kutokana na meli ile kisiwa hiki kikapewa jina la Latham. Lakini kwa nini tunakiita Fungu Mbaraka, maana haya ni lazima tufanye utafiti na tuyajuwe, ili unaposimama kuchangia utakapoulizwa kwamba kwa nini wewe unasema hiki cha kwako, una ushahidi gani, lazima uwe nao. Asitoke mtu akaja kuuliza maswali ndani ya chombo hiki, halafu akaambiwa hebu thibitisha hayo unayoyasema, akawa yeye mwenyewe hana uhakika wa kile anachokifanya.

Sasa lazima kwanza tufanye utafiti, lazima sisi wenyewe turidhike na ule utafiti ambao tumeufanya, halafu ndio tuje kusuguana humu ndani, lakini Waheshimiwa Wajumbe ambao walikuwepo kwenye Baraza lililopita basi watakubaliana na mimi kwamba suala hili tumelitolea maelezo ya kina kabisa. Haya yalianza kuzungumzwa baina ya Wajerumani na Waingereza, ndio waliogawa haya mapande, mapande haya leo tunayokaa yaligaiwa na Wakoloni, wao ndio waliogawa, akawaambia wewe pande lako litakuwa hili na mimi pande langu litakuwa hili, ndio tumerithi kutoka kwao, baada ya wao kuamua kugawa kwa maslahi yao wenyewe.

Suala hili Mhe. Naibu Spika, mwaka 1890. Tarehe 19/10/1898 bendera ya Zanzibar iliwekwa rasmi kwenye kisiwa cha Latham.

Mwaka 1898 karne ngapi zimepita hizo, 800 eeh ndio! Karne ngapi zimepita kama tayari watu waliokuwa wakati huo walitambua kama kisiwa hiki ni

kisiwa cha Zanzibar, lakini sio tu kuweka bendera, lakini waliweka bendera na matamko yakaandikwa, matangazo kwamba kisiwa hiki kiko chini ya umiliki wa Sultan, ndio maana kutokana na hayo mwaka 1963 katiba iliyokuwepo ya mwanzo ilitambua pia kama Latham ni sehemu ya visiwa vya Zanzibar. Sasa huo ndio ushahidi ambao tunao. Kama ukisoma kumbukumbu zetu zote tulizokuwa nazo ndivyo hivyo ambavyo zinavyotuelekeza. Wajerumani ambao ndio walikuwa wakitawala Tanganyika, hakuna hata siku moja ambayo walizua mjadala na kuhoji umiliki wa kisiwa hiki baada ya kupelekwa bendera ndani ya kisiwa hiki.

Sasa hizi ndio kumbukumbu ambazo tunazisema kama ushahidi ambao sisi tunao, inaonesha kama kisiwa hiki tokea enzi hizo kilikuwa chini ya miliki ya Zanzibar. Sasa mwenye maelezo tofauti na haya basi aje nayo, halafu tujadiliane. Lakini sisi taarifa zilizokuwa serikalini ni kwamba kile ni kisiwa chetu, ni kisiwa cha Zanzibar, hakuna mtu ambaye mpaka sasa hivi amesema vyenginevyo. Sasa hili naomba tuelewane na hiyo tumeelewana, kama isije ikawa kila siku Mhe. Naibu Spika, tunayarudia yale kwa yale, mtu atakaa huko atakuja kuuliza hilo hilo.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana kuna taarifa nyingi tulizisambaza, sasa sisi tuko tayari kusambaza tena taarifa zile kwa Waheshimiwa Wajumbe hawa wapya, ili nao watakapokaa kujenga hoja ya kusema kwamba kisiwa cha Latham ni cha kwetu, basi wawe wanajenga hoja kupitia kwenye kumbukumbu ambazo zipo, wasijenge tu hoja ikawa na wao hawana ushahidi, kwa hivyo wajenge hoja wakiwa na wao wana ushahidi.

Kwa hivyo, ofisi yangu nitahakikisha kwamba tunawasiliana na Ofisi ya Katibu, ili kutoa *photocopy* ile taarifa ambayo tuliipeleka Baraza la Mapinduzi, na ile taarifa ambayo tulikuja kuitoa hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, ili Waheshimiwa Wajumbe nao wawe nayo, kwa wakati wao wapate kuisoma historia hii ilivyo.

Mambo haya yalianza muda mrefu sana Mhe. Naibu Spika, tokea miaka hiyo ya 1880, hayakuanza kuzungumzwa leo. Sasa suala hili la mipaka ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelizungumza, na kama ambavyo Mhe. Waziri wa Fedha amelisema. Ukisoma Katiba yetu ya Zanzibar, ibara ya kwanza kabisa ya Katiba ya Zanzibar inasema, Zanzibar na mipaka yake. Sasa tujiulize kwa nini Zanzibar na mipaka yake, isiwekwe ibara ya mwisho, ikawekwa ibara ya kwanza kabisa inazungumzia Zanzibar na mipaka yake.

Lakini ibara ya pili, ikazungumzia Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ilizungumza vizuri ilisema, Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba, pamoja na visiwa vidogo vidogo vilivyozunguka na bahari yake, ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Sasa hili ndio tamko la kikatiba, baada ya hapo Katiba haikusema kitu ilinyamaza. Je, hatuna kumbukumbu nyengine inayothibitisha haya mambo yaliyoelezwa kwenye katiba?

Mhe. Naibu Spika, yapo, na mkataba maarufu uliokuwepo wa *Anglo - German Treaty* wa mwaka 1890, au kwa jina jengine unaitwa *Heligoland*, ndio mkataba ambao uligawa mipaka baina ya Muingereza ambaye ndiye alikuwa anamlinda huku Sultani, na Wajerumani ambao ndio walikuwa wakitawala Tanganyika. Sasa ukisoma mkataba ule hata kisiwa cha Lamu kilikuwa kwetu, hata Mafia pia ilikuwa kwetu, maeneo mengi tu yalikuwa chini ya himaya ya Sultani. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wapate fursa wapitie mkataba huu. *(Makofi)*

Sasa pa kuanzia Mhe. Naibu Spika, tunapo. Kama kuna tatizo ambalo linatokea huwezi ukasema huna pa kuanzia, pa kuanzia ni mwaka 1890 ambapo mkataba wa *Heligoland* baina ya Wajerumani na Waingereza ndio uliogawa mipaka baina ya Tanganyika na Zanzibar.

Baada ya Mapinduzi na baada ya Jamhuri kupata uhuru wao, hakuna mtu aliyekaa kuanza tena kujadili mipaka. Kwa sababu sote tukijua kama tayari tumesharithi mipaka hii kutoka kwa Wakoloni. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, kwamba tupate fursa hii mikataba tunayoizungumza tupate kuisoma, tukishaisoma mikataba hii halafu sasa tuje kukaa tujadiliane kama kwa nini Lamu imeondoka sasa sio tena sehemu ya Zanzibar, kwa nini Mafia imeondoka sio tena sehemu ya Zanzibar, haya ndio mambo ambayo inabidi tujadilane, tukishakujadiliana na tukakubaliana sisi sote tunakuwa na kauli moja tunapoulizwa huko mitaani nitakavyojibu mimi ndivyo atakavyojibu Mhe. Gavu, na atakavyojibu Mhe. Gavu ndivyo atakavyojibu Mhe. Hassan wa Welezo. Kwa sababu itakuwa tafsiri ambayo tumeipata ni tafsiri yetu sote, na hii ndio inavyotakiwa Mhe. Naibu Spika, kuliko kukaa na kila mtu akawa na tafsiri yake mkononi.

Hatuwezi kuzungumza mambo makubwa kama haya ya nchi lakini kila mtu akawa ana tafsiri yake mkononi, ukiniuliza mimi nina tafsiri yangu, ukimuuliza Mhe. Sarahan ana tafsiri yake, ukimuuliza Mhe. Miraji naye ana tafsiri yake, haiwezekani. Haya Mhe. Naibu Spika, ni mambo ya nchi, sasa lazima sisi

viongozi tuwe na tafsiri moja, lazima tuelewane na tukubaliane ili tunapokwenda kwa wananchi huko, nyinyi wenye majimbo mkizungumza nao muwaeleze kutokana na historia ambayo tumeirithi na kutokana na kumbu kumbu ambazo tunazo. Sasa niwatoe hofu Waheshimiwa Wajumbe kama kwenye jambo hili hakuna *dispute* ambayo itaweza ikatokea na ikatufarakanisha.

Pia na Mhe. Waziri wa Fedha amezungumza vizuri umoja wa mataifa umetengeneza sheria maalumu; sheria ya bahari ya mipaka maalumu, kuzungumzia mambo haya tu na inaelezea utaratibu wa jinsi gani nchi zinapoanza kutaka kugawa mipaka ya baharini iweze kugawa, sasa taratibu za kisheria zipo nyingi Mhe. Naibu Spika. Sitaki kuchukua muda mrefu kwa sababu unajua yote haya ninayoyasema tutakapofika kwenye vifungu Waheshimiwa Wajumbe watasimama.

Lakini mengine ambayo ni lazima tuyajue Mhe. Naibu Spika, ni jinsi gani tunaweka utaratibu wa kodi, mpaka tukaja na jadweli ambalo lipo ndani ya sheria hii. Kuna taasisi ambazo kazi zao ni kufanya haya mambo tu, na kila mwaka wanatoa ripoti, ukitizama ripoti iliyotolewa mwaka 2015 ya *Oil and Gas Tax Guide for Africa* imetolewa na *Price Waterhouse and Coopers*. Hii ni taasisi moja muhimu ambayo inashughulika na mambo haya, imetoa kodi ya kila nchi ya Afrika inayochimba mafuta kila nchi imeelezea, Tanzania inatoza nini, Angola inatoza nini, Botswana inatoza nini, Uganda inatoza nini, Ni *document* yenye *page* mia mbili. Sasa mwekezaji anapokuja hatizami Uingereza inatoza kodi gani kwa sababu yeye haendi kuwekeza Uingereza, yeye anatizama kwenye *region* yako wewe unatoza nini na kwenye *region* atatizama East Africa, kama Kenya ana utaratibu gani wa kutoza kodi, kunatofautiana vipi na utaratibu wa Tanzania.

Lakini atatizama kwenye *region* ya *SADC* kama kuna nchi zinachimba mafuta nao utaratibu wao wa kodi ukoje, sasa investors hawa hawa Mhe. Naibu Spika, wanapokuja wanakuja wakiwa tayari wameshapitia *documents* zote hizi, sasa sisi ukisoma utaratibu wetu wa kodi na ukisoma utaratibu ambao upo kwenye *region* yetu hautofautiani, kwa sababu haiwezekani Mhe. Naibu Spika, wewe kwenye eneo lako ukaanza kutoa kodi ambazo ni tofauti na eneo ulilokuwapo wewe hatokuja mwekezaji atakimbilia kwengine. Wenzetu wa Libya wao walikuwa wakisema ukishachimba asilimia 90 itabaki pale Serikalini na 10 ndio atapewa mkandarasi, lakini wenzetu walishajitosheleza kwa mafuta yaliyokuwepo, sasa sisi ndio kwanza tunaanza, hatuwezi tukaweka kodi ambazo zitawakimbiza wawekezaji, hatuwezi sasa hivi tukasema sisi tuwe

kama Libya, leo Libya nani anakwenda hata useme mwekezaji achimbe pale achukue yeye kila kitu hakuna mtu atakayekwenda.

Hili naomba nilisisitize sana kwa Waheshimiwa Wajumbe, kama yote haya tunayoyafanya hayatoweza kutimia kama hatutonadi utulivu na amani ndani ya nchi hii, kama hakuna utulivu na amani ndani ya nchi hii hatokuja mtu kupoteza pesa zake akaja kuwekeza. Kwa sababu mwekezaji anataka atakapowekeza ajue kesho asubuhi akiamka hali ya nchi itakuwa tulivu kama alivyoiacha jana usiku alivyokwenda kulala, sasa leo nani anakwenda kuwekeza Syria, nani anakwenda kuwekeza Iraq hata uweke senti za aina gani hakuna mtu atakayekwenda kupoteza pesa zake kuwekeza. Sasa hili niwaombe sana waheshimiwa Wawakilishi, kama tunapopitisha sheria hii basi ni lazima twende huko tukahutubie amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya hayo mfalme Feisal wa Saudi Arabia yeye aliulizwa baada ya Saudi Arabia kuanza kupata mafuta, wakamuuliza unaonaje maendeleo ya Saudi Arabia baada ya sasa kupatikana neema hii ya mafuta, jawabu lake likawa kwenye zama zao ameiona Saudia inatoka kwenda kupanda ngamia na kwenda kuendesha ma-*CADILLAC* kwa wale wanayoyajua ni yale magari ya Kimarekani makubwa yale yenye milango sita kama la Obama lile. Anasema Saudia imeondoka kwenye kupanda ngamia kwenda kuendesha Ma-*CADILLAC* kwa jinsi wanavyotumia fedha za mafuta.

Lakini akasema ana wasi wasi kama vizazi vitakavyokuja baada yao watarudi tena kwenda kupanda ngamia kwa sababu ya fedha wanavyozitumia, sasa mimi nishukuru sana michango ambayo imetoka humu kwa Waheshimiwa Wajumbe kama lazima sisi tuweke utaratibu wa kuhifadhi hizi fedha zetu, *tusiache mbachao kwa msala upitao*. Tusiache mbachao, haya ndio yaliyowakuta wenzetu wa Uholanzi ukisikia *Dutch Disease,* ni hii kama waliacha mbachao wakashughulika na mambo mengine, sisi zao letu lililokuwa likitutoa hapa ni zao la karafuu, lakini ulipokuja utalii tukasahau kule kidogo tukashughulika kwenye utalii.

Leo Serikali ya awamu hii ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ndio tunaanza kuhangaika sasa kuirudisha karafuu kwenye chati, tuliacha kidogo mbachao tukashughulikia utalii, sasa lazima vitu hivi vitatu Mhe. Naibu Spika, lazima tuwe navyo tuendeleze mambo yetu ambayo tunayo; zao letu la karafuu lakini pia na utalii, hatuwezi kuanza kuchimba mafuta ikawa bahari zetu ni chafu, ikawa bahari zetu zinadondoka mafuta, lazima tuhakikishe pia tunalinda mazingira ili tuweze pia kuwafanya watalii waweze kuja zaidi na zaidi.

Pia, tulisimamia eneo hili sasa hivi vizuri, na kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba kile ambacho kama tumesema kwenye Mswada kama mali hii ni mali yetu basi iwe yetu kweli, iwe yetu sisi na wale ambao watakuja baada yetu.

Sasa mwisho Mhe. Naibu Spika, katika hoja za kamati ambazo walisema ni kifungu cha 151 wakasema vile ilivyo hatutokuwa tunatenda haki kama Serikali hii haitoitambua mikataba yote ambayo tayari imeshaingiwa na wawekezaji ambao waliokuwepo.

Ushauri wangu tufanye marekebisho kwenye kifungu cha 151(2) na ile ya 2 sasa hivi iwe ya 3 na ule mtiririko wa namba utakuwa kama utakavyokuwa. Na tuandike kama ifuatavyo.

" Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha kwanza, Serikali inaweza ikiona kuna haja kufanya hivyo kupitia upya mikataba iliyoingiwa awali na kuweka masharti mapya ya utekelezaji kwa kuzingatia masharti ya sheria hii".

Sasa hivyo hatutokuwa tumeifunga Serikali, yeye mwenyewe ndio ataamua akiona ipo haja ya kuwaita basi atawaita, lakini akiona hakuna haja basi ataendelea maana kile kifungu cha kwanza tumekiacha kama kilivyo.

Sitaki niendelee kusema mengi, naomba nirudie kwamba na mimi naungana na Waheshimiwa wenzangu kuiunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi kwa asilimia mia moja, niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kama tuipitishe hoja hii tukiwa na furaha, tujue kama tunaanzisha sasa Zanzibar mpya ambayo baada ya miaka ishirini itakuwa tofauti na hii ambayo tunayo sisi leo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na uzima tukawa tunaendelea na shughuli zetu mpaka muda huu.

Pia nikushukuru wewe kwa kunipa muda huu wa kuweza kutoa ufafanuzi na maelezo juu ya baadhi ya hoja na mapendekezo yaliyotolewa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nianze basi na suala la elimu kwa wataalamu.

Sera ya Mafuta na Gesi Asilia imetoa muongozo juu ya kujitosheleza kwa wataalamu wa ndani ili kuweza kufaidika kikamilifu na rasilimali hii ya mafuta na gesi asilia. Umuhimu wa uendelezaji wa rasilimali watu ni jambo lililosisitizwa kwa mashirikiano ya pamoja baina ya Serikali kuu, Makampuni ya mafuta, na washirika wa maendeleo mbali mbali, hili tumeanza kulitekeleza na faida zimeanza kuonekana, wataalamu tulionao kwa sasa tofauti na hali ya hapo kabla.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu itahakikisha kwamba inafuata matakwa ya Sheria ili kufikia malengo yaliyopangwa kuhusiana na kujitosheleza kwa wataalamu wa ndani.

Sehemu ya Saba ya Mswada huu imezingatia tamko la sera kuhusiana na elimu kwa wataalamu wa ndani ikijumuisha taasisi za elimu ya juu na vyuo vya amali, hata hivyo naomba kupokea ushauri kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kufikia lengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu mpaka hivi sasa tayari ina wataalamu wafuatao:

- Wahandisi wa Mafuta na Gesi Asilia 4,
- Wataalamu wa *Geology* 3,
- Mhandisi wa Umeme na Mawasiliano 1,
- Wataalamu wa Nishati 2,
- Mhandisi wa Mazingira 1,
- Mwanasheria wa Mafuta 1 na
- Mtaalamu wa afya na usalama kazini katika masuala ya Mafuta na Gesi 1.

Kati ya wafanyakazi hawa 13 wafanyakazi 10 wamehitimu shahada ya pili na watatu wamehitimu shahada ya kwanza katika fani zao, lengo kubwa kwa sasa ni kuwa na wataalamu waliohitimu shahada ya pili kwa kusimamia hatua za awali za utafutaji na ngazi nyengine za elimu zitafuatia kwa idadi kubwa katika hatua nyengine kama vile Mafundi Mchundo katika ngazi ya uzalishaji n.k.

Hata hivyo jumla ya wahitimu 11 wamemaliza mwaka jana na wako katika taratibu za uajiri, wanafunzi 60 wako masomoni katika vyuo mbali mbali duniani, takriban wanafunzi wote wanaomaliza katika vyuo hurejea Zanzibar kwa kuomba ajira. Napenda kuungana na Wajumbe kuhusiana na kutengeneza utaratibu bora wa kimaslahi na vivutio vyengine vikiwemo kuwapatia elimu zaidi, mfumo ambao utazingatia kuwaenzi na kuwavutia wafanyakazi kubaki na kutumika nchini kwa uzalendo.

Hata hivyo hatua hii ya kuimarisha wataalamu isiwe kwa Wizara yangu tu bali hata kwa mawizara mengine kama ilivyotanabahishwa na baadhi ya Wajumbe. Suala la elimu kwa wananchi kwa ujumla. Mhe. Naibu Spika, kama lilivyo suala la elimu kwa wataalamu, elimu kwa jamii imezingatiwa vyema katika kifungu cha 4 cha Sera ya Mafuta na Gesi Asilia.

Wizara katika kutekeleza hili imeshaanza kutoa elimu katika ngazi za Serikali na jamii, tumejipanga kuendeleza kupitia midahalo, semina na katika ngazi mbali mbali za jamii. Jumla ya taasisi 9 za Serikali zimeshiriki katika mafunzo ya mafuta na gesi asilia na warsha mbili zimefanyika kwa jamii, Unguja na moja Pemba. Mara tu baada ya Mswada huu kupitishwa Wizara imejipanga kutoa elimu kwa wananchi ili kupata uelewa na ufahamu wa Sheria kwa faida yao na Taifa kwa jumla.

Suala la Fedha na Mapato yatokanayo na Rasilimali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la masuala ya mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta na gesi asilia yatasimamiwa na sheria ya usimamizi wa mapato ya mafuta na gesi asilia kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 154 cha mswada huu na utakuwa chini ya mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na hapa napenda nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid kufafanua masuala mengi yanayohusiana na hayo, na naamini waheshimiwa wajumbe wamemuelewa vya kutosha.

Suala la Mamlaka ya Waziri. Mhe. Naibu Spika, ingawa Mhe. Waziri amepewa majukumu mbali mbali ya kuyatolea uamuzi kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 6 cha Mswada huu, ni vizuri ikumbukwe kuwa Mamlaka kama chombo kikuu cha udhibiti wa shughuli zao za utafutaji mafuta na gesi asilia ni mshauri mkuu wa Waziri katika shughuli zote za uendeshaji.

Vile vile maamuzi yote makuu katika sheria hii kama vile ufunguaji na ufungaji wa vitalu, uingiaji wa mikataba ya mafuta na gesi asilia, mazungumzo ya moja kwa moja na makampuni na kadhalika ni lazima Waziri apate baraka za Baraza la Mapinduzi.

Suala la kudumisha amani na utulivu nchini. Mhe. Naibu Spika, napenda kuungana na wajumbe wote waliochangia hoja hii ya msingi, na bila ya shaka yoyote Serikali itaifanyia kazi kwa nguvu zake zote kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea kutawala nchini pamoja na uendeshaji wa masuala ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Naibu Spika, Baadhi ya Wajumbe wamezungumzia masuala ya bodi na mamlaka yanayohusiana na sifa za kinga na wajumbe wa bodi pamoja na watendaji.

Napenda kuchukua nafasi hii kuelezea umuhimu wa shughuli yenyewe ambayo inahitaji uangalifu, uadilifu na uwezo mkubwa kwa kusimamia majukumu ya kazi zao.

Katika kifungu cha 15 cha Mswada huu imeelezwa sifa za uteuzi wa wajumbe ambazo nikiri ni za kiwango kikubwa, napenda kuwahakikishia Wajumbe kuwa watu wenye sifa hizo wapo hapa Zanzibar na kwamba Serikali itakuwa makini katika uteuzi wa Wajumbe hao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala la kinga kwa Wajumbe na watendaji. Napenda kuwatoa hofu waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi kuwa kinga hiyo haitomlinda mtendaji aliyetenda kosa kwa makusudi, kinga iliyokusudiwa ni ya kuwajengea uwezo wa kujiamini katika utendaji wao wa kazi.

Kuhusiana na uwasiliaji wa ripoti ya mwaka mbele ya Baraza lako tukufu. Suala hilo lina umuhimu wake kutokana na uzito wa shughuli za uchimbaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia, ni lazima tusimamie katika utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza Mhe, Wanu Hafidh Ameir kwa michango yake ya kuimarisha vifungu mbali mbali vya mswada huu, ambavyo Mwanasheria Mkuu amesikia na vitazingatiwa ipasavyo.

Kuhusiana na suala la kuadhibiwa kwa mamlaka kifungu cha 7(2)(a) kimeelezea wazi kwamba mamlaka inaweza kushtaki ama kushtakiwa.

Mhe. Naibu Spika, vigezo vilivyotumika katika kuweka mirahaba vimezingatia ushindani katika eneo zima la Afrika ya Mashariki na uzoefu duniani, viwango vidogo vitasababisha mapato madogo kwa Serikali, lakini viwango vikubwa zaidi pia vitasababisha kukimbiza wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, ushauri umetolewa na kuongezwa vifungu na kurekebishwa baadhi ya vifungu. Naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa nyongeza na marekebisho hayo yamepokelewa na yatafanyiwa kazi ipasavyo.

Ushauri juu ya mazingira, haki za wafanyakazi na usalama wao kazini, jinsia, maradhi ya kuambukiza pamoja na suala la uajiri wa wazawa yamezingatiwa katika sehemu ya sita na ya saba ya mswada huu.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la wadau walioshirikishwa katika kupitisha sera na sheria ya mafuta na gesi asilia naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Ikumbukwe kuwa utengenezaji wa Sera na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ni suala lililotekelezwa na Serikali kwa nia safi kabisa katika muda mfupi sana mara tu baada ya kupitishwa sheria ya mafuta na gesi asilia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Agosti 2015.

Katika kipindi hicho kifupi Serikali imetumia mbinu ya kushirikisha sekta mbali mbali za Serikali, viongozi wakuu, Wawakilishi wa wananchi na wataalamu wetu wa ndani, na ndio maana tukaweza kufanikiwa kufikia hatua hii ya leo ambayo ni ya kupigiwa mfano, kazi kubwa tuliyonayo kwa sasa ni kuhakikisha sera na sheria hii zinafikia wananchi katika ngazi mbali mbali.

Kama nilivyotangulia kueleza hapo awali elimu hii itaendelea kutolewa siku hadi siku kulingana na mahitaji na wakati, waheshimiwa tunaomba msaada wenu wa hali ya juu katika suala hili.

Vile vile, wataalamu walioshiriki katika kutayarisha sera na sheria hizi hawakupata uwanja mkubwa wa kutembelea nchi mbali mbali kutokana na sababu za muda, hata hivyo nchi zilizotembelewa na baadhi ya wajumbe ni pamoja na Norway, Uholanzi, China, Uganda na Tanzania Bara. Kwa kutumia *TEKNOHAMA*, uzoefu wa nchi mbali mbali umezingatiwa na kamati husika katika kutayarisha sera pamoja na Mswada katika kiwango ambacho tumekishuhudia. Hata hivyo, uzoefu katika ulimwengu unaonesha kuwa hitilafu ndogo ndogo zinapojitokeza katika matumzi ya sera na sheria za mafuta na gesi kutokana na changamoto mbali mbali hupatiwa ufumbuzi kwa kuzipitia sera na sheria hizo kila inapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, suala la fidia tayari limeelezwa vya kutosha katika kifungu cha 99 cha mswada huu, mahitaji yatakayojitokeza kwa mujibu wa wakati yatashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, suala la uwazi katika shughuli za mafuta na gesi asilia limesisitizwa sana katika vipengele tofauti tofauti vya mswada huu, ili kuondoa mianya ya rushwa na ajenda za siri.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni, naomba kuwasilisha. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mpaka kufikia hapa leo tumemaliza shughuli yetu kwa mchana huu, sasa ningewaomba kwamba jioni Mhe. Waziri anayehusika atakuja kujibu hoja zenu, kwa hivyo ningewaomba sana mufike kwa wakati ili mupate kusikia, na isiwe kwamba kwa sababu mtu hakuwepo hapa tena ikawa buti nyingi sana. Kwa hivyo ningewaomba sana muhudhurie kwa wakati na naamini mimi mkihudhuria kwa wakati hata shughuli hii tutaimaliza kabla ya ule wakati wake ambao umepangiwa.
Baada ya kusema hayo naahirisha kikao hadi saa 11.00 jioni leo Ahsanteni.

(Saa 7.19 Mchana kikao kiliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe leo tutakuwa tunamaliza mswada wetu huu wa Mafuta na Gesi Asilia kama ambavyo mumeshasikia, kwa hivyo nitampa Mhe. Waziri afanye majumuisho na baadae tutaingia kwenye Kamati kwa ajili ya kupitisha vifungu.

Waheshimiwa Wajumbe leo kwa sababu ya ukubwa wa huu mswada tutakuwa na utaratibu tofauti kidogo wa upitishaji vifungu, tutatumia Kanuni ya 87(3) ambayo inasema kama ifuatavyo:-

"Kamati ya Kutunga Sheria itajadili na kupitisha, au kufanya mabadiliko na kupitisha, Mswada kifungu kimoja baada ya kingine, isipokuwa kwamba Mwenyekiti anaweza kutoa kwa Kamati ya Kutunga Sheria suala kuhusu kujadiliwa kwa kundi moja lenye vifungu kadhaa au vilivyomo katika sehemu moja ya Mswada".

Sasa mswada wetu Waheshimiwa Wajumbe una sehemu kumi nitakuwa ninakutajieni hiyo sehemu na vifungu vilivyomo kwa mfano kama cha 1 mpaka cha 8 au cha 9 kilichomo katika ile sehemu ya kwanza, halafu Mjumbe ataweza kunyanyuka sasa na kuhoji kifungu chochote ambacho kimo katika mafungu hayo halafu baadae Serikali itaweza kujibu. Lakini pia kifungu itakuwa kama mwanzo kwa mujibu wa kanuni kwamba hakitahojiwa zaidi ya mara tatu kifungu mahususi ndani ya sehemu hiyo. Kwa hivyo utaratibu utakuwa ni kama ule wa zamani, lakini kwenye kuhoji kupitisha tutakuwa tunaipitisha sehemu

nzima ili kuweza kuokoa muda, kwa sababu mswada ni mkubwa sana na sijajua Mhe. Waziri anahitaji muda gani kwa ajili wa kumaliza na sitaki nimfunge ili aweze kukuridhisheni.

Baada ya kusema hayo machache sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili aweze kumalizia sasa hivi kwa kujumuisha mswada wake. Karibu sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutuwezesha kufika hapa leo tukiwa na afya njema na amani na utulivu.

Aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa umakini wao na michango yao yote iliolenga katika kuiboresha sheria hii muhimu sana kwa mustakbali wa nchi yetu. Wameuliza maswali mengi kwa ufasaha, kushauri na kutoa maoni na kutupa hongera na pongezi nyingi kwa kufanikisha kuwepo kwa mswaada huu muhimu ulioandika historia ya Zanzibar leo hii.

Ushauri na maoni yenu ni muhimu sana kwetu na tunashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako niwataje wote waliochangia moja kwa moja na wale waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Waliochangia moja kwa moja ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti)
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said (Makamo Mwenyekiti)
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Simai Mohammed Said
5. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
6. Mhe. Ussi Yahya Haji
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
9. Mhe. Shamata Shaame Khamis
10. Mhe. Omar Seif Abeid
11. Mhe. Mgeni Hassan Juma
12. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
13. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
14. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri
15. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi

16. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma
17. Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa)
18. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
19. Mhe. Shehe Hamad Mattar
20. Mhe. Said Omar Said
21. Mhe. Said Soud Said
22. Mhe. Juma Ali Khatib
23. Mhe. Mohamed Aboud Mohamed
24. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed
25. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Waliochangia kwa Maandishi ni:

1. Mhe. Riziki Pembe Juma
2. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
3. Mhe. Tatu Moh'd Ussi
4. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
5. Mhe. Hamida Abdalla Issa
6. Mhe. Chum Kombo Khamis
7. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
8. Mhe. Ame Haji Ali
9. Mhe. Moudline Cyrus Castico
10. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
11. Mhe. Ali Khamis Bakari
12. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf
13. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
14. Mhe. Khamis Juma Mwalim

Mhe. Spika, hawa wote niliowataja waliweza kuchangia mswada huu muhimu sana.

Baada ya uchambuzi wa michango ya Waheshimiwa Wajumbe, hoja zote zimejikita katika maeneo makuu matano ambayo tuliyaweka kwa pamoja.

1. Suala la elimu kwa wataalamu na wananchi kwa jumla
2. Suala la fedha na mapato yatokanayo na rasilimali hiyo
3. Suala la mamlaka ya Waziri
4. Suala la mipaka ya Zanzibar
5. Suala la kudumisha amani na utulivu nchini
6. Mengineyo yaliojitokeza

Mhe Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba ushauri, mapendekezo na pongezi zilizotolewa katika Hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi yamepokelewa na yatafanyiwa kazi ipasavyo. Mambo muhimu yaliyokuwamo katika hotuba hiyo ni pamoja na:-

- Elimu kwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu hata baada ya kupitishwa kwa Mswada huu
- Elimu kwa wananchi kwa jumla ikiwa ni pamoja na kutumia vyombo vya habari
- Tafsiri ya Sera ya Mafuta na Gesi Asilia kwa lugha ya Kiswahili
- Kuhakikisha kuwa maslahi ya Wataalamu wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia yanazingatiwa ili kuwaenzi wataalamu hao. Lakini mwisho walijikita katika mashirikiano ya karibu baina ya Taasisi za Serikali.

Kwa ujumla sina budi kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya hasa katika kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu, misamiati na upangaji wa vifungu hivyo, na nina hakika baada ya marekebisho hayo masuala mengi ya wajumbe yatakuwa tayari yameshapata majibu, masuala yote ya kisheria yataendelea kufanyiwa kazi kupitia ofisi ya Mwanasheria Mkuu ikishirikiana na Wizara yangu.

Mhe. Spika, kwa kuwa maswali mengi ambayo yalichangiwa tuliyachanganya katika kuyajibu kwake kama nilivyoeleza awali na Mhe. Naibu wangu wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ameyatolea ufafanuzi wa kutosha sina haja ya kurejea.

Mimi naomba nizungumze suala la mipaka na migogoro itakayojitokeza ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali mengi ameweza kuyafafanua.

Kwanza naomba kuwahakikishia na kuwatoa hofu wajumbe wako wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kuwa hakutotokea mgogoro wowote utakaojitokeza baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu Kuu zifuatazo:-

1. Dhamira za viongozi wetu wakuu wa nchi katika kufanikisha suali hili.

Sote tumekuwa mashahidi katika mkutano wa hadhara wa CCM uliofanyika Kibanda Maiti wakati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akiwahutubia wana CCM na wananchi kwa jumla alitamka wazi dhamira yake na kuitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

iharakishe kukamilisha mchakato huu ambao leo hii tunaufanyia kazi ili Zanzibar iweze kuwa na mamlaka yake ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Vile vile tafsiri ya suala zima la mipaka liko wazi katika Katiba zote mbili; ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla na baada ya muungano na hili Mwanasheria Mkuu alifafanua vizuri sana.

Aidha naomba mkumbuke kuwa muungano huu umejengwa juu ya misingi ya udugu, upendo, urafiki na ujirani mwema. Ambapo hata siku moja mimi naamini hatuwezi kufarakana katika maswali yenye malengo ya kukuza uchumi na maendeleo ya nchi zetu.

Mhe. Spika, kutokana na hoja hiyo, nawashauri Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuupitisha Mswada huu na kuwa Sheria kamili ili Wizara yangu ianze kulishughulikia suala hili la mipaka, ugawaji wa vitalu na usimamizi wake chini ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Ni imani yangu kubwa na bila shaka yoyote kuwa jambo hili halina matatizo kati ya Serikali zetu mbili na tunategemea kupata mashirikiano makubwa mno kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na rasilimali za mafuta na Gesi Asilia.

Mhe. Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wajumbe waliozungumzia sana suala la amani na utulivu. Sisi lazima tukubali kuwa nchi hii inaendeshwa na viongozi mahiri, wenye busara, hekima na uadilifu chini ya Chama cha Mapinduzi ambapo dira yetu ni kuwa na nchi huru yenye amani na utulivu.

Mhe. Spika, mimi naamini kwa mashirikiano ya pamoja kati yetu sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wananchi na vyombo vya ulinzi, nchi hii itaendelea kuwa ya amani, najua kuwa wapo wachochezi wanaotamani siku moja nchi hii isieleweke, itetereke lakini kwa uwezo wa *Allah* hawatoweza kutimiza ndoto hizo milele. Serikali hii iko makini katika kulinda usalama wa wananchi wake wakati wote.

Mhe. Spika, kwa ujumla maelezo aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri wangu, Waziri wa Fedha na Mipango na ufafanuzi alioutoa Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba yachukuliwe moja kwa moja kuwa ni sehemu ya majibu yangu.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Usimamizi (Utafutaji na Uchimbaji) wa Mafuta Na Gesi Asilia, Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Kuhakikisha Uwajibikaji wa Taasisi za Mafuta na Mambo mengine yanayohusiana na hayo

Sehemu ya Kwanza

Vifungu vya Awali

Katika sehemu hii itaanzia Kifungu cha 1 mpaka cha 3

Sehemu ya Pili

Haki za Mafuta na Gesi kusimamiwa na Serikali

Katika sehemu hiyo kinaanza kifungu cha 4 hadi 5

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilileta *schedule of amendment* ya Sehemu ya Pili ambayo ina vifungu 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7. *Schedule of amendment* yangu ipo katika sehemu ya 8 kifungu cha 8(2)

Sehemu ya Tatu

Mamlaka ya Udhibiti (Utafutaji na Uchimbaji) wa Mafuta na Gesi Asilia na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia

Utaanza kuanzia kifungu cha 7 mpaka cha 32 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunitanabahisha.

Mhe. Spika: Samahani kidogo, wataalamu wa wizara wanaweza wakashuka chini.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti katika *schedule of amendment* yangu kwa niaba ya wakwezi na wakulima nilileta mapendekezo ya kifungu cha 8 baada ya kukifanyia utafiti wa hali ya juu. Kazi za Mamlaka zitakuwa kama zifuatazo:

Katika *schedule of amendment* yangu nilipendekeza kifungu cha 8(2) kirekebishwe kwa kuongeza aya ya (u) iliyopo sasa iwe (v), aya hiyo mpya isomeke kama ifuatavyo:

Kupitia mkataba inayohusiana na mafuta na gesi asilia kabla ya kusaini na Kampuni. Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii tunayoipitisha kifungu cha mwisho ni kifungu cha (u) niliomba kiongezwe kwa sababu hawa wataalamu wapewe kazi ya kupitia mkataba pia, kwa sababu nchi nyingi za kiafrika Mhe. Mwenyekiti zinafeli katika mikataba. Sasa wapewe na kazi nyengine ya kupitia mkataba.

Mhe. Mwenyekiti wanaokuja kufunga mikataba wanakodi wataalamu wa kuishurutisha Taasisi au nchi au kikundi cha watu kiwezeshe kufunga mikataba na sisi wataalamu hatuna, wamesomea *small printing*, wamesomea *convincing language*, ni wataalamu waliobobea katika kuhakikisha mtu ana-*sign* mkataba, na sisi basi kwa unyonge wetu hapa ndipo tunapotakiwa kama nchi tulinde mafuta yetu katika mikataba.

Kwa hivyo nimependekeza hii iwe na jukumu jengine la kupitia mikataba kabla ya haijatiwa saini.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimeona hoja ambayo Mhe. Hassan amekuja nayo kama katika kazi hizi ambazo mamlaka imepewa tuzidishe kifungu ambacho kitaonesha yale ambayo ameyapendekeza. Lakini nimhakikishie Mhe. Hassan kama angesoma kifungu cha 6(1)(d) lakini pia kama angesoma kifungu hicho hicho cha 8(2)(l) hizi zote ni kazi za mamlaka ambayo wamepewa kupitia hiyo mikataba kabla ya kumshauri waziri. Sasa kimsingi yale ambayo anayapendekeza tayari yameshakuwemo kwenye sheria. Sasa kuongeza kifungu chengine ni kurudia yale yale ambayo tayari yameshaingizwa kwenye sheria. Sasa yeye angesoma kama hivi havitoshelezi maana vyote vimo, kwamba moja ya kazi ya mamlaka ni hiyo, wao wanapitia halafu sasa wanamshauri Mhe. Waziri kabla hakupeleka Baraza la Mapinduzi. Sasa anachosema Mhe. Hassan tayari kimo kwenye mswada wenyewe wa sheria Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeipitia kwa kina sijaona pahali panaposema kupitia hii mikataba, sasa ningeomba Mhe. Mwanasheria Mkuu aniongoze, hoja yangu ni mikataba, hii Bodi pia iwe inapitia mikataba, iwe *one of the* jukumu ni kupitia mikataba na mambo mengine lakini sijaona mikataba. Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu mwenzangu ana macho mengi angeweza kunionesha ningeshukuru sana. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru, inawezekana hilo neno analolisema Mhe. Hassan kupitia halimo lakini unapoweka kifungu ukasema itasimamia maana yake ndio kazi hizo ambazo imepewa mamlaka, kusimamia pia kupitia mikataba hiyo. Sasa tafsiri ya maneno ambayo hii imebeba dhana na tafsiri pana ambayo tayari imo, ndio maana tukasema hata hicho kifungu cha 8(2)(l) tayari imeshakidhi haja ambayo Mhe. Hassan amekuja nayo. Sasa ni kuongeza tu vifungu kwenye vifungu ambavyo tayari maelekezo yake yameshatolewa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, hatushindani, leo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeleta mswada mzuri kwa maendeleo ya nchi yetu sote tunaukubali lakini tuna jukumu la kulinda maslahi ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti kwa ushahidi nchi 9 nimefanya utafiti zinakwama katika mikataba. Mhe. Mwanasheria Mkuu kasema vizuri lakini ninachokipendekeza kipewe jukumu la kupitia mkataba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa nimefanya hii kazi tumejua jinsi gani nchi za Kiafrika zinavyoibiwa, hatushindani hapa, hapa tunaunda maslahi ya Wazanzibari. Mikataba hii lazima ipitiwe na watu wasiozidi 40, kwa sababu ndipo tunapoibiwa na kufeli, wenzetu wako *specialists* katika masuala ya mikataba Zanzibar nzima na Tanzania kama sikosei hakuna *specialist* aliye-*specialized* katika masuala ya mikataba.

Mhe. Mwenyekiti, naamini wazi *it doesn't do any harm* kama tutaongeza kipengele hiki ingawaje Mwanasheria Mkuu amejipanga kupinga, lakini sifikirii kama anachokipinga kitakuwa kina usahihi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuuliza. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate muongozo kwanza nina hoja nyingi katika sehemu hii niseme zote au niseme nikae, niseme nikae.

Mhe. Mwenyekiti: Sema moja moja Mheshimiwa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kifungu cha 19(2) nilieleza hoja yangu kwamba kifungu hiki kinaipa Bodi mamlaka kuteua wakuu wa idara na vitengo. Sasa hoja yangu ilikuwa kwamba Mhe. Mwenyekiti bodi zetu tunajua jinsi ya muundo wake unavyokuwa na bodi inatokana na wajumbe mbali mbali kutoka nje ya ile sehemu yenyewe husika, anaweza akatoka sehemu nyengine, sehemu nyengine. Sasa hawa wajumbe wa bodi watajuaje kwamba *staff* huyu na *staff* huyu ndio wako *effective* kuwa

wakuu wa idara, kwa nini utaratibu ule ule usitumike kwamba *Managing Director* ndio achague wakuu wa idara badala ya kuipa *power* Bodi kuchagua wakuu wa idara.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Wanu hoja yake ambayo anaijenga, lakini Mhe. Mwenyekiti kama ambavyo tumekuwa tukilizungumza suala hili muda mrefu, kama bodi hizi za mashirika ndio zinafanya kazi kama Tume za Utumishi kwenye yale mashirika. Sasa moja ya wajibu ambayo tume hizi na bodi hizi zimepewa ni pamoja na kazi za kuajiri, kazi za kuchukua hatua lakini pia kazi za kupanga *scheme of service* katika maeneo ambayo wanayasimamia. Sasa huwezi ukaiondoa kazi ya bodi ambayo imeelezwa kwenye sheria Nam. 2 ya Mitaji ya Umma ya 2002 na ukampa Mkurugenzi Mkuu, kwa sababu kwenye sheria ile ile ndio sheria mama ambayo imetoa miongozo ya jinsi gani mashirika haya na bodi ifanye kazi zake. Kwa hiyo, hizi ni kazi ambazo zimepewa *specific* kwa bodi, na huwezi ukazitoa kwenye bodi ukampa mtu mwengine, kwa sababu hata huyu Mkurugenzi Mkuu yeye anawajibika kwa hiyo bodi wenyewe. Nimeiona hoja ya Mhe. Wanu lakini majibu yake ni hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii naona washereheshaji wengi. Nilikuwa nataka kusema kwamba inapokuja sheria ya utumishi na kazi za bodi ipi ina-*prevail* Sheria ya Utumishi au kazi za bodi. Maana sheria ya utumishi ndio imetoa mamlaka kwa Tume ya Utumishi kuajiri na kufanya yote ambayo Mwanasheria Mkuu anasema. Sasa nataka kujua kipi kina-*prevail*, ni sheria ya utumishi ama ni kazi ambazo bodi inapangiwa kufanya.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ukisoma ile Sheria ya Utumishi wa Umma imeeleza aina ya Tume za utumishi ambazo zipo. Imetaja tume hizi za utumishi ya serikali ambayo inasimamia mawizara na taasisi hizi nyengine ambazo hazina mfumo wa kibodi. Kwa hiyo, taasisi hizi nyengine zote za kiwizara zinasimamiwa na Tume ya Utumishi Serikalini. Halafu imetaja Tume ya Utumishi ya Baraza, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na tume nyengine, lakini sheria ile ile ikatambua kuwepo kwa bodi za wakurugenzi. Ukisoma sheria ile ile imetambua kuwepo kwa bodi za wakurugenzi kama bodi zile kwenye mashirika zinafanya kazi sawa na zinafanya kazi tume za utumishi.

Kwa hiyo, wao wajibu waliopewa kisheria ni kushughulikia mambo ya utumishi kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, wao hawaendi kwenye Tume ya Utumishi Serikalini mambo yao yanapotoka kwenye bodi yanakwenda kwenye

Kamisheni ya Utumishi wa Umma moja kwa moja, kwa sababu ndio jukumu ambalo limepewa kwa sheria ile.

Sasa nimuhakikishie Mhe. Wanu kama Tume ya Utumishi ya Serikali haisimamii mabodi haya yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria, lakini bodi zenyewe vile vile zinafanya kazi kama tume katika maeneo yao ambayo wamepewa mamlaka na sheria zao. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nimemfahamu kidogo Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini nilikuwa nataka nitahadharishe tu serikali kwamba wanavyoweka sheria moja isimamie kitu fulani halafu mkaenda kuwapa *power* wengine kufanya kazi ambayo sheria imewekwa ipo na ina-*regulate* yale mambo ambayo wamepangiwa wale watu wengine inakuwa kama wanaweka *double standards.* Kwa hiyo, ni vizuri wakawa na kitu kimoja ambacho kinaongoza kwa utumishi wote.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza nimeghumiwa kwa sababu hiki ninakwenda kwenye vifungu lakini viko vingi sasa nitajaribu nataka ushauri wako…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nilipoingia hapa mwanzo nadhani utakuwa umechelewa kidogo…

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Aah! Nimesikia kila kitu, nilikuwa nakusikiliza Mheshimiwa nilikuwa naomba tu kama…

Mhe. Mwenyekiti: Changia *specific* kifungu kimoja halafu baadae tutakupa nafasi kwa kifungu…

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Kwa nia njema kabisa tutakwenda katika hiyo sehemu kidogo kidogo ili tuweze kuangalia vizuri. Ahsante nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kazi ya kuendesha niachie mimi tu hapa.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo kazi ya kuendesha niachie mimi wewe fanya hiyo yako wewe tu.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Kabisa mkuu, ahsante *no problem*, ahsante mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha Kiingereza Nam. 29(1) hapa nili-*suggest* kwamba kwenye ule mstari wa mwisho nilisema kwamba baada ya kuweka *in accordance with accepted accounting principles* badala yake isomeke *in accordance with the laws of Revolutionary Government of Zanzibar.*

Halafu kwenye kifungu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukiseme kwa Kiswahili hicho kifungu, yaani hayo marekebisho tunayoyafanya yawe kwa Kiswahili.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Sasa huku tuna sheria mbili tumepewa Mwenyekiti mimi najaribu kuweka sawa yote.

Mhe. Mwenyekiti: Imepitishwa na ya Kiswahili Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante, ngoja basi nifungue na hii kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu Nam. 29 inaposema Mkurugenzi Mwendeshaji atawezesha kuweka vitalu vya hesabu vya kumbukumbu za miamala ya kifedha kwa kuzingatia misingi ya hesabu inayokubalika. Sasa hapa ukiangalia kwa mujibu wa sheria hii nilishauri iwe ni kutokana na sheria ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Halafu ukiangalia kwa kifungu hicho hicho 29(3) ambacho kinazungumzia taarifa za hesabu *the statement of accounts shall include*, lakini huku inasema taarifa za hesabu zitajumuisha. Sasa mimi nashauri hapa baada ya kuweka zitajumuisha taarifa za hesabu zitajumuisha na zitawekwa kwa utaratibu kwa mujibu wa sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hiyo moja tunakwenda kidogo kidogo.

Halafu kwenye kifungu cha 32 suala la zabuni…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umeingia kifungu chengine tuta-*deal* na cha 29 tu kwanza.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Kwanza eeh, haya sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Tatizo lako ni nini?

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria sijui kama umemuelewa Mhe. Simai.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nimeelewa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hoja ya Mhe. Simai ni kwamba tuongeze maneno ya sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mimi nafikiri anayo hoja lakini nadhani sahihi ni vyema tungeweka kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na sheria ya fedha za umma. Nadhani tukifanya hivyo kwa sababu ile ndio sheria ambayo inayoongoza matumizi yote ya hesabu za umma serikalini. Sasa tukifanya hivyo nadhani ile haja ambayo ameielezea itakuwa imeshakidhi kuliko kutaja sheria, lakini sheria ipo na sheria yenyewe ni sheria ya fedha za umma. Kwa hiyo, tukitaja hivyo nadhani haja yake itakuwa imeshatimia.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mwenyekiti, mimi ningependa nione kidogo kama naweza kumsaidia Mhe. Mwanasheria kama tafsiri hiyo itakuwa ni vizuri inaingia hapo. Kama itakuwa kwa mujibu wa sheria za umma ambazo tunaiweza tukaitaja hiyo sheria labda. Naona tuendelee kama ameshaweka hapo sawa basi haina shida.

Mhe. Mwenyekiti: *AG* kimsingi amekubaliana na wewe lakini amekupa tafsiri sahihi, maneno sahihi ameshayaweka kwa hiyo pamoja na mabadiliko tutahoji.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Nimemuelewa.

Mhe. Mwenyekiti: Pamoja na mabadiliko tutahoji.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mkuu nimesikia naomba niendelee kifungu chengine.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana nitakupa tena nafasi.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Haya ahsante.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi lakini kwa bahati mbaya alighafilika Mhe. Waziri hakunitaja

jina langu. Lakini nashukuru alinikumbuka baadae aka- *acknowledge* kweli nimechangia kimaandishi, namshukuru sana.

Sasa hoja yangu iko kwenye kifungu cha 8 na 32 kwa pamoja. Kifungu cha 8 kinazungumzia kazi na wajibu wa mamlaka pamoja na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia 32 kwa pamoja hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumza kwamba ukiangalia sana undani wa hizi kazi za mamlaka na kampuni zinaingiliana zote husimamia uchimbaji na tafutaji. Sasa nilitaka kujua tu nani yuko *higher in authority*, huyu *ZPDC* yaani kampuni au mamlaka, kwa sababu hizi kazi naona zinaingiliana na wote wametoa *room* ya kusimamia nani sasa bosi wa mwenzake? Nataka kufahamu hivyo Mhe. Waziri atuweke sawa kidogo hapo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru mamlaka ndio *regulator*, mamlaka ndio anawa-*regulate* hawa wote wanaokuja kuomba leseni. Lakini kifungu cha 32 kwanza hata hazikuwekwa kazi za kampuni, lakini ukisoma kifungu cha 32(5) kazi kubwa ya kampuni hii ni kufanya biashara na kulinda maslahi ya taifa katika shughuli za mafuta na gesi asilia. Kwa hiyo, kazi ya kampuni ni kufanya biashara kwa niaba ya serikali kwenye sekta hii ya gesi na mafuta na kazi ya mamlaka ni ku-*regulate* na kutoa miongozo kwa wale wote ambao sasa wanataka kuomba kupewa leseni, lakini baada ya kupewa leseni husimamia utekelezaji wa zile kazi zao. Kwa hiyo, ni vitu viwili tofauti Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniona nina hoja ukurasa wa 78 kwenye kifungu cha 21 na 31(3). Lakini kwanza niendelee kwenye 21 pana kinga kwa wajumbe wa bodi na maafisa wa mamlaka.

Wakati nikichangia nimesema hakuna haja ya kuwawekea watu kinga, kinga ninafahamu anaweza kuwekewa daktari kwenye kazi yake wakati anafanya *operation* au vyenginevyo, lakini hatuwezi mtu tunamuwekea kinga tunampa rasilimali yetu kubwa tukamuwekea kinga, chochote kinaweza kikafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nataka hapa kidogo maelezo au tukifute kifungu hiki neno kinga hatuwezi kuweka, kwa nia njema kinga gani ndio nia njema. Kinga gani ndio nia njema? Kwa sababu nilisema hata *jahannam* iko kwa nia njema tu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Dimwa alipokuwa Naibu Waziri angetusaidia kule kusema haya na tungeyatoa kule ingekuwa vizuri maana yeye katika waliopika chungu hiki na yeye pia alikuwemo. Lakini niseme tu Mhe. Mwenyekiti, kama huu ni utaratibu ambao tunauandika kwenye sheria nyingi, na hasa unapotoa dhamana kubwa na pana kama hizi ambazo zinabeba *interest* ya nchi nzima. Kama lazima uwape kinga wale ambao wanasimamia *interest* hizi kwa niaba ya nchi, kama inawezekana wakafanya mambo kwa nia njema lakini ikaonekana katika utendaji wao kwamba jambo lile lilikuwa limeleta sintofahamu lakini walilifanya kwa nia njema, na maneno haya nia njema tayari tumeshasema mara nyingi kama yana tafsiri yake. Kama *malafide* Mhe. Gavu anapenda kutumia na *bonafide* tayari haya ni maneno ambayo yana tafsiri yake. Sasa ukishaweka tu neno hili yule ambaye anatakiwa kutafsiri sheria anajua sasa ni kwa kipimo gani apime ajue kama jambo hili kweli lilifanywa kwa nia njema, au jambo hili kweli halikufanywa kwa nia njema, lakini hatua itachukuliwa baada ya kuweka kila kipimo cha nia njema yenyewe Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana ndugu yangu Mwanasheria Mkuu juu ya maneno yake aliyosema, lakini bado naendelea kusimamia hoja yangu tunaweza tukasema nia njema. Lakini ipo nia njema ya kuelekea *jahannam*, sasa je tutakuwa tuna uwezo gani wa kumjua huyu mtu anafanya nia njema, hata akituibia kuna mengine lugha Mhe. Hassan *Diaspora* anasema mengine mijizi, hata hiyo ujizi inaweza kuwa nia njema tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kinga ipo na hii kinga imewekwa iwapo inatokea tatizo wakati yule mjumbe anatekeleza jukumu lake, lakini kinga ile ukisoma vifungu vya chini unaona kabisa haimzuii kushtaki au kushtakiwa kwani nini? Kwa sababu kama binadamu anaweza kuwa na mapungufu yake na ndio maana kwamba kinga ipo lakini kinga ile sio anapofanya kitu ambacho sicho pia na yeye anaweza kushtakiwa. Lakini pia kinga inaweza kumlinda wakati anafanya majukumu yake ya kazi kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwa hili tuendelee nakwenda na hoja yangu ya pili ya hapo hapo niliyoitaja mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti: Subiri Mheshimiwa nitakupa tena baadae.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, mjumbe aliyepita alinifilisi kwa sababu nilikamata sana kifungu hiki naomba tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, bado natetea hoja yangu kutokana na utafiti nilioufanya kwamba nchi nyingi za Kiafrika tunaingia matatani katika mikataba. Kwa hivyo, bado nasema miongoni mwa kazi…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tumeshakimaliza hicho huwezi kurudi tena, naomba mpishe Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi mimi nasimamia hicho hicho kifungu cha 22(1).

Mimi katika mchango wangu wakati nilipokuwa nikichangia nilikisoma kifungu hicho na nikataka kwamba kirekebishwe kiongezwe maneno kidogo. Kinasomeka:

"Kwa mujibu wa Sheria hii, mtu ambaye ni mjumbe wa Bodi au mfanyakazi wa Mamlaka hatotoa taarifa yoyote ambayo ameipata katika utendaji wa kazi yake".

Sasa mimi nikauliza hata kama mtu kapata taarifa ya hujuma ya kampuni isitolewe siri hiyo. Kwa hiyo, mimi nikapendekeza kwamba kwa hapo iongezwe neno isipokuwa yashushwe maneno mawili au moja ya kuonesha kwamba iwapo itapatikana taarifa ya ubadhirifu wa aina yoyote, siri hiyo iweze kutolewa ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua za haraka kabla tatizo halijakuwa. Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza dhamira ya kifungu hiki ni kwamba kutoa angalizo kwa wale ambao wamepewa majukumu ya kusimamia kazi hizi, ikiwemo Bodi na ikiwemo wafanyakazi kama katika utekelezaji wa kazi zao wanapokea na kupitia taarifa nyingi ambazo ni za watu. Na ukisoma sheria hii imetoa kinga za taarifa hizo, kama taarifa hizi za watu Mhe. Mwenyekiti hazitakiwi zitolewe ila kwa utaratibu maalumu ambao umewekwa kisheria.

Sasa hapa sheria hii inatoa angalizo kwa wale ambao wanafanya, kama yeyote atakuja atakayetoa siri hizo basi kuna kifungu hata cha adhabu wamewekewa kama watachukuliwa hatua. Sasa dhamira ya kifungu hiki ni kama kutoa taarifa hizi nje ya mamlaka yao ya kazi, lakini kwa ndani mambo haya tunafanya una-*share* na mwenzako unazungumza naye, lakini nje ya utaratibu ule mzima wa kazi kama wewe umepata taarifa lakini unakwenda kumnong'oneza mtu

mwengine, unamwambia ah, mwenzio fulani kaja hapa ana hiki, ana hiki na hiki, hizo ndio taarifa ambazo zimekatazwa zisije kutolewa.

Kwa hivyo, sheria hii imeweka kinga kabisa kwa wale Wajumbe wa Bodi ambao ndio watakuwa wanapokea hizi taarifa, lakini kwa wafanyakazi wengine ambao watakuwa wanafanya kazi kwa niaba ya bodi na kwa niaba ya mamlaka pia, kwamba wajue watapokwenda kinyume na kuanza kutoa siri basi kuna kifungu cha adhabu ambacho kitawakumba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini bado mimi nina wasiwasi juu ya jambo hili. Kwa sababu amesema kwamba siri zibakie ndani lakini kwenye hiki kipengele amesema yoyote, kuna neno 'yoyote' ina maana iwe ya ndani iwe ya nje. Kwa hiyo, mimi nafikiria ili kuliweka sawa hili jambo lisije likaleta utata ni vizuri ilikuwa hayo anayoyazungumza yaainishwe kwamba isipokuwa kwa ndani, nje au mambo mengine. Mimi nasema tuendelee lakini naona hapo ilikuwa ni vizuri hilo neno na busara itumike. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Simai Mohammed Said anachangia ulimkataza asizungumze kwenye *version* ya *English*, lakini Mhe. Mwenyekiti, *version* zote tumepatiwa na *version* ya *English* pia ina marekebisho ambayo ndio Mhe. Rais anakwenda ku-*sign*. Sasa kifungu changu kinachofuata kinahusiana na marekebisho kwenye *English Version* kama utaniruhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu Hafidh Ameir mjadala utakuwa kwa Kiswahili na tutarekebisha Kiswahili, ya Kiingereza naomba muiache, irekebisheni kwenye Kiswahili. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Bado nina hoja nyengine naweza kuendelea au vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio unaweza kuendelea.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu nyengine ni kwamba kulikuwa kuna *formatting* nilikuwa nataka kurekebisha kidogo katika hii *version* ya Kiswahili, sio lazima lakini kama serikali itapendezwa nilikuwa naona kwamba, kwa sababu sheria inazungumzia kuhusu *Managing Director* kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, napata tabu kuzungumza kwa sababu nilitumia *English Version*. Kwa hiyo, naomba tuendelee nijiweke sawa hoja nyengine itakapokuja nitakuwa nimeshakaa tayari.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu ipo katika kifungu Nam. 30(2) ambacho kinakwenda sambamba na 31(1), ambacho kinataka hesabu ziwasilishwe kwa *CAG* miezi mitatu baada ya mwaka kumaliza. Lakini pia inataka Bodi ya Wakurugenzi kuwasilisha taarifa za mwaka ambazo ni *Annual Reports* katika kipindi cha miezi minne baada ya mwaka kumaliza.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ina maana kuwa *CAG* ana muda chini ya mwezi mmoja kukamilisha, na ukiangalia hapa kwa kawaida *CAG* anahitaji kutoa taarifa zake ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea hii hesabu. Sasa mimi nashauri muda muafaka katika hapa wa bodi kupeleka taarifa yao inatakiwa miezi saba baada ya mwaka kumaliza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sikumfahamu Mhe. Simai Mohammed Said hoja yake, kwa sababu vifungu hivi ni *standard* kwenye sheria ya fedha. Kama tunavyojua baada au kabla ya mwisho wa mwaka inatakiwa upeleke ripoti yako. Kwa mfano, kipindi hiki tumeshamaliza mwaka wa fedha uliopita, kwa hiyo kabla ya tarehe 30 Septemba lazima ripoti zetu ziwe zimeshawasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sasa hivi ni vifungu ambavyo vimo kwenye sheria hatuwezi tukarekebisha, sheria mama yenyewe ndio inasema hivi, na ndio utaratibu uliokuwepo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, hoja ninayo lakini kama anasema itabidi na sheria nyengine hivyo basi tuendelee kwa kifungu hiki.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia nilichangia kifungu cha 31(3) kinasema kama ilivyo: "Waziri ndani ya miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya mwaka ataiwasilisha taarifa hiyo katika Baraza la Wawakilishi pamoja na taarifa nyengine ambazo ataona inafaa".

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko hapa, hizo nyengine hazijawahi kuletwa tangu Baraza hili lianze. Sasa na hii tena vile vile italetwa. Mimi ningeomba tuifute kabisa iwe haipo ili serikali ijiweke sawa isilete kabisa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu ndugu yangu Mhe. Mohammed Said Mohammed, nadhani kama uamuzi wake ni huo na ile hoja yake binafsi angeifuta. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini huu ndio utaratibu kwamba lazima ikifika mwisho wa siku taarifa ziletwe kwenye chombo hiki, kama kujadiliwa zijadiliwe ndio utaratibu ulivyo. Sasa kama hazikuwahi kuletwa na zinaletwa tu kwa utaratibu mwengine, zinaletwa kwenye hesabu za serikali, kwenye ripoti za *CAG*. Sasa utaratibu wa kuleta upo na kanuni imeelekeza vizuri juu ya namna ya kuwasilisha ripoti hizi. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mwanasheria Mkuu na ni mtu ambaye msomi amebobea, lakini anashindwa kuzijua kanuni au kuziona Kanuni za Baraza la Wawakilishi, anasema zinaletwa. Kweli zinaletwa lakini hazikidhi haja na tunachotakiwa tusipigane mchanga wa macho, kitu kikubwa kama hiki ambacho hapa tunakijadili kwa maslahi ya nchi hii mimi naomba tukiondoe tu kwa nia njema ile aliyosema hata ya kuelekea *jahannam*,tuondoe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi ningeshauri kibaki na hoja yako kwa namna unavyoileta najua kuna hoja ambayo inakuja baadae kwenye shughuli za Baraza, ambayo sasa itataka wale wote ambao hawaleti pia warejeshe. Sasa mimi nadhani tusingeendelea huko.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na wewe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Yangu mimi ni 31(3). Katika *schedule of amendment* yangu nimependekeza, naomba kuisoma. "Waziri ndani ya miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya mwaka ataiwasilisha taarifa hiyo katika Baraza la Wawakilishi pamoja na taarifa nyengine kama bodi itakavyoona inafaa", imemalizia hapo. Mimi nimependekeza iongezwe "kwa ajili ya kujadiliwa". Kwa sababu anaweza kuwasilisha, *what for*, nimependekeza hivyo kwa ajili ya kujadiliwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimefahamu hoja yake ni nzuri ina mantiki lakini mambo haya yameachiwa kanuni, Kanuni za Baraza ndio zina-*govern* utaratibu wa kuleta ripoti ipi inajadiliwa ipi haijadiliwi, huu ni utaratibu wa kikanuni. Sasa kama yeye anaona kanuni haijakidhi haja juu ya utaratibu wa kuwasilisha hizo ripoti sawa, lakini sisi mawazo yetu ni kwamba tayari Kanuni za Baraza zimesha-*provide* utaratibu mzuri wa kuwasilisha hizo

ripoti za serikali na utaratibu wa kujadiliwa na kuchangiwa ndani ya Baraza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu amebobea kisheria, inatuongoza katiba, sheria, kanuni, hapa tunatunga sheria.

Nashukuru kwamba ameona inafaa na inapendeza, kwa hivyo, ningeomba iongezwe "kwa ajili ya kujadiliwa". Kwa sababu hii ni sheria tunayoitunga kwa manufaa ya wakwezi na wakulima.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Imekubaliwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi niko katika kifungu Nam. 32 ambavyo vinazungumzia masuala ya zabuni. Kwenye hiyo sheria hapo haijatoa uwezo wa kuwa waziri au mamlaka kuomba taarifa zaidi ya waombaji wa vitalu kama zinahitajika kwenye uamuzi wa zabuni. Pia ukiangalia kampuni zinazoomba vitalu ni muhimu zifanyiwe ukaguzi wa kutosha kuliko wao kuleta taarifa za kwenye zabuni wanazozileta. Lakini ukiangalia kwenye sheria ya Jamhuri kifungu Nam. 49 kimewekwa, sasa hapa naona pako kimya naomba kidogo ningepata maelezo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sikumsikia kifungu chake ambacho anakijengea hoja, labda nimuombe arudie kile kifungu ili nijue kifungu gani.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu cha 32.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kifungu cha 32, nimuombe arudie hoja yake ili nipate kumjibu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia hiki kifungu Nam. 32 kwa ujumla kina maeneo matano, kinazungumzia masuala ya pamoja yote kwa wazabuni. Lakini ninachokisema hapa kwamba nilipochangia nilizungumzia juu ya kifungu hiki kwamba katika sheria ya Jamhuri nafikiri Mwanasheria Mkuu alikwenda kusali jana nilipochangia, alinambia alikuwa hayupo. Sasa hapa ndipo tunapokuja kubanana, naona ametaja wengi lakini mimi ya kwangu hajayafanyia kazi ndio maana tunakuja kushikana hapa sasa.

Mimi nilizungumzia katika vifungu vitano vilivyotajwa hapa, lakini ukiangalia kama tutategemea taarifa ya mwekezaji anapoleta *proposal* kwa kutegemea kwenye makaratasi lakini hatumjui, zipo kampuni tayari tunazijua zimeshaanza sasa hivi utaratibu wa kuzungumza na serikali. Lakini ukiangalia nyuma pengine hazina hata historia ya kuchimba mafuta, hatumjui mtu katoka wapi, sasa ndio maana katika maeneo hapa kwamba tuongeze kifungu kimoja kidogo ambacho kitaweza kumpa waziri au mamlaka kuweza kufanya upekuzi wa kutosha ili kuzijua hizo kampuni zinazofanya haya masuala ya uchimbaji mafuta na gesi ili waweze kupata taarifa zao zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, alipokuja waziri kwa sababu hiki ni kifungu muhimu sana, kwa sababu safari yote inaanzia hapa, lakini muombaji anapokuja kama humjui ni sawa sawa na mtu kama mtumishi anakuja anagonga mlango nyumbani kwako anakwambia mimi mwananchi wako naomba unisaidie. Sasa utathibitisha vipi? Hii ni sawa sawa hapa tunarusha mkuki kizani.

Mimi nashauri hapa patafutwe njia paongezwe maneno ambayo mamlaka itapewa nguvu kwa kushauriana pamoja na waziri ili kupata taarifa zaidi za hizi kampuni ambazo zinaweza kuleta zabuni zao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Simai Mohammed Said anazungumzia kifungu cha 32 au kifungu gani chengine cha 32? Kwa sababu ukisoma kifungu cha 51 ndio kinaweka sasa utaratibu wa utoaji wa leseni na ukisoma masharti yake yako vizuri, yameelezwa vizuri tu.

Kwanza atawasilisha mapendekezo ya kazi lakini taarifa ya utaalamu na sifa ya sekta ya mafuta, taarifa ya utaalamu na rasilimali ya sekta ya mafuta na gesi asilia zilizopo, taarifa aina ya rasilimali ya fedha zilizopo kwa muombaji zikijumuisha mtaji, miundombinu, dhamana, mambo mengi yameelezwa. Sasa mimi sina hakika Mhe. Simai Mohammed anajenga hoja yake kwenye kifungu gani. Kwa sababu kama utaratibu wa kumjua muombaji utamjua wakati analeta yale maombi yake, na maombi yameanza kuelezwa kwenye kifungu cha 51.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwanasheria Mkuu ana hoja naomba tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nije katika kifungu cha 32 ambacho kinazungumzia wale Wajumbe wa Kampuni ya *ZPDC*.

Ukisoma kifungu hiki hii ni kampuni muhimu *Scottish Gas and Oil Company* wajumbe wake imewawekea sifa zao wawe na sifa hizo kwa sababu wao ndio watakwenda kufanya kazi na kampuni ya kigeni, lazima wawe na uzoefu, wawe na elimu, taaluma, kwa sababu wawekezaji wa kigeni wengi wao wanakuwa ni wajanja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa humu hamna sifa. Kwa hivyo, nilikuwa nimependekeza wajumbe hawa wawe na sifa kama za wajumbe wa bodi ambao sifa zao iwe 15(3) lazima wapewe, kwa sababu hawa ndio kila kitu, si mamlaka wala si bodi, wajumbe hawa Mheshimiwa ndio watakaoweza kutuvusha au kutukwamisha. Kwa sababu wao ndio wanaokwenda kufanya biashara na kampuni ya kigeni. Nilikuwa naomba wajumbe hawa wasiwe watu tu, wawe watu wenye sifa na sifa zake nilizozipendekeza kama kifungu cha 15(3) sifa za Wajumbe wa Bodi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba, maana yake napata shida kidogo kwa sababu kifungu cha 32 ukikisoma kinazungumzia Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia. Sasa swali haliingii moja kwa moja kwenye kifungu. Kwa hiyo, napata shida kidogo labda Mjumbe angeweza kusema kile alichokusudia, lakini kwenye hii ya 32(1) mpaka (5) haizungumzii hicho ambacho anakizungumzia.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwa macho yangu mimi kifungu cha 32 kinazungumzia kuanzishwa kwa kampuni ya maendeleo ya mafuta na gesi asilia Zanzibar.

Hoja yangu hawa wajumbe wa kampuni hawa wafanya kazi ndani ya kampuni wawe na sifa, mambo mangapi yaliyowekwa hapa, mambo manne mpaka matano haijataja sifa za wajumbe hawa, wawekewe sifa kama kifungu cha 15(3); awe Mzanzibari, awe na elimu, awe na hiki na hiki huyu ndiye anayekwenda kufanya kazi na kampuni ya kigeni ambayo imesomea ghilba na kuwadhulumu Waafrika.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndio hoja yangu na iko *very clearly* katika kifungu cha 32 hamna sifa mna vifungu vidogo moja mpaka tano lakini hawa hawajawekewa sifa. Kwenye mamlaka wamewekewa sifa, kwenye bodi wamewekewa sifa hawa wanaokwenda kufanya kazi na kampuni, watafutwe watu tu waje kufanya kazi, haiwezekani!

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kuunda kampuni ni utaratibu wa kisheria ambao unaongozwa na sheria ya makampuni. Huo ndio

utaratibu wa kuanzisha kampuni yoyote, kama lazima kwanza ukaisome *Companies Act* inaeleza nini, utaratibu wake ukoje, nani anaweza kuwa *shareholder* na nani anaweza kuwa *director*. Sasa sidhani kama Mhe. Hassan Khamis amesoma ile sheria na ndio maana hapa hakikuelezwa kitu, imeelezwa kwamba utaratibu wa kuanzishwa utafuata sheria ya makampuni ambayo ndio imetaja utaratibu wake mzima. Hii ni taasisi ya kibiashara ina utaratibu wake wa kuajiri, ina utaratibu wake wa idadi ya *board of directors* ambayo itakuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa nadhani haitokuwa muafaka tukianza kujadili sifa za Wajumbe ambao sheria yake inayoongoza mambo haya ni sheria ya makampuni na ndio maana tumesema kwamba kampuni hii itasajiliwa kwa kufuata sheria ya makampuni ambayo ipo. Sasa hoja ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh sidhani kama hapa ina- *hold any water* kama ambavyo yeye mwenyewe anaisimamia.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini akumbuke kwamba leo Wazanzibari tangu mimi nazaliwa nasikia mafuta na gesi yapo, hayapo, vitalu Bububu, leo tunapitisha sheria muhimu; wako waliosema hatuwezi lakini tumeweza. Hii sheria ni sheria ya aina yake ya kimapinduzi, sasa hapa ninachosema ni kulinda mali ya wana Mapinduzi wakwezi na wakulima. Kama Mwanasheria Mkuu anajitoa kuwalindia mali yao fahuwa, lakini ningeona inafaa kwamba kwenye sheria hii maalumu kwa lengo maalumu la Kimapinduzi wakwezi na wakulima lazima Wajumbe hawa katika kusimama mali yao wanaokuja kusimamia mali hii tuwajue ni kina nani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu nimefanya utafiti katika kampuni, *Gas & Oil Companies* za Scotland wajumbe wake wako *clear* wana sifa, Garbon wajumbe wake wanaosimamia *oil and gas* wana sifa, Malawi wana sifa, lakini sijaona kwa nini Zanzibar wajumbe wataokwenda kusimamia mali ya wakwezi na wakulima ambayo ni kampuni wasiwe na sifa.

Mhe. Mwenyekiti, sioni tatizo kuwawekea sifa wajumbe hawa, wala sheria ya kampuni hapa haichukui nafasi. Hii ni sheria ya aina yake hata wewe Mhe. Mwenyekiti, umesema wazi leo tutapitisha kwa sehemu sio kama tulivyozoea. Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nadhani nimemuelewa na nadhani ufafanuzi ambao nimeutoa ndio ambao unakidhi haja iliyokusudiwa. Kama kutaja hizo sifa, kwa sababu unapounda kampuni lazima uwe una *memorandum and*

Articles of Association ya ile kampuni, ile ndio inatoa mwelekeo mzima wa kampuni utafanya kazi gani, nani atakuwa *board of directors*, nani atakuwa *share-holder* wako, nani atakuwa na sifa gani, nani atakuwa na kazi gani; utaratibu wake ni wa kisheria ambao umeelezwa ndani ya sheria husika Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nadhani hapa tumeeleza wazi kama kampuni hii itafuata masharti ya sheria ya makampuni katika uanzishwaji wake. Nashukuru.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaona kama hapa kuna tatizo, lakini sasa leo hatutaki kubishana. Nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu kanifahamu lakini tena ndio Mwanasheria Mkuu. Lakini ni kwamba naamini na yeye yumo katika kulinda mali ya wakwezi na wakulima. Kwa hivyo, kama yeye anataka kuitoa tumuachie yeye. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, langu ni dogo lakini kabla hatujaondoka katika sehemu hii nahisi ni vyema nikaliongelea hapa, kwa sababu mimi nilikwenda kwa maandishi na kwa mawasiliano baina ya mimi na Mhe. Naibu Waziri nilishauri kwamba lugha rasmi ambayo ya matumizi katika mawasiliano ambayo kwenye sheria ya Sudani ya Kusini waliitaja na nikashauri kama itajwe katika sheria. Lakini pia ilikuwa suala sio *sovereign fund*. Kwa hiyo, nilikuwa nataka ufafanuzi katika mambo mawili.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani hicho Mheshimiwa hujataja kifungu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, haya ni katika maelezo ambayo hayakutolewa.

Mhe. Mwenyekiti: Lazima unipe kifungu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Unajua Mhe. Mwenyekiti, tulipoondoka pale mwanzo tuliondoka kwa haraka sana kwenye sehemu ya kwanza, sasa hapa tunaondoka sehemu nyengine muhimu.

Mhe. Mwenyekiti: Tumeshapita hapo Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, basi nilikuwa nashauri, basi ushauri wangu naomba uchukuliwe.

Mhe. Mwenyekiti: Sio pahali pake hapa Mheshimiwa. Katibu tuendelee.

Sehemu ya Tatu

Mamlaka ya Udhibiti (Utafutaji na Uchimbaji) wa Mafuta na Gesi Asilia na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia

Kuanzia kifungu cha 7 hadi cha 32 pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne

Shughuli za Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Kuanzia kifungu cha 33 hadi 109 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu nilizungumza kifungu 33 (3) pamoja na mbembwe za Uwakilishi wa Mwanasheria Mkuu kuja kutunasibisha *Latham Island* ilikuwa mwaka vipi, nafikiri hata mtendaji mkuu wa shughuli za serikali alitoa maelekezo kwamba tupatiwe ramani halisi ya Zanzibar.

Naomba tupatiwe ramani halisi ya hivi vitalu ili tuweze kujua kipi tunachoenda kukifanyia kazi. Hilo sijapata majibu yake Mheshimiwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Abdalla Diwani ampitishie kwanza Mhe. Waziri hii sheria yake. Kwa sababu sheria hii ndio imetoa sasa utaratibu kwa waziri na kwenda sasa kugawa haya maeneo. Sasa mpitishie kwanza halafu akagawe uje umuulize, lakini sasa hivi hujampitishia unamwambia akupe ramani ya hayo maeneo tutakuwa nayo wapi.

Mimi nimuombe Mhe. Abdalla Diwani ampitishie kwanza Mhe. Waziri hii sheria yake kwa sababu kwenye vifungu huku vya nyuma moja ya kazi ambayo Mhe. Waziri amepewa ni kutayarisha sasa hizo ramani ya ma- *blocks*, sasa tumpitishie kwanza ili sasa akafanye ile kazi ambayo inatakiwa kufanywa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na yeye Mhe. Mwanasheria Mkuu nafikiri sisi sote hapa tumeshashona, huwezi kutoa mshono wa kanzu au suruali kabla ya kuwa na kitambaa. Kwa hiyo, sisi tayari tunataka kushona kitambaa tunacho sasa inakuwaje tusipate hizo taarifa mapema. Sasa nafikiri tungeambiwa tu hakuna lolote kutoka Kaskazini Zanzibar mpaka hapa meli fulani tukawa tunafahamu hicho baadae mbele tutasubiri mengine.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani, sawa, sikutaka kusema mengi pale awali. Lakini nimuhakikishie kwamba kabla ya utaratibu huu ambao tunaufanya sasa hivi kisheria mambo haya yalikuwa yakishughulikiwa na *TPDC*, sote tunajua kama wao ndio walikuwa na mamlaka ya kuyashughulikia mambo hayo na wao pia walipewa mamlaka ya kugawa ma-*block* ambayo sasa hivi yapo wanapozungumzia ma-*block* 1,10,12 haya yaligaiwa na *TPDC*.

Sasa hivi sisi tunasema kwa mujibu wa mamlaka ambayo tunampa Mhe. Waziri kwa sheria hii na yeye atakuwa na nafasi ya kuweza sasa kuyapitia yale ambayo tayari yameshagaiwa na *TPDC*. Sasa hii ndio kazi ambayo tunafanya kama tumpe halafu sasa tukayapitie yale ambayo sasa kwenye maeneo yetu na yale ambayo hayapo kwenye maeneo yetu awaachie wengine waendelee na kazi zao, ndio jawabu sahihi Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mipaka aliyozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba iko chini ya himaya ya *TPDC*, sisi ni ndugu nafikiria kama nilivyofahamu hizo tulikuwa hatuna uwezo huo sisi, tulikuwa tunataka kupitisha sheria. Nafikiri hakuna ubaya hata hivyo basi tukajulishwa kidogo tu angalau tukapata muono wapi tunapotaka kwenda, tukumbuke kwamba tulikaa nyuma sisi sote ni mashahidi na tukaambiwa kwamba kabla ya kuja kusomwa mswada huu tutapewa ramani nafikiri sote humu ni mashahidi. Sasa inakuwaje inakuwa gumu hili suala.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Kifungu cha 35 (1) kinasema kwamba:

"Mtu aliyekusudia kufanya utafiti wa awali ataomba kwa mamlaka kibali cha kufanya utafiti huo"

Naomba niende kidogo kidogo natumia Kiswahili. Kwa nilivyofahamu sheria hii kwamba *power* ya hii *up streaming* ipo kwa waziri. Lakini *survey permit* ambayo kile kibali cha awali kinaombwa kwa mamlaka ya mafuta. Nilikuwa nataka kujua hii ikoje, unajua kwamba *Minister* ndio ana ile *power* ya utafutaji na uchimbaji. Lakini kibali kiombe kwa Mamlaka ya mafuta. Nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo hapo ili tupishe sheria yetu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambayo Mhe. Wanu Hafidh amesema kama ukisoma sheria hii kila eneo limepewa kazi yake na wajibu wake. Waziri amepewa maeneo yake na mamlaka pia imepewa maeneo yake. Hapa tunapozungumzia ni ule utafiti wa awali kama mtu anapokuja sasa

anataka kuomba kibali cha kufanya utafiti wa awali ajue huko ndani kwenu kuna kitu gani hii ndiyo leseni ambayo inazungumziwa.

Sasa ukisoma kifungu hichi kwamba inavyotakiwa kwa hapa kama lazima aombe kwa mamlaka kwa sababu hii haimruhusu hata kama akigundua inabidi sasa aje arudi tena kuomba leseni nyengine sasa ya operesheni. Sasa kama kilivyo ni sahihi kama anatakiwa kwanza aombe kwa mamlaka kabla sasa ya kuomba kwa waziri baada ya kugundua kilichokuwepo na akataka sasa kupewa leseni inabidi aanze huko. Sasa kama kilivyo ni sahihi Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mwanasheria Mkuu lakini nilikuwa nataka aniweke sawa kidogo kwamba utafiti wa kwanza unaombwa kwa *authority* kabla ya kujua kuna kitu gani, anamaanisha kwamba tayari ikigundulikana yule ambaye anakuja kuchimba anatakiwa aombe kwa waziri kama ndio hivyo nilivyomfahamu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ni sawa sawa kibali kinatoka kwa mamlaka kwa ule utafiti wa awali, halafu waziri anatoa leseni wakati wale wameshafanya utafiti ambao mamlaka na wakati wowote kama utasoma sheria hii vizuri utaona kabisa kwamba hii sheria inakwenda kwa mtiririko, kwa sababu pia mamlaka ina wajibu ya kushauri. Tunashauriana tutakuwa tunafanya kazi kwa pamoja kwa leo yanayohitaji msaada. Lakini kawaida katika sheria hii kibali kinatoka kwa mamlaka na waziri anaendelea kutoa leseni.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, waziri alipozungumza ndipo aliponigusa kwamba mimi ninachofahamu haya mamlaka ina kazi ya kumshauri tu waziri. Sasa nikawa nashangaa kwamba sasa watu wanapokuja wakaombe kibali kwa *authority* wakati wao kazi yao ni kumshauri tu waziri. Lakini maelezo ya mwanzo ya Mhe. Waziri nimemfahamu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, katika *schedule of amendment* ilikuwa ina kifungu 51 na 59 kimantiki ilikuwa na lengo moja.

Mhe. Mwenyekiti, si siri baadhi ya watendaji na Waheshimiwa katika nchi za Kiafrika ikiwemo Zanzibar si waaminifu, nchi hii hii Zanzibar tumeshuhudia watu wamenunua majenereta watu wamegharamika mabilioni ya pesa yako pale Mtoni leo hii yanaoza kwa sababu ya 10%, si siri.

Mhe. Mwenyekiti kumpa mamlaka Mhe. Waziri ya kutoa leseni, kumpa mamlaka waziri ya kuongeza muda wa kibali mimi nina wasi wasi na wasi wasi ndio akili. Waziri huyu leo Da Salama leo *alhamdulillah* kahiji Mwenyezi Mungu amuweke. Lakini anaweza kuja Waziri mwengine wa kesho na mwengine roho yake haijashindiliwa ana tamaa hii leseni akaitoa kwa 10% na hichi kibali akatoa kwa 10%.

Mhe. Mwenyekiti, nchi zilizoendelea wana msemo mmoja wanasema *always majority ideas is the only way forward,* kwa hivyo hapa nilikuwa naomba kuna *schedule of amendment* yangu jambo hili asitoe leseni wala asitoe kitu bila ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi ambayo ndio chombo kikubwa kwa nchi hii kwa kuepusha na kulinda mali kwa maslahi ya wakwezi na wakulima, sio wote Waheshimiwa Mawaziri na watu wengine waliokuwa roho zao safi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru mawazo ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh mawazo ambayo ya serikali na akisoma kifungu cha 64 (3) ndivyo ambavyo kinasema. Waziri hatotoa leseni ya uendeshaji chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hichi bila ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, tayari marekebisho hayo yapo kwenye kifungu cha 64.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa nazungumzia vifungu, kifungu cha 51 kunako sheria mimi sikusoma sheria lakini tunakwenda kwa mujibu wa vifungu.
Kifungu cha 51 na 59 hicho kifungu anachokizungumzia Mhe. Mwanasheria Mkuu ingawaje yeye ndiye *the master,* ni chengine na hivi ni vifungu vyengine.

Ombi langu na pendekezo langu maneno haya yawemo kwenye kifungu hichi, nimeona kunako baadhi ya vifungu maneno haya yamewekwa. Mimi *schedule of amendment* ime- *specify* namba 51 na 59 kweli kwengine imo lakini kwengine hamna, humu ninazungumzia 51 kwa Kiingereza na 59 *in English.* Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 51 kinaweka utaratibu wa kuomba leseni na kifungu cha 64 ndio kinatoa utaratibu wa jinsi gani hiyo leseni itolewe. Sasa hiyo leseni kabla haijatolewa kama anavyosema yeye, tayari Mhe. Waziri hawezi kutoa bila ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi na ndivyo ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 64(3).

Sasa vifungu hivi lazima uvisome pamoja, huwezi ukasoma kimoja kimoja na kila pahali uandike maneno ambayo kila kifungu kina utaratibu wake, hapa ni uombaji halafu kuna utoaji. Sasa kifungu cha 64 ndicho kinaelezea sasa utaratibu wa utoaji wa leseni na kuingia mikataba na huwezi kufanya hivyo kabla hujapata idhini ya Baraza la Mapinduzi.
Sasa anachosema Mhe. Hassan Khamis ni kile kile ambacho kinasema serikali kupitia mswada huu, kama tayari kipo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hata kamati imependekeza vifungu hivyo. Sasa namshangaa sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, yeye ni nguli wa sheria, wakati anachokisema yeye hicho ni kifungu chengine mimi Hassan Khamis Hafidh wa Welezo nazuia kifungu chengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu kaeleza vizuri kwamba hizo *process* za kutoa leseni kwenye hicho chengine cha mwisho alichokitaja cha 61 nadhani ndio kinatoa mamlaka sasa kwamba lazima apeleke kwenye Baraza la Mapinduzi, hivyo unavyotaka wewe inakidhiwa na hicho cha mwisho alichokizungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mimi nadhani tuendelee tusivutane. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, wewe ndio mwenyekiti kwa heshima na taadhima sijaridhika kwa sababu msimamo wangu uko wazi, mimi kuna siku nakufa katika kulinda mali ya wakwezi na wakulima. Lakini kwa vile kiti ni chako Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee kama ulivyoniomba, naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu iko kwenye kifungu cha 45 (7) jana wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kifungu hichi na naomba nikinukuu kinasomeka kwamba:

"Kwa madhumuni ya sheria hii kampuni itaiomba kampuni kuomba leseni au kibali na itawasilisha kwa kampuni tarifa zilizoelezwa katika leseni au kibali husika".

Mimi nilitaka nipewe ufafanuzi kwanza ni kampuni gani itakayoiomba kampuni, ni kampuni gani itakayoomba na kampuni gani itaombwa, maana yake hapa kuna kampuni itaiomba kampuni. Kwa hiyo, ni kampuni gani itakayoomba na itakayoombwa.

Pia nikapendekeza kwamba kuongezwe maneno kwamba ili kitajike kampuni tanzu itaiomba kampuni, kwa sababu hapo kuna kampuni itaiomba kampuni.

Sasa haijulikani ni kampuni gani ambayo itaiomba mwenziwe. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nitoe ufafanuzi ili wasije Wajumbe wakauliza tena kama mbona kuna K kubwa na k ndogo. Ukiona K kubwa sehemu yoyote ya mswada huu ni Kampuni ya serikali, na ukiona k ndogo inazungumzia kampuni ni kampuni ile ambayo inakuja kuwekeza kwa kushirikiana na Kampuni ya Serikali ni kama unavyotaja *Bank of Tanzania you always prefer capital B* kwenye *Bank of Tanzania* na benki nyengine zozote unazungumzia ukizitaja *small capital b*, na hapa ni hivyo hivyo, kama ukitaja *capital k* unazungumzia kampuni ya mafuta ya serikali na hii *small capital k* ni kampuni zinazokuja kuwekeza ndani ya nchi. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mwanasheria Mkuu yeye ni Mwanasheria mimi nakubali. Lakini pamoja na kuwa ni maneno ya kisheria, je, haoni kwamba mambo haya yanajifunga jifunga na hii mikataba ni mali ya Wazanzibari, na Wazanzibari wengi walioko huko vijijini pengine wanataka kujua haya, lakini wao hawawezi kujua kama *capital* kubwa sijui ndogo au nini mambo haya.

Kwa nini isiwekwe wazi ikataja kama kampuni kadhaa au ya serikali ndio itaiomba hiyo kampuni au itaitaka kampuni pamoja na hivyo, ni sawa ni mambo ya kisheria, lakini kwa nini isiyaweke wazi haya ikawa inasomeka kwa kila mmoja akaielewa. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu jaribu kuangalia tafsiri kule mwanzo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaona.

Mhe. Mwenyekiti: Ipo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, Mwanasheria hebu atuelekeze hapo ilipo.

Mhe. Mwenyekiti: Ukurasa wa 67 Mheshimiwa hebu angalia kampuni. Maana yake ni kampuni, sawa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ukianza kusoma kwenye tafsiri imeelezwa vizuri nini maana ya

kampuni. Lakini katika tafsiri hii ime-*refer* kifungu cha 32 inamaanisha hiyo kampuni maana yake nini ambapo ukienda kifungu cha 32 kiko wazi kabisa kinasema kwamba:

Kampuni maana yake ni *ZPDC* ambapo tafsiri hii halisi itakuwa ndio ile Mheshimiwa Mjumbe anaiulizia.

Kwa hiyo, kampuni imetafsiriwa katika *interpretation*, na katika *interpretation* imeelekeza wazi kwamba unapolikuta neno kampuni inatakiwa ku-*refer* moja kwa moja katika kifungu 32 (1) imetafsiriwa na unapokwenda kusoma kifungu cha 32(1) tafsiri ya kampuni iliyotafsiriwa ndio ile Shirika la Serikali *ZPDC*, ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi pamoja na majibu mazuri ya waziri lakini nataka nione, maana yake hapa naona hizo kwanza hizo K zilizotajwa hiyo kubwa na ndogo zote ziko sawa. Kwa hiyo, ni ipi katika hizi mbili, maana yake kampuni ni k na hii nyengine hivyo hivyo. Hebu Mheshimiwa tuelekeze au tupendekeze itafsiriwe katika *interpretation* tafsiri yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kwenye ukurasa wa 67 ukianza eneo la kwanza unakuta kwamba kuna neno kampuni imeandikwa vizuri tu imeandikwa "kampuni" kuna koma mbili zile maana yake ni Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 32 (1) cha sheria hii ambapo ukisoma hicho kifungu cha 32(1) kinaeleza hivi kampuni ya Maendeleo imeanza kwa *capital*. Maana yake kuanzishwa kampuni ambayo imeanza kwa *capital* ya maendeleo ya mafuta na gesi asilia Zanzibar ambapo kifupisho chake kitakuwa ni *ZPDC*, ambayo itashiriki katika shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa niaba ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Naam, Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na majibu hayo lakini bado ninasimamia ile hoja yangu, kwa nini hiyo aliyosema (k) na yenye koma hizo mbili alizoziashiria hivyo. Je, kwenye huu mstari huu hiyo kampuni imeoneshwa hizo koma mbili alizozitaja Mhe. Waziri. Mimi ndiyo hoja yangu ilipo, mbona hapa haipo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ni zaidi ya mara tatu sasa hivi utakuwa unahoji.

Mhe. Omar Seif Abeid: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Utakuwa unaenda *beyond* mara tatu ambayo sasa kama hujakubali nitalazimika kuwahoji Waheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Sawa Mhe. Mwenyekiti, mimi naona haijanikalia sawa hii.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tuhoji au vipi, tuipigie kura.

Mhe. Omar Seif Abeid: Naam! Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tuipigie kura?

Mhe. Omar Seif Abeid: Basi tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nimelazimika kusimama kati kati ya shughuli zetu hizi ili kumtambulisha mgeni ambaye ninamuona pale juu, ambaye ni Waziri wa Nchi Afisi wa Makamo wa Rais Anayeshughulikia Muungano na Mazingira. (*Makofi*)

Ni Mhe. Januari Makamba, karibu sana, inatia moyo kwa sababu haya mambo tuna ridhaa nzuri sana ya wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bila shaka Mhe. Waziri amekuja kutuunga mkono. Ni jambo ambalo linatia moyo sana. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaendelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mimi nilipokuwa ninachangia nilichangia Kifungu cha 45 (5) kinachosema kwamba kuna neno hili "isiyozidi asilimia 25", niliomba sana, kwa sababu naomba kunukuu kifungu chote.

Kinasema kwamba Kifungu cha 45 (5)

Kifungu cha 45 (5) ; "Leseni iliyotolewa chini ya Kifungu kidogo cha kwanza (1) itataka kampuni kuwa na hisa ya ushiriki zisizodi asilimia ishirini na Tano (25)".

Ni ndogo sana kwa sababu bora tubadilishe isiyozidi tuseme isiyopungua, kwa sababu mtu anaweza kuweka asilimia 5, anaweza kuweka asilimia 10, asilimia

2. Kwa sababu isiyozidi asilimia 25. Naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu aniwekee wazi ili niweze kufahamu vizuri ili angalau basi iwe isiyopungua, najua iko asilimia pale 25.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Abdalla Maulid Diwani na hoja yake ya kusema kwamba zile hisa za ushiriki ya kampuni ya serikali ambayo Kifungu cha 45 (5) kinasema iliyotolewa chini ya Kifungu 45 (1) itaitaka kampuni kuwa na hisa za ushiriki zisizozidi asilimia 25 na yeye anasema kidogo. Labda tuweke asilimia 50 au 70. Lakini tunachozungumza hapa, tunazungumza ni *funds*.

Tunazungumza ni fedha. Kama mtu anakuja kuwekeza *a multi billion business* ya mafuta. Wewe Serikali kampuni yako, kila anayekuja kuwekeza wewe ndiyo una-*hold* leseni. Sasa ukisema tuweke isiyozidi asilimia 50. Maana yake wewe unachotaka kusema kama sasa kila anayekuja kuwekeza wewe, utoe na wewe asilimia ya yule ambaye anakuja kuwekeza.

Mhe. Mwenyekiti: Imesema isiyopungua asilimia 25 Mheshimiwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Isiyopungua 25. Ndiyo maana yake anataka tuanzie asilimia 25 kwenda mbele. Sisi tunachosema ni kama tunaanzia moja isizidi asilimia 26. Na hii ndiyo ambayo kwenye *region* watu wanavyofanya. Kama huwezi uka-*subject* kampuni yako kuwekeza zaidi ya asilimia 25 ambao uwezo wenyewe wewe hukuujenga. Kama lazima kwanza ujenge uwezo, kampuni yako ile uijenge uwezo, ikishakuwa na uwezo moja ya jambo ambalo inafanya itakuwa inashiriki wenyewe kwenye kutafuta hayo mafuta, wala haitokuwa na haja ya kutafuta mshirika mwengine.

Lakini tunachosema sasa hivi ni kama tunaijengea uwezo ile kampuni yetu. Kama atakayekuja kuwekeza basi na yeye awe na asilimia kuanzia moja mpaka ishirini na tano, kiwango tutakubaliana. Hii tutawekeza asilimia kumi na tano, hii tutawekeza asilimia 20, hii tutawekeza kumi na tisa itategemea na uwezo wetu kila unavyokua kwa kadri ya hali itakavyokuwa.
Sasa utakapoiongezea Mhe. Mwenyekiti, uwezo ujue inaiongezea gharama ambazo kwa sasa hivi hatuna. Ndiyo maana tukaweka hivi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na ninampongeza. Mimi wazo langu ni kwamba tukisema isiyozidi asilimia 25, kuna watu wengine wanakuja hapa wawekezaji wakasema wanaweka asilimia moja tu, tutampa pia kwa sababu hajafika asilimia 25.

Sasa angalau tuweke kwenye asilimia 25 kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hii ni raslimali kubwa sana na unyeti wake ni mkubwa sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu ningekuomba sana katika hichi ninafikiri uridhie. Laa kama ndiyo mumeshaamua munakuja kwamba hamtaki kuondosha harufi moja, basi tupige makofi tuondoke, lakini nafikiri sisi sote tuna nia njema sana ya nchi hii, nyinyi wa mbele muna nia njema ya Mswada huu na sisi vile vile. Na sisi pia tumeusoma na kuupitia tukawafuata wanasheria wakatuongoza.

Sasa sijui kuna ugumu gani angalau basi mukatukubalia hii isiyopungua asilimia 25. Kwa sababu wajanja wengine wanaweza kuja hapa wakaja na asilimia 3, tutawapa pia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi nakuona unataka kusaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, suala hili tunalozungumza hapa ni suala la biashara ya mafuta, na biashara hii inapaswa tukumbuke kwamba inafanywa ukanda mzima huu ama itafanywa ukanda mzima.

Miongoni mwa jambo ambalo limeishawishi Serikali kuweka hii *bar* ya 25 iwe ni miongoni mwa vichocheo ambavyo vitawashawishi makampuni mengine makubwa kuja kuwekeza kufanya biashara na sisi. Tujue tu kwamba kwa wenzetu takriban nchi tatu, mwamala ule wa kampuni za serikali zipo asilimia 15. Sisi tukasema tupandishe tusijifunge katika asilimia 15, twende kwa *bar* ya 25.

Maana yake kama ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza mtaji ule unaokuja kuwekezwa ni sehemu ya hisa ambazo zinazotokana na kile kibali ambacho kampuni yetu ya Serikali inakuwa imepatiwa. Kwa hivyo ukitazama ukubwa wa mtaji ambao unakuja kuwekezwa katika sekta hii ya mafuta, ukimwambia mwekezaji kwamba mimi ninachukua asilimia 25 au 30 au 40 ya mtaji ule ambao unakuja kuwekezwa, kwa sababu tu wewe unamiliki leseni. Bila shaka yoyote wewe utakuwa unawakimbiza wawekezaji, na kama unawakimbiza wawekezaji, maana yake wewe utakuwa na raslimali ya mafuta ardhini lakini unashindwa kuivuna kwa sababu hatuna uwezo mkubwa wa kitaalamu, hatuna uwezo mkubwa wa fedha kwa ajili ya kuchimba, hatuna vifaa. Kwa hivyo ile faida ambayo tunayoitarajia hatutoweza kuifikia.

Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Mjumbe akubaliane na dhana ya Serikali ya kwamba tuwe na uwezo wa kuvuna faida kwa msingi ya kuwa tuwekeza hisa

zetu kutoka asilimia 1 mpaka 25 ikiwa kama ni kichocheo cha kushawishi wawekezaji waweze kuja kutumia fursa hii. Ni kweli ungeona kwamba kuna haja ya kuwa na asilimia 40, 30, 50 lakini unapokwenda ushindani wa biashara, lazima utazame na wewe kuweza kushinda, ili kuweka zabuni na watu wa kuja kuwekeza nchini kwako ili utazame matokeo mengine utakayopata baada ya kuvuna mafuta, usibaki na mawazo kwamba una mafuta, unashindwa kuyatumia kwa ajili ya kuimarisha huduma kwa wananchi wako.(*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninamsifu sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ufafanuzi wake mzuri, maelezo mazuri, lakini mimi ninakumbuka ninarudi nyuma kidogo.

Hapo zamani Baba wa Taifa wa nchi hii alikataa kuingia katika biashara na wawekezaji wa nje kwa sababu ya kuhifadhi kile ambacho alichokuwa nacho, kuliko kuruhusu halafu ikatoka tukaachiwa mashimo na mahandaki ambayo hayana faida, ambao mfano mdogo sasa hivi unaonekana huko Shinyanga na sehemu nyengine. (*Makofi*)

Sasa hii asilimia tunayozungumza hapa pamoja na maelezo aliyokuwa nayo Mhe. Waziri, kuna ugumu gani basi wangesema kuanzia asilimia 10, isizidi asilimia 25 ingekuwa afadhali. Lakini sasa leo unaweka wazi isiyopungua asiyopungua asilimia 25, mtu anaweza kuja asilimia 1. Je, pia tutakubali hilo? Ndiyo swali langu lipo hapo tu hata asilimia 1 utampa, kwa sababu hakimfungi akiweka moja, akiweka asilimia mbili, asilimia tatu, yote anaweza hayo.

Basi aweke *specific* angalau kuanzia asilimia 10 lakini asiyepindukia asilimia 25.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa labda na mimi nisaidie kidogo. Unajua hii asilimia, Serikali wanaita asilimia lakini katika uhalisia ni fedha ambayo inayowekezwa ni fedha halisi. Hili suala la uchimbaji wa mafuta, uwekezaji wake unachukua gharama kubwa. Hii asilimia inayozungumzwa hapa ni asilimia ya kifedha ambayo itachangiwa na Serikali katika kufanya shughuli ile ya uchimbaji mafuta. Sasa ninadhani tuliangalie hivyo, halafu labda nimpe Mhe. Mwanasheria Mkuu azidi kutoa ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa ufafanuzi ambao umeutoa ni ufafanuzi sahihi.

Naomba Mhe. Diwani afahamu tu hapa siyo ile kampuni inayokuja. Hii ni kampuni ya Serikali. Ile inayokuja itatakiwa iwe na hisa nyengine hizi ambazo tutakubaliana. Na sisi tunasema ni kama tuna uwezo wa kujadiliana na mtu kuanzia hisa moja mpaka hisa ishirini na tano, kama na sisi Serikali hututokubali uje uwekeze useme una hisa moja au hisa mbili. Nimesema kwenye *region* ilivyo sasa hivi kwenye nchi ambazo zina mashirika ni *fifteen percent*. Kuanzia moja mpaka *fifteen percent*. Sisi tumeongeza tuseme kama basi isipungue asilimia ishirini na tano. Ndiyo *region* ilivyo Mhe. Mwenyekiti, na ninakushukuru kwa ufafanuzi wako. Kama hichi tunachokizungumza hapa ni pesa. Mtu anapokuja kuwekeza dola bilioni moja akakwambia wewe toa asilimia ishirini na tano, maana yake unatakiwa utoe pesa nyingi.

Lakini ukisema aah! kwenye hii mimi basi asilimia yangu itakuwa kumi. Angalau na wewe unajipanga jinsi gani uingie kwenye hii biashara. Lakini tutakapokua na sisi tuna uwezo hata wa kufanya wenyewe biashara Mhe. Mwenyekiti, bila hata kushirikisha mtu mwengine yeyote. Lakini kwa sasa hivi na kwa sababu ndiyo kwanza tunaanza hatuna mtaji huo, lazima na sisi tuweke *bar* ya kuchangia katika kuwa na hisa katika hizi kampuni zitakazokuja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri sana marefu mno, siasa nyingi za Mwanasheria Mkuu basi madhali sote humu na tumekuwa mashahidi kwamba tunawatafutia wakwezi na wakulima maslahi yao ya nchi hii, basi tuendelee *in shaa Allah*. (*Makofi*).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, wala isionekane vioja kwamba Mwenyekiti akapiga buti.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunamshukuru Ndugu yetu Mhe. Januari Makamba Mhe. Waziri wa Jamhuri karibu sana na hii ndiyo ile aliyoizungumza Mhe. Waziri kwamba katika eneo hili wakati Bunge na Mhe. Waziri alikuwemo katika kutunga sheria hakutokuwa na matatizo yoyote. Tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ipo katika Kifungu cha 99 na hili tulikubaliana kutokubaliana na Mhe.Waziri pamoja na timu yake. Kifungu hichi tulishindwa kukubaliana katika eneo ambalo labda nikisome chote,

Kifungu cha 99; "Endapo, katika shughuli ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia, Kampuni na Mkandarasi wataingilia haki za mkaazi halali wa ardhi yoyote au watasababisha hasara ya mazao, miti, majengo, ghala au kazi zinazofanywa kulingana na shughuli zinazofanyika, Kampuni na Mkandarasi watamlipa mkaazi halali fidia inayofaa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Ardhi".

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu ingawa Wanasheria unaposema *best practice* hawapendi lakini lazima tuitumie. Uzoefu katika uwekezaji hasa kwenye ukanda wa mahoteli. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wengi katika ukanda wa pwani ikiwemo kwetu Pwani Mchangani walilipwa vipando vyao pengine mashina kumi ya minazi na mihogo na migomba na wengine wakapata pesa za kuwekezea nyumba zao tu. Lakini uwekezaji ule sasa hivi unaingiza mabilioni ya mashilingi lakini wao wamerudi katika umaskini wa kutupwa. Wakati maeneo yale walikuwa wakilima wanasomesha watoto wao na wanaendeshea familia zao.

Sasa sisi kwenye Kamati tulishauri basi ile fidia atakapopewa mwananchi iendane na bei ya soko au alipwe fidia endelevu. Mfano kama mtu alikuwa na shamba lake analima basi aangaliwe na tutakapokuja kupitisha ile Sheria ya *Revenue Management Act*, pale wanaweza wakaja wakawekewa utaratibu wa kulipwa ukawa endelevu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama hatukuweka katika msingi wa sheria hii, ina maana watakuja kulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu sasa hivi hapa wapo pale Darajani, Baghani visima huko Oman vinachimbwa huku wanavuna tu kwa mikoba kila siku. Sasa sisi hapa Mhe. Mwenyekiti, isije ikawa uvunaji wa gesi na mafuta unavunwa mtu shamba lake keshaambiwa huwezi ukalitumia tena, keshapewa pesa zake keshanunua bati, halafu anakosa haki yake moja kwa moja.

Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, ndiyo tulikuwa tunataka kujenga nguvu ya haki ya wananchi, ule ushirikishwaji wa wananchi tunataka uanze *from day one*. Mtu eneo lake anaambiwa usilitumie tena, anahakikisha kila mwezi na yeye anavuta.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ukisoma maelezo ya Kamati kwenye hotuba ya Kamati walipendekeza alipwe fidia ya bei ya soko, ndiyo ambayo walipendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tunapoyazungumza mambo haya, mambo haya lazima tuyatambue msingi wake. Moja tumesema kwamba ardhi ni mali ya Serikali. Wewe unafidiwa vile vilivyokuwa juu. Kama umejenga nyumba, kama una vipando, wewe unafidiwa kwa vile vilivyokuwa juu lakini vilivyokuwa chini si vyako, ni mali ya Serikali. Na ukisoma Sheria hii inaeleza vizuri mtu huyu atalipwa fidia kwenye maeneo gani, lakini fidia hii inaongozwa na Sheria ya Ardhi, kwa sababu Sheria ile ndiyo inayotoa mamlaka ya kutoa hiyo ardhi ya Serikali kwa wananchi. Lakini Sheria hiyo hiyo ikaweka utaratibu wa namna gani Serikali inapotaka kuchukua ardhi ile.

Ukisoma pia Katiba imeelezea hivyo hivyo kama unaweza ukachukua ardhi ya mwananchi lakini unachotakiwa kufanya ni kumlipa fidia.

Zamani tukichukua tuki-*confiscate*, hatulipi fidia, unachukua cha mtu ume-*confiscate*, umekitaifisha humlipi fidia yake. Lakini kwenye zama hizi za utawala bora tumesema inapotokea dharura na pale ambapo Serikali itaamua kuchukua basi hilo eneo, basi ni lazima imlipe fidia, na fidia yenyewe imewekewa utaratibu wake kwenye Sheria ya Ardhi.

Siyo hivyo tu Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kifungu hichi hichi cha 3, kama mtu ambaye hatoridhika na ile fidia aliyopewa, ana haki ya kwenda kushitaki na kupeleka hoja yake, kusema mimi mali yangu gharama yake ni kiasi fulani, lakini Serikali imenipa kima fulani, sikuridhika na kima ambacho Serikali imenilipa, kwa hivyo naleta maombi yangu. Hapa hatumlipi fidia mwananchi kwa kile ambacho tunatarajia kutoa chini ya ardhi, sisi tunamlipa fidia kwa kile ambacho kipo juu ya ardhi ambacho amekiendeleza. Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na ufafanuzi wake nimeusikia lakini Waswahili wanasema, "*Ukupigao ndio ukufunzao*". Sasa Mhe. Mwenyekiti, amezungumza vizuri kwamba mwananchi ile ardhi atalipwa kile ambacho alichokiweka juu, kile cha chini siyo cha kwake.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na shamba langu lina ekari tano na shamba lile ndilo nilikuwa ninalima viazi, migomba ndiyo ninatoa maisha ya familia yangu yote. Hata ajira Serikalini sina. Sasa leo Mhe. Mwenyekiti,...

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Hamza. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ninakuona kwenye *gallery* wakati nilikutegemea uwemo humu ukumbini, tena upo kwenye kivazi ambacho siyo rasmi kwa hapa Barazani. Naomba ukabadilishe hicho kivazi halafu urudi humu ndani Mheshimiwa. (*Makofi*)

Tuendelee Mhe. Hamza.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! *Astaghfirullah laadhim*, ndiyo mambo. (*Kicheko*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, narudia tena kusema, suala hili ni zito kidogo, naamini pengine tutakapokwenda kutoa elimu kwa wananchi wetu, katika eneo moja litakalotupa tabu sana ni hili.

Mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, hebu tuwaangalie wenzetu Songosongo. Kamati yangu tunaishukuru sana wizara iliwapeleka wajumbe wangu Songosongo kwenda kuangalia wananchi ambao walikuwa wakitumia bahari na sehemu nyengine, jinsi gani serikali kwa kupitia *TPDC* walivyowapa sasa hivi huduma za maendeleo za kudumu.

Wenzetu Mhe. Mwenyekiti, kule mpaka umeme wanapewa bure Songosongo. Leo kama wale wangeambiwa tu basi leo tunawalipeni hii fidia, endeleeni kufanya shughuli zenu nyengine, wale leo wangekuwa wanalipa umeme.

Leo Mhe. Mwenyekiti, Songosongo watoto wanasomeshwa bure, kulikuwa hakuna skuli, Songosongo kunavunwa gesi Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa mwisho msomi wa kule kafika darasa la tano. Leo watoto tayari wana *masters* wako Dodoma Chuo Kikuu, kutokana na uzalishaji uliokuwepo pale wa gesi, sasa ile ndio faida endelevu tunayoitaka kwa wananchi.

Leo kama wale wangeambiwa basi eneo lenu limeshachukuliwa. Ile faida wanayoipata wale wananchi pale ni kijiji kizima. Ndio maana tukasema kama mtu hapa angalau, maana yake unajua katika biashara hii kubwa wananchi wetu sio lazima walipwe mabilioni ya shilingi, wanaweza wakawekewa utaratibu ili asijute kwa ile biashara kuja kufanyika katika lile eneo lake. Mifano hai ipo ndani ya Tanzania kwa nini sisi tunashindwa kuiga. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Hamza Hassan Juma sana na ninamshukuru kwamba kafahamu utaratibu wa kulipa fidia. Anachosema sasa hivi yeye, ni utaratibu gani tutaweka wa

kuliendeleza lile eneo husika, lile ambalo litakuwa limechimbwa na kuanza kuvunwa hayo mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri na ni la msingi, lakini utaratibu wake unawekwa kwenye yale maombi ambayo mwekezaji anatakiwa alete. Moja ya jambo ni hilo, kuweka utaratibu wa jinsi gani utatoa manufaa kwa eneo husika. Kama utajenga hospitali, kama utajenga skuli, kama utawekeza kwenye maeneo gani. Lakini moja ya shuruti ni lazima uhakikishe kwenye lile eneo ambalo unalifanyia kazi unaliendeleza. Ni kweli leo na inasikitisha sana kama kwenye maeneo yetu ya fukwe yote, mfano ya kutoka Kiwengwa mpaka mwisho kule, hakuna hata *dispensary* kubwa ambayo ipo na mtalii akipata dharura kule akimbilie Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kinachotakiwa ni kwamba wawekezaji wale wote sasa wajenge nguvu ili kuwekeza kwenye maeneo yale. Sasa nimemfahamu Mhe. Hamza Hassan, lakini namwambia hoja yake hiyo itakuja kushughulikiwa kwanza mnapoingia ile mikataba, lakini pia ni moja ya sharti la muombaji ambaye anatakiwa apeleke ni jinsi gani ataliendeleza eneo husika. Sasa fidia mimi nadhani tuache utaratibu wake ule ule, lakini yale anayosema ya kuendeleza yamo, ni lazima uendeleze eneo husika. Sasa utaratibu wake Mhe. Mwenyekiti, utaelezwa kwenye ile mikataba ambayo tunaingia na makampuni hayo Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tunapitisha mambo mengi hapa kwa nia njema, lakini hapa sheria imetaja wazi wazi, kampuni na mkandarasi watamlipa mkaazi halali fidia inayofaa kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa ardhi. Huyo mwekezaji katika huo mkataba atakuja na kifungu hiki cha sheria.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni Mwenyekiti wa Kamati, na kama nilivyosema ilifika pahala tulikuwa tunaahirisha kikao, tukawaambia nendeni mkafikiri. Wanakwenda wanafikiri wee. Sasa mimi nilikuwa naomba sana kwamba katika hiyo mikataba, unajua mimi Mhe. Wanu Hafidh keshanirithisha Kiingereza, *Revenue Management Act*, sijui kwa Kiswahili inaitwaje. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sheria hiyo itazungumzia mpaka mapato ya halmashauri. Sasa mimi nadhani kuna maeneo kule ndio maana katika ripoti yangu nilipendekeza, kwamba sheria hiyo ikija kuna maeneo lazima itabidi yaje Barazani kwa ajili ya *approval*.

Sasa hiyo ndio itakuja labda kuwalinda hao wananchi wetu katika maeneo ambayo watakayoathirika. Kwa hivyo, kitu ambacho nilikuwa najaribu kutoa angalizo ni kwamba iko haja sasa hivi sheria yetu ya ardhi Mhe. Mwenyekiti, ingawa sio pahala pale katika kupitisha vifungu, iko haja ya kuifanyia marekebisho ya kutosha, kwa sababu sasa hivi haiwasaidii wananchi, isipokuwa inawavunja moyo wananchi. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, kama Mhe. Hamza Hassan angesoma kwanza kifungu cha 134, angeona utaratibu gani ambao umewekwa wa kutoa, kinasema;

"Kampuni na wakandarasi watachangia katika jamii kwa kusaidia taasisi za kijamii za elimu ya juu na vituo vya elimu ya amali".

Imeelezwa utaratibu wake mzima na akisoma kifungu cha 137 pia imeelezwa utaratibu wake. Yeye hoja yake mwanzo ilikuwa ni utaratibu wa kulipa fidia na tukasema fidia hiyo utaratibu wake umewekwa muongozo wake kwenye sheria ya ardhi. Sasa haya ya kusaidia jamii utaratibu wake ni huu wa kisheria. Sasa kiwango gani, maelezo haya ya ziada kwa sababu kutakuwa kuna ule muongozo ambao mwekezaji amekuja nao, lazima uwemo kwenye muongozo wa kila mwaka wa kazi zake anazotakiwa kufanya.

Sasa Mhe. Hamza anayoyasema kwa niaba ya jamii, tayari yameshughulikiwa kwenye kifungu cha 134 na 137, lakini kulipa fidia utaratibu wake umeelezwa kwenye sheria ya ardhi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, 'kampuni na mkandarasi wataingilia haki za mkaazi halali kwa ardhi yoyote, au watasababisha hasara kwa mazao...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis, hivi punde tu Mhe. Hamza Hassan nadhani alikuwa na jambo hilo hilo, katika kifungu hicho ambacho kimetolewa ufafanuzi mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, niliwasilisha *schedule of ammendment* Mhe. Hamza ni Mwenyekiti. Sasa kwa vile ni mpya naomba kufahamishwa. Lakini bado nalinda hoja yangu kwenye *schedule of ammendment* yangu, kwa sababu niliifanyia *research* ndio nikaleta *schedule* kwa maandishi kwako. Sasa kama ninayo haki sawa kama sina haki nitakusikiliza Mwenyekiti, wewe ndio Mwenyekiti wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, haki unayo lakini hatufanyi *repetitions* tu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, yangu mimi sio *repetition*, kwa sababu

Mhe. Mwenyekiti: Una hoja tofauti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Eeh. Kwa sababu *according to the schedule* yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya tumsikilize.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, inafanya kuingiliana. Naendelea kumaliza kuisoma, na shughuli zinazofanywa na kampuni na mkandarasi, watamlipa mkaazi halali fidia. Sasa mimi nimesema iwe fidia endelevu kwa kipindi chote cha uwekezaji kwa mujibu wa makubaliano.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja ndio ile ile ya Mhe. Hamza Hassan hiyo hakuna tofauti. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi ni mpya, napenda kuelekezwa na kiti chako, kama...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tumekufahamu sote hakuna matatizo, naomba ukae. Mhe. Omar Seif Abeid *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi tena. Mimi hoja yangu inakuja kwenye 73(1) naomba kuisoma, inasema;

Kifungu cha 73(1)

"Mkandarasi hatosimamia haki yoyote ya leseni au sheria hii,

(a) Bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa waziri inayohusiana na…", ikisha ndio ikaendelea.

Sasa mimi jana nilitoa mapendekezo wakati nilipokuwa nikichangia, kwamba iwekwe vizuri, kwa sababu ukisoma bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa waziri inayohusiana, naona haiko sawa. Ama ningependekeza liwekwe neno, waziri anayehusiana au kama itaendelea kwamba ibadilishwe kutoka waziri iwe wizara, kama tunaendelea na hii sentensi. Lakini hapa hii

haifahamiki au haieleweki vizuri. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sikumpata vizuri, lakini acha nikisome ili tuelewane. Kifungu cha 73(1) kinasema,

Kifungu cha 73(1);

"Mkandarasi hatosimamia haki yoyote ya leseni au sheria hii

(a) Bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa waziri inayohusiana na;

Sasa hii inayohusiana imetaja orodha ya mambo ambayo anatakiwa apate ridhaa ya maandishi. Sasa hii inayohusiana na, inahusiana na yale mambo ambayo yameorodheshwa, kama kwenye haya mambo ambayo yameorodheshwa hatofanya kazi mpaka kwanza apate ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mhe. Waziri. Sasa sikumfahamu hoja yake ni nini kwenye kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mimi hoja yangu iko kwenye hilo neno waziri, na inayohusiana, hayo maneno mawili tu, mimi ndipo nilipo. Ningeomba yafanywe marekebisho. Ikiwa tutatumia neno wizara inasomeka vizuri, laa ikiwa ni waziri iwe waziri anayehusiana na;

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ni *syntax error* tu nafikiri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Nimemfahamu naomba nimjibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri hapa Mhe. Omar Seif alikuwa anazungumzia kuhusu lugha, lakini pale imezungumziwa ridhaa, na ridhaa inayohusiana, yaani na mimi nilikuwa napata shida kwenye sheria, ndio hiyo *best practice and lead practice,* lakini nafikiri baada ya mswada huu wengi wetu tumepata uelewa. Kwa hivyo, kutokana na neno ridhaa ndio maana likaja lile neno inayohusiana, najua alikuwa anarekebisha Kiswahili, naomba Mhe. Omar Seif akubali hili kwa sababu wataalamu wetu walijitahidi kutufahamisha katika uandishi na maneno yanavyokwenda, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Sawa tuendelee.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu afungue Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 ya Jamhuri, wakati tunakwenda sambamba na kifungu cha 62

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, *reference* yetu ni sheria hii tunayoipitisha.

Mhe. Simai Mohamed Said: Sawa, nimeanza vizuri najaribu kusaidia. Kwa hivyo, naomba basi kifungu cha 62 (1) na (2). Wakati nilipokuwa nachangia nilizungumzia juu ya kifungu hiki jinsi mamlaka muda uliotolewa kwenye kifungu hichi ni mdogo mno.

Kifungu hiki kinazungumzia muda uliotolewa ambao ni mfupi sana kutokana na sehemu gani ya ugunduzi utakaofanyika, muda umebainishwa kuwa usizidi miaka miwili kwa utafiti wa mafuta na miaka mitatu kwa gesi asilia. Sasa ukiangalia katika bahari kuna kina kirefu, muda huo utalazimika kuongezeka kwa sababu kifungu hicho hakitoi ruhusa kwa mamlaka kuongeza muda kwa kampuni kufanya tafiti husika. Sasa ukiangalia kwenye sheria ya Jamhuri kwenye kifungu cha 65(1) na 66(1) hiyo ruhusa imetolewa. Sasa kwa muda huu na hiki kifungu hapo kilipowekwa mamlaka itashindwa kutoa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hapa Mhe. Simai Mohamed nadhani angefahamu kwamba hapa kinachotafutwa ni kufanya utafiti juu ya kile kima ambacho kipo, kwa sababu kama ugunduzi tayari ameshagundua. Lakini sasa inabidi afanye utafiti mwingine wa kibiashara, kama utafiti niliougundua huu *is it commercial*, unaniwezesha mimi kuanza kuchimba na kurudisha faida yangu ambayo nimewekeza, kwa hivyo ndio maana ikawekwa hii miaka mitatu, kuwa asichukue muda mrefu akawa yeye anafanya kazi zake anafanya utafiti tu. Afanye kwa muda mfupi, kama ameamua kuwa hii haimtoshi sio *commercial* kwake yeye aache apewe mtu mwengine.

Sasa ndio maana hapa ikabanwa kama yule mtu tumpe hii miaka, kwa sababu kama ugunduzi unakuwa tayari umeshagunduliwa, hapa kinachotafutwa sasa ni ule mpango wa biashara, kama je, ugunduzi huu niliougundua *is it commercial viable*, kwamba utaniwezesha mimi kuweza kurudisha uwekezaji ambao nimeuwekeza. Kwa hivyo, ndio dhamira ya kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, na ndio maana tukamuwekea *specific time*, kama tumembana ndani ya miaka mitatu lakini hatukutaka kufungua muda mrefu ili asiweze kufanya kazi, ndio maana tumembana kwa muda Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kama utafanya utafiti wa kwenye *off shore* na kama nilivyosema kwamba kwenye bahari kuna kina kirefu, na ukizingatia jambo ambalo katika hii sheria yenyewe hawajaonesha ukubwa wa vitalu, ambapo ukiangalia vitalu vya sasa hivi ambavyo *TPDC* amevikata ni kati ya mita za mraba 10,000. Sasa ukiangalia kwa muda wa miaka mitatu bado kampuni inataka kuendelea kufanya utafiti, hapa haijatajwa sasa mamlaka atakuwa hana ruhusa ya kuweza kumuongezea muda.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama hii ni biashara, kama umeshafanya ugunduzi maana yake ulichopewa sasa kuza, fursa uliyopewa ni ya miaka mitatu, kusema kama aah! sasa hiki nilichokigundua.

Ukisoma mfano kwenye kifungu cha 62(4), endapo mmiliki wa leseni ameona kwamba ugunduzi hauna faida ya biashara, kutokana na tathmini za kitaalamu na kiuchumi zilizofanywa katika eneo ambalo ugunduzi umefanyika, mmiliki wa leseni hiyo atarejesha eneo la ugunduzi. Sasa huwezi ukamuachia mtu afanye muda mrefu, achukue muda, kwa sababu kama yeye ameona hakuna ugunduzi basi ni vyema ndani ya kipindi cha miaka mitatu tumpe mtu mwengine aje, sasa hatuwezi tuka-*renew* ile leseni ili yeye afanye huo ugunduzi, kama je hichi nilichokigundua kitaniwezesha mimi kufanya biashara, na ndio maana hatukuweka muda tumembana kwenye muda maalumu wa miaka mitatu Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria Mhe. Mwanasheria Mkuu hajanifahamu, kwa sababu ya vitu viwili. Jambo la kwanza mamlaka ambayo inayosimamia suala hili lote imeshatoa muda wa miaka mitatu, lakini hiyo kampuni inaendelea kufanya utafiti au inataka kufanya utafiti, lakini mamlaka itakuwa hairuhusu tena ile kampuni kuendelea kwa sababu ule muda wa miaka mitatu umekwisha. Lakini hizi tafiti kwenye *off shore* zinaweza kwenda hata miaka mitano, kwa sababu ni eneo kubwa linakwenda kilomita tano kwenda chini. Hatuongelei nchi kama za wenzetu za Kuwait au Oman, unapotaka kwenda mita 400, pengine mita mia 800 au 900 tayari unakuta mafuta yapo. Huu tunaofanya sasa hivi ni utafiti kwenda kutafuta, unampa mtu miaka mitatu. Sasa mamlaka katika kipindi kile cha miaka mitatu ikishafika, inabidi yule unam-*cancel* aondoke. Ninachokisema hapa mamlaka ipewe nafasi, kama yule mtu anataka kuendelea kufanya utafiti basi asilete maombi mapya, mamlaka iwe na uwezo, hapa hajatolewa mtu kupewa kitalu, ni suala la utafiti, kwa sababu mwisho wa siku ni serikali ndiyo itakayofaidika na hizi tafiti zenyewe, mimi hoja yangu iko hapo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Simai Mohamed swali lake.

Katika ku-*create efficiency* na *effectiveness* na ndio maana pale Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa akifafanua, alikuwa anasema tumebana, kwa sababu kama utamuachia mtu muda mrefu kufanya utafiti, basi ataendelea tu kufanya utafiti hata kama amemaliza, hawezi, hawezi kusema kwa sababu yeye pengine ana mambo yake, lakini kama umembana maana yake atafanya kwa muda ule ambao umempa. Lakini uzoefu unaonesha kabisa, kwa sababu ilivyoandikwa hii watu wame-*study* katika maeneo tofauti, wengine wametembea lakini wamesoma sheria za wenzetu. Kwa hivyo, unaona kabisa kwamba ili uweze kuyagundua ni muda gani, lakini hata hayo makampuni mengine baadhi unapoongea nao wanaonesha kabisa ile *indication* ni muda gani unaohitajika katika kufanya shughuli hii. Kwa hivyo, ni vigezo ambavyo vilichukuliwa ili kufikia hapa tulipofika. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Naam! Mhe. Simai Mohamed hii ni mara ya tatu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Naelewa.

Mhe. Mwenyekiti: Haya.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, lengo hapa ni kujenga. Sasa ikiwa Mhe. Waziri anasema kwamba wameangalia sheria tofauti, lakini ukiangalia katika sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kifungu cha 65(1) na 66(1), hii ruhusa imepewa kwa mamlaka. Sasa katika kifungu hiki mimi naamini tutawakimbiza wawekezaji, kwa sababu hapa muda unakuwa tayari umeshaufunga, tafiti hizi katika *off shore deep water* ni kitu kipya, lakini ikiwa Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri wote wanataka hii ibakie, *in shaa Allah*, tuendeleeni, lakini watarudi hapa baada ya miaka miwili.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii tutastahamiliana kwa sababu huo upitishaji wa leo Mhe. Mwenyekiti, itabidi tuwe kama tunacheza mduara, tunakwenda mbele halafu tunarudi nyuma.

Mhe. Mwenyekiti mimi hoja yangu ipo katika kifungu namba 53 ambacho kinazungumzia kwamba kwa mujibu wa kifungu 53 (2), Waziri ndani ya siku 60 baada ya tarehe ya kupokea maombi atamjulisha muombaji uamuzi wake wa kutoa au kutokubali kutoa leseni.

Hoja yangu ni kwamba nilikuwa naona kama huu muda ambao Waziri amepewa ni mdogo, kwa sababu ukiangalia muda ambao Waziri ametoa kutoa ruhusa kwa ile *survey* ya mwanzo ni siku 90. Lakini *survey* imeshafanyika sasa Waziri anataka kumruhusu muombaji aje kuchimba mafuta anapewa siku sitini za kufikiria, *survey* ilikuwa 90 lakini kumruhusu imekuwa 60.

Nilikuwa naomba pendekezo langu iwe siku120 ili tumpe Waziri muda wa kukaa na kufikiria na kumaliza vikao vyote vinavyomuhusu, ili wakati wanapofanya maamuzi wasikurupuke kama wanavyokurupuka siku nyengine, ili haya maamuzi yatoke ambayo yana manufaa na wananchi wa Zanzibar. Nilikuwa naomba hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hiyo lugha ya kukurupuka hiyo sio lugha nzuri sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Wanu lakini hapa angetambua kama tayari kazi zote zile za kuipekua ile kampuni imeshafanyika huko nyuma, na mamlaka baada ya kutimia kuwa ile kazi maombi haya sasa yamepelekwa kwa Mhe. Waziri, hapa kinachombana ni ule muda wa Mhe. Waziri, kutoa maamuzi, kwa sababu na hii ni biashara na watu wamekuja kuwekeza lazima wajue ndani ya muda maalumu, ni kipindi gani Waziri atatoa maamuzi. Sasa ndani ya kipindi cha siku 60 sisi tunaona ni *reasonable* kama inamtosha Waziri kutoa maamuzi, usimuwachie muda mrefu Mhe. Waziri akaweka wawekezaji ambao tayari wanataka kujua kama je maombi yetu ya leseni yamekubaliwa au yamekataliwa.

Kazi nyengine zote zitakuwa zimeshafanywa na Mamlaka mpaka kufika kumpelekea maombi Mhe. Waziri basi mambo mengine yote yameshafanywa na ndio maana wakaridhika, wakampelekea Mhe. Waziri ile ruhusa ya kutoa maombi, sasa hapa ni kumbana Waziri ule muda kama asichukue muda wa siku 60 akawa bado anafanya mambo mengine bila ya kutoa maamuzi, atoe maamuzi kwa muda wa siku 60, na hili tunadhani ni jambo la muafaka Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na kwamba wao ndio wanaofanya kazi, na wao ndio wanaojua hizo siku ngapi ambazo wanaweza wakachukua kutoa maamuzi, lakini *practice* ya sheria za wenzetu hata ukiangalia sheria ya Nigeria, Libya, na nyenginezo unakuta ni 120 *days*, sasa sijui mwendo kasi gani ambao SMZ wanao wa kuweka 60 *days* ya kumpa muda Waziri kutoa maamuzi, sijui hawa wenzetu labda wanafanya kazi zaidi ya hizo Serikali nyengine.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti nimemfahamu na ufafanuzi wangu ni ule ule ambao tayari nimeshautoa, kama kwenye hili mawazo yetu sisi ni hayo kama hatuna haja ya kuchukua muda mrefu, Waziri lazima na yeye ajue amewekewa *specific time* ya kutoa maamuzi, na hii ni biashara na wale wanaokuja kuwekeza na wao wana mambo mengi wanataka kujua. Sasa usimfunge mtu siku 120 unamuweka tu hukutoa jawabu ama umempa leseni au hukumpa, muamulie tu, ndio maana tumeweka siku hizi 60 Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee tuwaachie Mawaziri wakaamue tu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sijui mara hii nitafanikiwa. Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 65(2) ambacho kinazungumzia Waziri hatokataa ombi la leseni ya uendelezaji iliyoelezwa chini ya kifungu hicho, na chini ya kifungu hichi isipokuwa kama *notice* imetolewa na muombaji juu ya nia ya kukataa kutoa leseni na kueleza sababu za kukataa huku.

Ukiangalia kifungu hicho kama inavyosema kwamba Waziri haruhusiwi kumnyima leseni hadi iletwe *notice* kwa muombaji, lakini muombaji anatakiwa pia apewe muda wa kujieleza.

Samahani kifungu cha 65(2) leseni ya muombaji, kwa hivyo basi hapo Mhe. Mwenyekiti, muombaji anatakiwa apewe muda wa kujieleza na kumpa muda wa kurekebisha sababu za kumnyima leseni, ukishindwa kujitetea au kurekebisha makosa ndipo leseni isitolewe bila ya kuwa na haki ya kujitetea na kurekebisha makosa itawakatisha sana wawekezaji, kwa sababu tayari huku mbele tunabana sana katika maeneo tofauti.

Katika kifungu hichi hichi ukiangalia sheria ya Jamhuri nafikiria ya mwaka 2015 kifungu 69(2)b wameweka katika haki hii ili kuweza kupata haki kwa pande zote mbili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nimemfahamu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai Mohammed Said, sasa sikumfahamu pendekezo lake ni nini, maana ameeleza na ame-*quote* Sheria ya Tanzania, sasa pendekezo lake ni nini ili tujue hicho ambacho anakipendekeza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti hapa ni kwamba patafutwe njia ya lugha ya kisheria kurekebishwa kwa sababu hapa inazungumziwa upande mmoja tu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo pendekezo ulitoe hapa kwa sababu tukisha kupita kama halijatoka hapa itapita kama ilivyo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Nililete wapi pendekezo?

Mhe. Mwenyekiti: Hilo pendekezo lako.

Mhe. Simai Mohammed Said: Aa niliseme, *okay*.

Mhe. Mwenyekiti: Ulitoe ili Serikali ilikubali au ilikatae hapa hapa. Naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Hapana Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu sana hapa ni pahala muhimu sana hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa mimi nimejaribu kukusaidia umekaa kimya Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Sawa nilikuwa bado sijairekebisha hapa kwa sababu sijui kifungu kipi, vipo vingi hivi vifungu, sasa naomba nisome basi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba tuendelee.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naangalia kifungu namba 114 uondoshaji wa mali za kampuni.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kifungu cha ngapi, samahani kifungu cha ngapi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Kifungu namba 114.

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika huko.

Sehemu ya Nne

Shughuli za Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Sehemu hii imeanzia Kifungu 33 hadi 109 Pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tutalirudisha Baraza kwa ajili ya kuhoji muda ili tuweze kuendelea mpaka tumalize.

Wahe. Wajumbe: Tutawahi.

Mhe. Mwenyekiti: Tutawahi sawa tuendelee.

Sehemu ya Tano

Ukomo wa Shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Sehemu hii inaanzia Kifungu cha 110 hadi 117 Pamoja na Marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Hapana nimemuona Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii hapa naomba tufanye marekebisho ya lugha hapa au nipate maelezo ya neno hili liliopo.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu cha ngapi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Kifungu No.114 inasomeka hivi endapo leseni imewasilimishwa hebu iangaliwe naomba Mwanasheria atueleze hapa hili neno limekusudiwa nini au kama si hivyo liondoke.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kuna rekebisho linahitajika hapo la kwenye sentensi neno la tatu nadhani kwenye hiyo sentensi, endapo leseni imewasilishwa lakini limeandikwa nafikiri kuna makosa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Tunakubali nadhani ni *typing error,* tutaitizama ile ya Kiingereza halafu tutafanya tafsiri, nadhani imewasilishwa imekusudiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mheshimiwa tuendelee.

Sehemu ya Tano

Ukomo wa Shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Sehemu hii inaanzia Kifungu cha 110 hadi 117 Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Afya na Usalama Kazini na Misingi ya Mazingira

Sehemu hii inaanzia kifungu cha 118 mpaka kifungu cha 133 pamoja na marekebisho yake

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi tena hoja yangu ipo katika kifungu cha 126 ambacho kinasema, kampuni Mkandarasi na mtu mwengine yeyote atawajibika kwa uchafuzi wa mazingira bila ya kujali kushindwa kwake. Ambayo ya kizungu inasema: *shall be liable for pollution damage without regard to fault.*

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba katika hili ile *fault* itizamwe kwa sababu saa nyengine wananchi wanafanya uzembe wa makusudi na inaweza ikaja ikapelekea yule ambaye mkandarasi sijui au kampuni yule ambaye anafanya ile shughuli imuingize kwenye *liability*, sasa nilikuwa naomba kwamba hii Sheria hapa iseme kwamba *fault* ile ya mkandarasi sijui au ndio nani iangaliwe. Yaani iwekwe katika *consideration* halafu ndio wamhoji sio kwamba wamfanye awe *liable* bila ya kuangalia ile *fault* yenyewe ambayo imetokea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nimemfahamu lakini nadhani kama angesoma kifungu cha 126(2) nadhani kingekidhi hiyo haja yake ambayo Mhe. Wanu ameisema, lakini pia tutambue kama haya makosa *of course* yanaamuliwa kulingana na ukubwa wa lile jambo ambalo limefanyika, sasa wale ambao wamepewa dhamana ya kutoa adhabu hizi pia wamepewa dhamana ya kupima ukubwa na huo udogo, na ndio maana wakaachiwa sasa wawe na nafasi ya kutoa maamuzi na kutoa adhabu kwa namna ya kiwango ambacho wao wataona mtu huyu amekosa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini hata sheria ya mazingira yenyewe ile inasema kwamba lazima *liability* iangaliwe na iwe ya yule ambaye amesababisha ile *fault* yenyewe ndio awe *liable*. Lakini sheria hii inasema kwamba haitoangalia hiyo *fault* yenyewe ilikuwa ya nani isipokuwa itamtia yule ambaye ameharibu mazingira moja kwa moja katika kosa.

Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mwanasheria Mkuu waangalie, yaani sheria iseme tu kwamba ita-*consider* ile *fault* ambayo imefanywa kuliko kumuacha hivi hivi, wakati mwengine wananchi wetu tunawajua kwani si yanatokea hapa

wanakatazwa wasikae mabondeni, wanakwenda wanakaa na baadae wanailaumu Serikali wakati kosa ni la kwao waliokwenda kukaa mabondeni. Kwa hivyo na hili nalo liangaliwe kwa jicho lile lile ambalo Serikali inaingia katika lawama.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema awali kama ukitizama msingi wa Sheria hii ni kwamba unataja vitu vitatu. Kwanza ni kampuni, pili mkandarasi na tatu inataja mtu mwengine yeyote ambaye atahusika katika uchafuzi huo wa mazingira, sasa yatakapotokea haya yule ambaye amepewa dhamana ya kutoa adhabu hizi basi atapima kile kiwango cha uchafuzi wa mazingira ambao umetokea na yeye ndio mwenye dhamana ya kutoa hiyo adhabu. Sasa hapa hakuwekewa hicho kiwango kwa sababu ameachiwa yeye a-*determine* kile kiwango na atoe adhabu ambayo inatakiwa Mhe. Mwenyekiti.

Sasa anachosema Mhe. Wanu na tunachosema sisi nadhani ni yale yale tu, ni sawa sawa nadhani tunachokizungumza ni kitu kimoja.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, hata hao wanaowaachia ku-*determine* kuangalia ile *punishment* yenyewe siku hizi nao wanalalamika, Mahakama zinakuwa zinalalamika sana siku hizi kwamba Sheria zinawaachia wazi sana, na saa nyengine wanashindwa kosa jepesi lakini sheria inabana *punishment* inakuwa kubwa inabidi yeye a-*determine* alivyoamka, lakini sheria zinavyokuwa wazi kama ambavyo ninavyopendekeza kwamba *at least* ili *fault* iangaliwe, inakuwa afadhali kuliko ukiacha hivi wazi kama ilivyokuwa.

Nilikuwa namuomba Mwanasheria Mkuu akubali tu kwamba hapa kosa ambalo yule mkandarasi au mtu yeyote atakayefanya ile *fault* bila ya kuwaachia hao wanaotoa *punishment* wa-*determine* wenyewe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimjibu Mhe. Wanu kama mwenzangu alivyojibu kwamba kama yuko makini kusoma hichi kipengele nafikiri tumeangalia pande zote mbili na tumeona athari yake, ndio maana ukifuata hiki kipengele unaona kabisa nani anabeba dhima kati ya mkandarasi lakini kuna mtu mwengine, ukisoma hivi vipengele vimechanganua vizuri.

Mimi naomba atulie, asome vizuri ili aelewe, lakini nafikiri uchambuzi umetoka wa kutosha na hichi kipengele kimekaa vizuri, kwa sababu anachokizungumza ndicho tulichokizungumza na ndicho kilichopo lakini

tunakitizama kwenye *concept* tofauti. Kwa hivyo mimi naomba akubali na aridhie tu hichi kifungu kibakie kama kilivyo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti nimesikia maelezo ya Mhe.Waziri, na kwa taarifa yake tu nimjulishe kwamba nimesoma, nimekaa nikaelewa na ndio maana nikaja na hii hoja, lakini *at the end of this*, sheria haiendi kumfaa baba yangu wala mama yangu, tuendelee.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Wakati nilipokuwa nikichangia hoja hii nilikuwa nazungumzia suala la usalama, kwa hivyo hapa kuna kipengele namba 118 kinachozungumzia afya na usalama kazini, sasa hapa usalama una maana pana sana, lakini mimi nilitaka kujua vipi usalama wa wale wanaofanya kazi wakiwa kule baharini, pamoja na wenye kampuni pale na mali zao usalama wao ukoje, Serikali imeangalia vipi katika suala la usalama wa wafanyakazi na mali zao wakiwa baharini kule wakiwa katika kazi za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti naomba arejee swali sikumfahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri msikilize kwa makini.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Wakati nilipokuwa nikichangia nilielezea suala zima la usalama wa wafanyakazi na mali zao za kampuni wakiwa kazini, sikupata ufafanuzi watu hao watakuwa na usalama gani wakati wako bahari kuu kutenda kazi zao hizo za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Katika hili la ulinzi na usalama wa watu na mali zao uko katika utaratibu chini ya Mamlaka zinazohusiana na ulinzi na usalama, na imeelezwa wazi kifungu na limewekwa hili kwa sababu, wakati mwengine katika kazi hizi kunatokea mambo mengi, inaweza kutokea ajali kinaweza kutokea kitu chengine. Kwa hivyo kampuni husika itachukua jukumu.

Pia kwa upande mwengine kwamba ile kampuni mama itasimamia kwa maana ya kwamba utekelezaji wa zile shughuli na ufuatiliaji.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, bado sijapata jawabu la makusudio yangu. Usalama wa wafanyakazi pale wanapofanya kazi kama wataumia, nakusudia kwa sababu wako mbali na nchi kavu, kwanza kuna maharamia wanaweza kutokezea pale wakavamia sehemu ile pale, wakaweza kushindwa

kufanya kazi zao huu ndio usalama ninaokusudia mimi, ndio ninataka kujua vipi nchi imejipanga katika masuala haya, na tukiangalia nchi yetu sasa hivi ina mipenyo wanaweza kutuingilia maadui.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama nimemfahamu Mwenyekiti wa Baraza Shehe Hamad Mattar kama angesoma kifungu cha 119 ambacho kinazungumzia sasa Kampuni na Mkandarasi au mtu mwengine yeyote anayeshiriki katika shughuli za mafuta na gesi asilia, wakati wote atadumisha maandalizi ya kuchukua hatua za dharura kwa lengo la kukabiliana na ajali na dharura ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa maisha, majeraha, uchafuzi wa mazingira au madhara makubwa kwa mali.

Sasa utaratibu avisome vifungu hivi vyote, ataona utaratibu gani umewekwa wa kulinda yale ambayo yeye anayazungumzia. Yeye amesoma kifungu cha 118 tu.

Mhe. Mwenyekiti: Kama nitakuwa nimemfahamu vizuri Mhe. Mattar ulinzi alioukusudia mfano *oil rig*, kisima kiko mbali kiko nje, *offshore* sijui *whatever*, *onshore* sijui mnaita kiko mbali baharini, kina ulinzi wa eneo la ile shughuli yenyewe ndio usalama huo nadhani aliokuwa anau-*refer*.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, *of course* kwanza hilo ni dhamana ya ukiacha ya Serikali lakini ya yule mwenye mali mwenyewe, kama yeye lazima ahakikishe kwenye maeneo yake ambayo amewekeza kuna ulinzi wa kutosha. Kwenye yale maeneo yake ambayo amewekeza yeye dhamana yake ya kwanza ni kuhakikisha kwamba kuna ulinzi wa kutosha, ukiacha hayo lakini pia sheria imekwenda mbali na kuhakikisha kwamba sio mali tu lakini hata wale ambao wanatakiwa wafanye kazi kwenye maeneo yale basi Kampuni au Mkandarasi inatakiwa achukuwe juhudi ya kuhakikisha pia usalama wao kwenye maeneo yale.

Sasa yote mawili Mhe. Mwenyekiti, yameelezwa, ni kuvisoma tu vifungu hivi vyote ili kujua kipi kinazungumzia nini na kipi kinazungumzia nini.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mheshimiwa nimeelewa tuendelee.

Mhe. Omar Said Abeid: Mimi niko 131(2) jana niliomba ufafanuzi napenda kuisoma hiyo:

"Endapo tathmini ya athari ya mazingira itahitajika au masharti yanahitaji kutimizwa kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa mazingira ya

Zanzibar na sheria nyengine husika, muombaji leseni au ithini atatimiza masharti au matakwa".

Nilitaka nipewe ufafanuzi wa neno ithini.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Hii iliyokusudiwa ni idhini nadhani ni *typing error.*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, wajumbe naomba wasome pamoja na marekebisho ya Kamati, Kamati uliipa siku 6 kuifanya hiyo kazi.

Sehemu ya Sita

Afya na Usalama Kazini na Misingi ya Mazingira

Sehemu hii imeanzia kifungu cha 118 hadi kifungu cha 133 pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Saba

Thamani ya Wadau wa ndani Jukumu la Ushirikishwaji wa Jamii na Kiapo cha Uadilifu

Sehemu hii imeanzia kifungu cha 134 hadi kifungu cha 138 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, niko kwenye ukurasa wa 125 kwenye kifungu cha 145(g), pamoja na maelezo yote mazuri adhabu iliyotolewa ya dola 20,000 na miaka 5 ni ndogo sana. Adhabu hiyo astahiki kupewa angalau miaka 10 ili mtu akome kutoa taarifa hizi au kufanya vitendo visivyokuwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Naona kama umewahi Mheshimiwa ni sehemu ya 8, kwa hivyo naihoji sehemu ya 7.

Sehemu ya Nane

Makosa na Adhabu

Katika sehemu inaanzia kifungu cha 139 mpaka kifungu cha 146 pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tisa

Utatuzi wa Migogoro

Sehemu inaanzia kifungu cha 147 hadi kifungu cha 150 pamoja na arekebisho yake.

Sehemu ya Kumi

Masharti ya Mpito

Katika sehemu hii inaanzia katika kifungu cha 151 mpaka kifungu cha 155.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Katika sehemu hii kwa sababu uandishi wa sheria uko tofauti sitaki kujenga hoja, lakini maelezo ya Mwanasheria Mkuu pengine yatanisaidia na mimi katika kuelewa uandishi wa sheria. Katika sehemu ya Kumi na Moja kumewekwa jadweli la kwanza lakini jadweli la kwanza hili linaongelea mwenendo wa Bodi ambao upo chini ya kifungu cha 16

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe Sehemu ya Kumi ina kifungu kimoja tu cha 151.

Sehemu ya Kumi na Moja

Masharti ya Jumla

Katika sehemu hii inaanzia kifungu cha 152 hadi kifungu cha 155 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, sipotezi nguvu kurudia yale ambayo nimeyasema nadhani nimesema muda mfupi kabisa. Ninachotaka kujua kwa nini hii jadweli la kwanza linazungumzia mwenendo wa Bodi, kwa nini huu mwenendo wa Bodi usiingie kwenye *provisions* kule chini ya kifungu cha 16 na badala yake kimekuja kuwekwa kwenye jadweli hili la kwanza. Kama nilivyosema sibishi uandishi wa sheria uko mwingi labda maelezo ya Mwanasheria Mkuu pengine yanaweza yakanielimisha na mimi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa ninakushukuru na kama ambavyo Mhe. Wanu alivyosema ni uandishi wa sheria ambao umetumika, kama wakati mwengine unapotumia haya majadweli unakuwa unampa uwezo Mhe. Waziri wa kuweza kufanya marekebisho bila ya kuja kuomba ridhaa ndani ya Baraza

la Wawakilishi. Sasa ni utaratibu tu ambao unatumika. Mara nyengine unaweza kuona mambo haya tumeyaingiza ndani ya *substantive provision* ambavyo vimo ndani ya sheria. Lakini mara nyengine tunaandika jadweli ambalo sasa linatoa muongozo, yote yanatumika inategemea tu unatumia kwenye mazingira gani. Lakini ikiwepo hapa sidhani kama inaleta dhara yoyote, kama ambavyo ikiwepo ndani ya sheria yenyewe. Ni utaratibu tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Mwanasheria lakini kwa ushauri ili kuweka mtiririko mzuri wa sheria hii na Baraza la Wawakilishi lionekane kwamba limefanya mambo kwa tungo, kwa nini hili jadweli la kwanza lisiingie kwenye *substantive provision* halafu majadweli yakabaki kama tulivyozoea.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ukiliangalia vizuri jadweli la kwanza ni mwenendo wa Bodi chini ya kifungu cha 16, imeandikwa imo kwenye mabano.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Nimefahamu Mhe. Mwenyekiti, lakini ninavyosema kwa nini tusiache majadweli yakawa majadweli na *provisions* zikawa *provisions* kwenye sheria yenyewe.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema kama haya majadweli yanatengenezwa kutokana na masharti ambayo yamewekwa kwenye sheria na kifungu cha 16 ndio kimetoa uwezo wa kutengeneza haya majadweli. Sasa mimi nilichosema kwamba huu ni utaratibu ambao lazima utaratibu wake sasa ili uyaelezee mengi unachukua utaratibu wa kutengeneza jadweli. Kwa sababu ungeweka ndani ile ya *substantive provision* siku nyengine ungechukua muda mrefu katika kuvielezea hivi vifungu lakini ndio maana tumeweka humu ndani, kama inakuwa rahisi kuweza kulifanyia hata marekebisho jadweli hili.

Sasa mimi sijaona Mhe. Wanu hoja iko wapi kwenye utaratibu huu ambao umewekwa kama haufai au unafaa, mimi sijaona hoja yake Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nakubali sina hoja na tuendelee.

Sehemu ya Kumi na Moja

Masharti ya Jumla

Katika sehemu hii inaanzia kifungu cha 152 hadi kifungu cha 155 pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa naomba niwahoji kwa wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia 2016

(Kusomwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia mwaka 2016 usomwe mara ya tatu.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa naomba niwahoji kwa wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Ahsante waheshimiwa, Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kupitisha Mswada wa Sheria ya Mafuta na Gesi, lakini pia niipongeze sana Serikali kwa namna ambavyo

wameweza kusimamia shughuli hizi. Pia lakini nisiache kukushukuruni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe wote kwa pamoja, Kamati ambayo imesimamia jambo hili pamoja na nyinyi wengine wote ambao mumeshiriki katika kuliboresha hili suala na hatimaye tumeweza kulipitisha hapa kwa pamoja.

Jambo hili ni la kihistoria na bila shaka litapoanza kufanya kazi vizazi vijavyo vitatukumbuka kwa siku ya leo kuweza kubadilisha kupitisha sheria hii.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo machache, na kwa kuwa hatuna shughuli kwenye *order paper*, naomba nichukuwe nafasi hii sasa kuahirisha shughuli za Baraza la Wawakilishi, mpaka kesho siku ya Jumatano saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 1.30 usiku Baraza liliahirishwa hadi
Jumatano tarehe 28/09/2016 saa 3.00 asubuhi)